

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA SABA

Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 22 Juni, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile.

Na. 437

**Sheria ya Kuwalinda wafanyakazi wa  
Mahotelini na Majumbani**

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE (K.n.y. MHE. USSI SALUM  
PONDEZA AMJADI)** aliuliza:-

Sheria ya kuwalinda wafanyakazi wa mahotelini na majumbani imekwama kutungwa Zanzibar na Tanzania Bara kutokana na Azimio liliofikiwa na Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (*ILO*) kutoridhiwa na Bunge tangu Mkataba kusainiwa mwaka 2011, mkataba ambao unataka kila nchi

mwanachama kuwa na Sheria ya kulinda haki za wafanyakazi hao:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha azimio hilo kutowasilishwa Bungeni tangu Tanzania iliposaini Azimio la *ILO* wakati nchi nyingine zimeanza utekelezaji wake zikiwemo za Afrika Mashariki?

(b) Kwa kuwa Zanzibar haiwezi kutunga Sheria zake za kulinda haki za wafanyakazi wa mahotelini na majumbani mpaka azimio hilo lipelekwe na Ofisi yako Bungeni na kuridhiwa ndiyo kila upande utunge Sheria zake kutohana na mambo ya kazi kuwa sio ya Muungano: Je, ni lini Bunge litapokea azimio hilo la kulinda haki za wafanyakazi hao?

(c) Je, Serikali inawaeleza nini Vyama vya Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani ambao walianza kufanya matayarisho ya utekelezaji wa azimio hilo, lakini wamekwama kutohana na mkataba huo kutoridhiwa na Bunge tangu kuafikiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa mwaka 2011, nchi wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ikiwemo Tanzania, zilipitisha Mkataba wa Kimataifa kuhusu kazi za staha kwa wafanyakazi wa majumbani (*Convention No. 189 on Decent Work for Domestic Workers*). Hadi sasa nchi zilizoridhia mkataba huu ni 23 kati ya nchi wanachama 189. Kwa upande wa Afrika ni nchi mbili tu zilizoridhia ambazo ni Afrika Kusini na Mauritius. Serikali inaendelea kupitia kwa makini sana maudhui ya mkataba huo ili kufanya maandalizi ya kuuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya kazi na ajira siyo ya Muungano. Tanzania ina Sheria za Kazi, hali kadhalika na Zanzibar pia wana Sheria za Kazi ambazo zinawahusu wafanyakazi wote wakiwemo wafanyakazi wa mahotelini na majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inazo sheria mbalimbali zinazotambua na kusimamia maslahi ya wafanyakazi nchini, wakiwemo wafanyakazi wa majumbani, wafanyakazi na vyama vyao waendelee kutambua juhudzi za Serikali na kulinda na kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi kuititia sheria, kanuni na taratibu tulizonazo. Serikali itaendelea kuelimisha jamii na wadau mbalimbali kuhusu mifumo, maudhui na taratibu za uridhiaji wa mikataba ili kufanya maandalizi stahiki kabla ya uridhiaji wa mikataba hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nimesikiliza kwa makini sana majibu ya Mheshimiwa Naibu Wazir; swali langu la kwanza: Je, ni lini sasa Serikali italeta azimio hilo Bungeni kuweza kuitishwa? Maana amesema kwamba ni nchi mbili tu ambazo zimepitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; sisi Tanzania tuna Sheria ya Kazi nadhani ya mwaka 2004. Je, ni lini sasa kulingana na mazingira ya sasa mtaileta tena ili iweze kufanyiwa mapitio?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza ameuliza, ni lini? Katika majibu yangu ya msingi, nimesema Serikali bado tunaendelea kuititia maudhui ya

mkataba huu ili baadaye baada ya kujiridhisha tuweze kuuleta kwa ajili ya kuwa *ratified*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *Convention* hii namba 189; katika utaratibu wa hizi *Conventions* huwa pia wanatoa vitu vinaitwa *recommendation*. Katika *Convention* hii kuna *recommendation* namba 201 ambayo inatoa mazingira ya nchi zile wanachama kuona namna bora ya kuweza kuandaa baadhi ya *mechanism* ili mikataba hii iweze kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mambo mengi ambayo yapo katika mkataba huu tayari yapo ndani ya sheria zetu. Ukiangalia katika *article* ya kuanzia 13 mpaka 18 imezungumza kuhusu masuala ya *Freedom of Association*, masuala ya mikataba ambayo kwa mujibu wa sheria zetu, tayari yako *covered*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika nchi kama Kenya, ziko baadhi ya *Conventions* ambazo hawajazi-*ratify* kwa sababu wanaona sheria yao ni nzuri zaidi kuliko ile mikataba. Kwa hiyo, nasi bado tunaona kabisa kwamba yako maeneo mengi sana ambayo sheria yetu ime-*cover*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni mapitio ya sheria. Kwa mujibu wa utaratibu wa masuala ya kazi, sisi tunafanya kazi katika mfumo ambao tunaita ni *tripartism* kwamba ni Serikali, Waajiri na Wafanyakazi. Inapotokea kwamba kuna jambo lolote ambalo linahitaji marekebisho au mapitio ya sheria, wadau huwa wanafanya taratibu hizo. Nasi kama Serikali mara zote tumekuwa *flexible* kuhakikisha kwamba sheria zetu za Kazi zinakuwa *intact* ili ziwe msimamizi mzuri katika masuala ya kazi katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Roman Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na kusubiri mapitio ya huo mkataba, lakini hapa nchini pana vikundi mbalimbali vyatatu vinawakusanya watoto wetu wa nchi hii kwa minajili

ya kuwatafutia kazi za ndani nchi za nje. Habari tulizonazo ni kwamba baadhi ya hawa watoto wamekuwa wakinyanyasika, wakiteswa na hata kuuawa. Je, ni hatua zipi za wazi ambazo Serikali inazichukua kwa ajili ya kudhibiti vikundi hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA**

**NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge hapa alikuwa anazungumzia wale mawakala wa ajira ambao kwa namna moja ama nyingine, yamekuwepo malalamiko mengi sana ya kuwapeleka mabinti zetu katika nchi hasa za Uarabuni kwenda kufanya kazi za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alishatoa agizo na tangazo la kwamba wale wote ambao wanakwenda kufanya kazi nje ya nchi wapitie mfumo ambao upo katika Wizara yetu kuititia Wakala wa Ajira wa Serikali ambaye ni *TAESA*. Sasa tukibaini kwamba wako watu ambao wanafanya kazi hii kinyume na taratibu, sheria zetu ziko wazi, huwa tunawafutia usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumekuwa tukiwachukulia hatua kuhakikisha kwamba hawapati tena *registration* ili tuhakikishe kwamba nguvu kazi yetu hii wakienda kufanya kazi nje ya nchi tuwe tumewalinda kwa maana ya haki zao za kimsingi, tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo wako baadhi ya Watanzania ambao hawapitii katika Ofisi yetu na wakienda nje ya nchi wakipata manyanyaso tunakuwa hatuna taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata Balozi zetu zimeweka utaratibu mzuri; ile mikataba inayotolewa pale, mwajiri yeoyote wa nje ya nchi ambaye anamtaka mfanyakazi wa Tanzania lazima apitie katika Ubalozi na Ubalozi unawasiliana nasi kwa ajili ya kuandaa mikataba ili tumlinde na tulinde haki za mfanyakazi wa Kitanzania.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 438

**Kuboresha Maslahi ya Walimu Nchini**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliliza:-

Serikali imekuwa na dhamira ya dhati ya kuboresha maslahi ya Watumishi hususan Walimu kwa kutoa nyaraka mbalimbali ikiwemo Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 3 wa tarehe 20/10/2014 unaohusu mishahara na Posho ya Madaraka kwa Viongozi wa elimu (*Responsibility Allowance*):-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kutekeleza waraka huo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa Posho ya Kufundishia (*Teaching Allowance*) ili kuleta ufanisi wa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Serikali ilianza kutekeleza Waraka Na. 3 wa mwaka 2014 tangu tarehe 1 Julai, 2016 kuhusu Posho ya Madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu wa Elimu Kata. Walimu Wakuu wanalipwa sh.200,000/= kila mwezi na Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata wanalipwa sh.250,000/= kila mwezi. Kwa mwezi mmoja, Serikali inatumia takriban shilingi bilioni 5.01 kwa ajili ya kulipa Posho za Madaraka kwa viongozi hao kwa ajili ya kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya kufundishia ilijumuishwa katika Mshahara wa Walimu ili kuboresha maslahi ya Walimu wanapostaafu. Hata hivyo, Serikali hivi sasa kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora inafanya mapitio ya kazi kwa watumishi wote nchini ili kuboresha maslahi kwa kuzingatia uzito wa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa hatua hiyo. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tangu mwaka 2016 mpaka sasa hakuna ongezeko lolote la mshahara kwa watumishi. Serikali inatoa tamko gani kwa watumishi hawa ambao wamekuwa na moyo mkubwa sana wa kujitolea?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tangu mwaka 2016 mpaka sasa hakuna kupandishwa daraja kwa mtumishi yeoyote hususan Mwalimu. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kulipa malimbikizo ya mshahara kwa Mtumishi ambaye alistahili kupanda mwaka 2016 mpaka sasa? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya rejea ya takriban siku mbili, Mheshimiwa Waziri anayehusika na mambo ya Utumishi (Waziri wa Utumishi na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) alitoa maelekezo hapa kwamba katika hoja yetu ya Bajeti Kuu ilivyokuwa inapita watu walikuwa wanasema kwamba kwa nini sasa fungu hili la mshahara halipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba Mheshimiwa Rais alizungumza wazi alipokuwa katika viwanja vya Mkoa wa Kilimanjaro katika siku ya Mei Mosi. Jambo hili limezingatiwa katika bajeti yetu hii tunayokwenda

nayo hivi sasa. Ndiyo maana hata juzi Waziri wa Utumishi wa Umma alikuwa anatoa maelekezo kwamba kuna nyongeza ya fedha hapa ambayo itaenda ku-*address* jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la kupanda madaraja, hali kadhalika eneo hilo madaraja yalisimamishwa kutokana na zoezi maalum la uhakiki hasa wa vyeti feki na watumishi hewa. Vile vile naomba nifanye rejea ya Waziri wetu wa Utumishi wa Umma alipozungumza wazi kwamba suala la kupanda madaraja sasa limewekekwa utaratibu mzuri, kila mtu atapanda kwa stahiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie kwamba kila mtu atapata stahili yake kwa kadri inavyotakiwa na hili Mheshimiwa Waziri amelizungumza wazi kwa sababu yeye ndiyo anahuksika na Utumishi kwamba kila mtu atapata stahiki yake na jambo hili sasa hivi linakamilika na kila mtu atapanda daraja kama ilivyokusudiwa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ntimizi, swali la nyongeza.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Moja ya matatizo ya Walimu wetu ni kukosa makazi katika maeneo wanayofundishia katika vijiji vyetu. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inajenga nyumba za kutosha kwa Walimu wetu ili kuwapa motisha kufundisha vizuri katika maeneo yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la kuimarisha miundombinu hasa kwa Walimu, ni kweli tumekuwa na changamoto ya nyumba, ndiyo maana hata baadhi ya Watumishi wengine wakishaajiriwa wanakumbana na changamoto kubwa sana ya makazi. Ndiyo maana toka mwaka 2016 katika Sekta ya Elimu

tulitumia fedha nyingi takriban shilingi bilioni 64 kujenga miundombinu ya madarasa, vyoo na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanikiwa katika Shule ya Sekondari; mpango wa MMES II tumejenga nyumba takriban 283. Hata hivyo, naomba nishukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali. Tumeshiriki kwa pamoja kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali, lakini hata hivyo, katika mpango wa Serikali, mwaka huu tutaenda kushirikiana tena na wadau na fungu letu la Serikali kuhakikisha tunaongeza idadi ya nyumba. Lengo kubwa ni Walimu wetu na wataalam mbalimbali ambapo sio kada ya Walimu peke yake, waweze kupata makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hii bado ni changamoto kubwa, lakini naomba tushirikiane kwa pamoja, na Serikali imeweka nguvu za kutosha kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba za Walimu na wa kada nyingine katika maeneo mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Mngwali, swali la nyongeza.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na ninalo dogo sana. Naomba niseme kwamba Serikali isituambie hapa kama vile inaanza upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu zote hizi za kupandisha vyeo na mengineyo yalikuwepo kabla; lakini sasa hivi kilichotokea kibaya, kuna watu walipandishwa cheo wakalipwa mshahara mpaka miezi mitatu, wakasitishiwa mshahara, wakarejeshwa pale pale. Hivi Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kuhusu hili? Naomba njibowiwe kwa ufasaha zaidi ili watu waweze kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana maana ningekosa kupata hili swali, roho ya mama yangu Mheshimiwa Riziki ingepata shida sana kwa sababu nilikuwa namwona hapa, hasa nikijua mama yangu ni Mwalimu, kwa hiyo, alikuwa anataka kujua katika kero hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie kwamba; bahati nzuri juzi nilipata viongozi wa Chama cha Walimu kutoka Mkoa wa Rukwa, nilikuwa nao pale ofisini na hiyo ni miongoni mwa *concern* ambayo walileta pale ofisini kwetu. Ni kweli kuna watu ambao walipata mishahara ile miezi miwili, lakini baadaye mshahara ukakasitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto kubwa ni kwamba kuna wengine wanaenda kustaaifu. Sasa wakistaifu jambo hili linafanyika vipi? Leo hii mtu akistaifu atahesabiwa katika mshahara wa mwanzo wakati alipanda. Ndiyo maana nimesema jambo hili, kama Serikali, tumelichukua kwa uzito wa hali ya juu, tunafanya *analysis*. Kuna watu wengine ambao watastaifu hivi karibuni. Ina maana *tusipo-address* vizuri tutakuwa na changamoto kubwa katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna watu wengine walipanda, lakini kwa sababu ya utaratibu mzuri uliowekwa naomba niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge, jambo hili tumelichukua sisi kama viongozi na tumelijua ni tatizo kubwa, lazima tuliweke vizuri. Yalifanya kwa nia njema kwa sababu huko nyuma hali yetu ilikuwa siyo shwari. Suala zima la watumishi hewa liliikuwa ni jambo kubwa, watumishi takriban 19,000 *plus*, liliikuwa ni tatizo kubwa sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpango huu ulikuwa ni mpango mkakati wa Serikali kusaidia kulinda mapato, lakini kupeleka fedha kwa watu wanaostahili. Kwa hiyo, naomba niwatoe hofu wafanyakazi kwamba kila mtu atapata stahili yake na Serikali inafanya kazi kufanya *analysis* kwa undani zaidi kuondoa hilo tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, swalii la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa niulize swalii la nyongeza. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba *Teaching Allowance* ipo kwenye mshahara. Sasa tunapata tabu sana tukikutana na Walimu wanapotuambia juu ya kurudisha *Teaching Allowance*. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutamka ndani ya Bunge hili ili waweze kutambua kwamba *Teaching Allowance* yao iko kwenye mshahara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa tulilokuwa nalo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa leo wanalizungumza ni suala zima la maslahi mapana ya watumishi. Ndiyo maana hata hicho kilichokuwepo kama kidogo au kikubwa hakioneshi vizuri ni kwa sababu huenda lile fungu lenyewe, *purchasing power* imekuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, juzi juzi kulikuwa na kikao maalum kinafanyika kwa sababu kunaundwa bodi maalum ya kuja kupitia maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha *Teaching Allowance*, kuna mambo mengine; kuna suala la haki za watu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, jambo hili tutakuja kulitamka rasmi sasa baadaye kuhusu mchakato huu unavyokwenda. Hiyo Bodi iliyoundwa sasa kupitia mishahara, siyo kwa Walimu peke yake, isipokuwa watumishi wote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaona jinsi gani kila mtumishi atapata stahili yake na nyongeza kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili tutakuja kulitoleaa tamko rasmi hapa baadaye Bungeni likiwa katika utaratibu mzuri baada ya kutoa hii *documentation* vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Swali la Mwisho, Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuna shule Shikizi nyingi ambazo zina Walimu wa kujitolea na hawapati posho. Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho hawa Walimu wanaofundisha kwenye Shule Shikizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika jambo hili nadhani kila Halmashauri ina mkakati wake *ku-address* matatizo ya watumishi katika maeneo mbalimbali; na kuna baadhi ya maeneo mengine utakuta watu wanatumia *own source* kuonesha jinsi gani wana-*address* hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna mambo *specific* katika eneo la Mheshimiwa Njeza, tutalichukua halafu tuangalie jinsi gani tutafanya kuona nini kimetokea huko ilimradi tuliweke sawa ili kila mtu apate stahiki yake. Kama kuna maeneo mahususi katika Halmashauri husika, basi tutayatoa kwa lengo la kuweka mustakabali mzuri katika maeneo yetu hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Na. 439

### **Kutangaza Utalii uliopo Wilaya Kilwa**

**MHE. ZUBERI M.KUCHAUKA (K.n.y. MHE. VEDASTO E. NGOMBALE) aliuliza:-**

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitangaza Wilaya ya Kilwa kuwa ni moja ya maeneo makubwa ya Kiutalii katika Kanda ya Kusini kwa kuzingatia historia yake, maajabu mbalimbali yaliyopo, fukwe, mapango, malikale, mbuga, mabwawa na utamaduni wake?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Vedasto Edger Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Kilwa ni mionganoni mwa maeneo yenye fursa za uendelezaji utalii wa kihistoria na kiutamaduni yakiwemo magofu ya malikale yaliyopo eneo la Kilwa Kiswani na Songo Mnara ambayo ni maeneo yaliyopo kwenye orodha ya urithi wa dunia pamoja na vivutio vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuitangaza Wilaya ya Kilwa kuwa eneo muhimu la kiutalii Ukanda wa Kusini, Wizara imeandaa jarida la Karibu Kilwa (*Kilwa District Heritage Resources*); vipeperushi kama *Welcome to Kilwa in Tanzania*; ambavyo vinaonyesha picha na maelezo ya vivutio vya utalii vilivyopo Wilayani Kilwa na kuanzisha Kituo cha Taarifa za Kiutalii (*Tourist Information Centre*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Jarida na vipeperushi hivi vinatolewa kwa wageni wanaotembelea Kilwa pamoja na kutumika kutangaza utalii wa Kilwa katika maonesho ya

ndani, hususan maonyesho ya Saba Saba; Nane Nane na Maonyesho ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kuititia Bodi ya Utalii na kwa kushirikiana na taasisi ya nchini Ufaransa imeweza kuandaa filamu maalumu ambayo inaitangaza Kilwa. Filamu hiyo ilizinduliwa rasmi mwaka 2016 na imetafsiriwa kwa lugha tatu za Kimataifa ambazo ni Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa. Filamu hiyo inapatikana kuititia mtandao, kwenye tovuti ya Bodi ya Utalii na kwenye wavutu ya *YouTube*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mpango mkakati mmojawapo ni kutangaza kuingiza hiyo tovuti na filamu. Hapa swali lilikuwa linataka kujua mkakati thabiti wenye dhamira ya kweli kwa sababu hapo wanaposema, hata barabara ya kufika kwenye hivyo vivutio hakuna. Sasa huu mkakati, hata hao watu unaoingiza kwenye filamu, watafikaje kule Kilwa ambapo kwenye hivi vivutio hamna barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba Pwani ya Afrika Mashariki ni mahali ambapo kwanza walikuwa na *currency* yao, yaani walikuwa na pesa yao; ni Kilwa, lakini haya yote watu hawayajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa mfano, ukiangalia Vita ya Majimaji; asili ya vita hii ni Kilwa, lakini makumbusho ya Vita ya Majimaji yako Songea. Sasa Wananchi wa Kilwa walitaka waone, Serikali inafanya taratibu gani kuirudisha Vita ya Majimaji Kilwa na kuitangaza Kilwa kama sehemu ya Utalii? Hilo ni swali la kwanza. (*Kicheko*)

Swali la pili...

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza maswali mawili Mheshimiwa. Umeshauliza maswali mawili tayari, mpe nafasi Mheshimiwa Waziri Waziri hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Kuchauka nafikiri wewe na mimi kwa pamoja tunafahamu kwamba historia ya kwamba Kilwa haifiki au haipitiki ilikuwa labda zamani; lakini kwa sasa hivi ninavyofahamu na nafikiri Wabunge wengi wanafahamu, kama unazungumzia barabara ya kufika mpaka Kilwa; ni ya lami, kwa maana vivutio vya Mjini Kilwa, yale magofu pamoja na maeneo mengine ya utalii wa kiutamaduni pamoja na utamaduni wa kihistoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama anazungumzia Mbuga ya *Selous*, kufika ndani ya Hifadhi ya *Selous*, ni kweli kuna namna na haja ya kuboresha miundombinu ya kufika ndani ya *Selous* na kuzunguka ndani ya *Selous* yenye kwa maana ya barabara; lakini iko miundombinu ambayo ni maeneo ya malazi au *facilities* za malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mmoja ni jukumu la Serikali, kwa mfano kama barabara, lakini upande mwingine ni jukumu la taasisi binafsi ambazo sasa Mheshimiwa Mbunge usaidie Serikali mnapokaa kwenye Mabaraza kule ya Halmashauri kuweza kuona namna ambavyo mnaweza mkashirikiana na Serikali kuweza kuhamisha wawekezaji wakaweza kuweka vivutio ndani ya *Selous*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nimtaarifu tu Mheshimiwa Kuchauka kwamba mkakati anaoutaka mahususi sasa kwa ajili ya Kilwa yenye; sasa hivi tunakamilisha hadidu za rejea kwa ajili ya mkakati mahususi kabisa kwa ajili ya Kilwa. Siyo Kilwa peke yake, kwa ajili ya *southern circuit*. Huu ni utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo ya Miaka Mitano ambao tunaposema kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano, maana yake tunazungumzia diversification kwamba kutanua wigo wa vivutio vyatya utalii nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia mkakati huo, tuna uhakika kwamba tunakwenda kuboresha mazingira ambayo yataboresha utalii ndani ya Selous lakini pia vivutio ambavyo viko Kilwa Mjini hasa vyatya utamaduni na kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Vita ya Majimaji, hilo suala bado linajadiliwa. Wako upande mmoja katika Kambi nyingine wanasema ni muhimu zaidi kuzingatia kwamba historia ya Majimaji ina mizizi zaidi Kilwa, wengine wanasema ina mizizi zaidi Songea. Sasa nafikiri unatingisha kichwa kwa sababu hayo ni maoni yako, lakini nafikiri suala hili linajadilika, lakini hali ilivyo kwa sasa hivi, mazingira yaliyoko sasa hivi yanazingatiwa kwa mujibu wa historia hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri utakumbuka siku za nyuma tulikaa hapa tukawa tunazungumzia kuhusu suala la historia kwamba wengine wanasema historia inabidi ziandikwe upya, lakini hatuna sababu ya kuandika upya, lakini tutaweza kuweka utaratibu ulio makini kuweza kuweka suala hilo likakaa sawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Sannda swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fursa. Wilaya ya Kondoa hususan pale Kata ya Kolo na nyinginezo, ipo michoro ya mapangoni ambayo ni vivutio vikubwa sana vyatya kihistoria kwa ajili ya utalii, lakini vimedu havitangazwi sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvitangaza ili kizazi cha sasa na cha baadaye kitambue hii fursa na kuweza kuitumia ili hatimaye pia kipato kiongezeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, michoro ya kwenye mapango ya Kondoa ni mojawapo kati ya maeneo ya utalii wa kiutamaduni na utalii wa kihistoria ambao tayari unafahamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo imebaki sasa hivi ni ya kuweza kuboresha matangazo kwa maana ya utangazaji wa utalii; na nimesema katika majibu yangu ya maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka, kwamba tunachokifanya sasa hivi ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao unasisitiza juu ya *diversification of tourist attractions*, kwamba tunataka kuendelea kuboresha na kutanua wigo wa vivutio vya utalii ili tuondokane na vivutio vya utalii vinavyohusiana na wanyamapor peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, chini ya mpango huu, chini ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, tunakwenda kutangaza zaidi vivutio ambavyo ni vipyta; vimekuwepo lakini vimekuwa havitiliwi mkazo, lakini sasa tunakwenda kuvitilia mkazo kwa maana ya kwamba tutaboresha zaidi matangazo kwa ajili ya vivutio vya aina hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu, swali la nyongeza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kule Moshi Vijijini kuna vyanzo vingi vya kitalii ambazo havijatangazwa vizuri. Kwa mfano, kule Kata ya Uru Mashariki kuna maanguko ya maji ya ajabu sana yanaitwa Mnambeni na hivi karibuni katika Kata ya Mbokomu, kumevumbuliwa mti ambao unasemekana ni mrefu kuliko miti yote katika Bara la Afrika. Sasa nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itachukua hatua za makusudi

kuweza kuvitambua hivi vyanzo na kuvitangaza inavyostahili ili tuweze kuvitumia kikamilifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ni tajiri sana ya vivutio vya utalii. Kama nafasi ingekuwepo, karibu kila Mbunge hapa angeweza kusimama na kueleza kwamba katika Halmashauri yake kuna kivutio hiki na kile; sasa suala la kuboresha utangazaji siyo suala la Serikali peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaendelea na utaratibu wa kuweza kuboresha matangaza ambayo sasa hivi tunafanya, nitoe wito sasa kwa Mbunge moja moja lakini kuititia Halmashauri zinazohusika kuanza kuvibainisha vivutio vilivyopo kwenye maeneo yao ili viweze kwenda mbele ya wataalam wa Idara ya Utalii katika Wizara ya Maliasili na Utalii tuweze kuviorodhesha kwa pamoja, halafu tukubaliane kama vinakidhi viwango vya Kimataifa kama vivutio, tuweze kuvifanyia *grading*, halafu baada ya pale tuendelee na utaratibu wa kutangaza tuktambua kwamba ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 mwananchi mmoja wa Kenya alitamka maneno kwenye mkutano mmoja wa Kimataifa kwenye nchi mojawapo nje kule, kwa kurusha tu *clip* ndogo tu lakini ikatingisha dunia, lakini pia na sisi Watanzania tukaanza kusema kwa nini wanataka kuteka vivutio vyetu? Ule haukuwa mpango wa Serikali, ni mtu mmoja tu alifanya vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wa Tanzania nasi kwanza tushiriki katika utalii wa ndani ili tuvifahamu vivutio vyetu na sifa zake halafu baada ya pale nasi tuweze kushiriki kama Watanzania kutangaza vivutio vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kushirikiana na wenzetu walioko nchi za nje kwa utaratibu wa *diaspora* ili tuweze kufanya nchi yetu ikapata kutangazwa sawa sawa kwa maana ya vivutio vya utalii. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Peter Msigwa, swali la nyongeza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na swali la msingi ambalo niliuliza kuhusu vivutio, Mji wetu wa Iringa ni Mji mkongwe ambao una historia kubwa ya Mtemi wetu Mkwawa jinsi alivyopambana na Mjerumani. Ni juhudzi za makusudi ambazo zinafanywa na maliasili kuhakikisha kwamba mji huu wa Iringa na historia kubwa ya Mtemi Mkwawa inaendelea kujulikana katika dunia nzima na Tanzania kwa ujumla?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatua nyingi zinafanywa kuboresha utalii katika eneo zima la Kusini mwa Tanzania, lakini hususan Mji wa Iringa na viunga vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumefungua makumbusho ya historia ya Iringa na utemi wake kule. Pili, Serikali inapanua Uwanja wa Nduli kama ulivyoona kwenye bajeti. Vile vile Serikali imepanga kujenga barabara kutoka kwenye geti la Ruaha kuja Ruaha Mjini. Shughuli hii tumeishughulikia sana na Mheshimiwa Lukvi katika kuitekeleza pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 tumeanza kwa mara ya kwanza kuwa na Maonesho ya Utalii Kusini mwa Tanzania na yalikuwa Iringa na mwaka huu maonesho hayo ni makubwa zaidi. Waheshimiwa Wabunge, nawakaribisha mje kushiriki katika maonesho hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martin Msuha, swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Wilayani Mbanga yako mawe mawili makubwa ya ajabu ambayo yanafahamika kwa jina la Mawe ya Mbaji; mawe haya yanasadikika kuwa ni jiwe la kike na la kiume; lakini pia katika mawe hayo viko viumbe hai vyenye kimo kifupi sana vinavyofanana na binadamu, viumbe hivi huwa vinajitokeza hasa msimu wa michezo ya utamaduni. Je, ni lini Serikali itafanya utafiti ili kubaini ni viumbe vyaa aina gani hivyo ambavyo vinaishi katika mawe hayo na hatimaye kutangaza eneo hilo kama eneo la utalii? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, viumbe sijui, aah nadhani Mheshimiwa Msuha atawea kwenda kukuonesha vitakapoonekana. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye maswali ya nyongeza yaliyotangulia, nimesema nchi hii ni tajiri sana ya vivutio vyaa utalii, jambo ambalo hatujalikamilisha bado na tunaendelea kulifanya ni kuwa na orodha ya vivutio hivyo viliviyohakikiwa kwa sababu siyo kila kitu ambacho mtu mmoja anaweza kukiona kwamba kinatosheleza kuwa kivutio cha utalii, kinakuwa hivyo; ni mpaka wataalam wanaohusika waseme kwamba sasa hiki kinakidhi viwango vyaa Kimataifa vyaa kuwa kivutio cha utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, tayari imeshawasiliana na Halmashari zote nchini ili kuweza kuviorodhesha vivutio hivyo, vifike Wizarani, tuvifanyie uchambuzi halafu tuweze kuviweka katika makundi (*grading*) halafu tuweze kuweka mkakati wa pamoja wa namna gani ya kutangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema jukumu la kutangaza lisiwe jukumu la Serikali peke yake; kama mnavyofahamu na mnavyoona, dunia ya sasa ni kama kijiji; na kila mmoja akitumia wajibu wake wa kutumia mifumo ya mawasiliano ya kisasa, tunaweza kutangaza nchi yetu kwa namna ambayo ni ya mafanikio zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa nchi yetu ina maeneo mengi ya masalia ya Wafalme pamoja na majengo; kwa mfano, Mtemi Shomali Mwanansali wa Igurubi, kuna majengo ya Mtemi Humbi Ziyota Mwanantinginya pale Ziba. Kwa nini Serikali sasa isiyatambue maeneo haya yote yenye majengo na masalia ya Watemi nchini kote na kuyatangaza? Najua wenzetu kutoka Ulaya watakuja kuyaangalia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yalikuwa makazi au hata ni makazi hata sasa ya viongozi wetu wa kimila; Watemi, Mamwinyi na wengineo, kweli ni maeneo ambayo licha ya kwamba ni ya kihistoria, yana vivutio kwa sababu kimsingi yana record ambayo inaweza kutupa hata mafundisho kwa ajili ya siku za usoni. Kama ambavyo tunajua historia na faida zake, kwamba unaangalia tulikotoka, hapa tuliko na huko mbele tuendako, inaweza kuwa ni mchango mkubwa sana kwa upande wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukajiuliza, hivi ni kwa kiasi gani sisi wenyewe kwanza tunatembelea maeneo hayo? Ni kwa kiasi gani sisi wenyewe tunayapenda maeneo hayo na tunyatunza kabla hatujafikiria hata kuyatangaza kwa ajili ya watalii kutoka nje? Sasa wito

nililoutoa kabla na napenda kuurudia tena hapa, tuanze sisi wenyewe kwanza kwenye Halmashauri zetu kuanza kuthamini maeneo hayo, kuyaweka vizuri katika ubora wake, halafu baada ya pale, kuwasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii na kuweza kuona namna gani tunaweza kuviboresha na kuvitangaza vivutio hivyo ndani na nje.

**NAIBU SPIKA:** Swali al mwisho, Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nami kupata fursa hii ya mwisho ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mazingira ya kusini katika maana ya Ruaha, Rufiji mpaka Kilwa yanafanana kabisa na Hifadhi ya Msitu wa Liparamba unaounganisha upande wa Nyasa, Mbinga Mjini na upande wa Msumbiji. Ni lini Hifadhi ya Liparamba itapata hadhi inayostahili ili iwe kivutio cha utalii kwa *center*ya Kusini, hususan tunaunganisha nchi mbili za Msumbiji na nchi ya Malawi? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba Hifadhi ya Liparamba iliyopo mkoani Ruvuma ni mojawapo kati ya maeneo ya hifadhi ya wanyamapor i machache sana kwa Mkoa wa Ruvuma, lakini tajiri kwa wanyamapor na ambayo inastahili kabisa kuwa kwenye viwango vya Kimataifa vya kuwa mojawapo ya maeneo yenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia kwamba katika siku za nyuma, mkazo wa kuweka mipango na mikakati ya kuweza kuboresha utalii katika hifadhi hiyo, hapo nyuma hakukuwa na mipango madhubuti kwa sababu hatukuwa na utaratibu wa kuweza kuboresha utalii upande wa kusini mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hapo awali kwamba katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tumezungumzia juu ya ku-diversify au kuweka utaratibu wa kuwa na mtawanyiko wa vivutio kwa maana ya vivutio vyenyewe; aina za vivutio, pia mahali vivutio vilipo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, chini ya mpango huo, tutakwenda kuboresha utalii kusini na Hifadhi ya Liparamba ni mojawapo kati ya hifadhi ambazo zinaenda kuwekwa katika kipaumbele ili kuhakikisha kwamba sasa watalii hawaendi tu Arusha, Moshi, Kilimanjaro na maeneo ya Kaskazini, pia waweze kwenda Mbeya, Songea, Mtwara na maeneo mengine ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi tuweze kukamilisha mipango iliyopo kwa ajili ya kutekeleza sehemu ya mpango wa miaka mitano ili tuweze kuona sasa tunaboresha utalii upande wa kusini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swalı lake.

Na. 440

#### **Ukosefu wa Mahakama – Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Katika Jimbo zima la Mlimba hakuna Mahakama hata moja, jambo linalosababisha mahabusu kupelekwa Jimbo la Kilombero umbali wa takriban kilometa 260 kuhudhuria mahakama:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Jimbo la Mlimba ili kuwaondolea wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu katafuta huduma ya Mahakama?

## **WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo nchini unaongozwa na Sheria ya Mahakimu, Sura 11 ya Sheria za Tanzania (*The Magistrate Courts Act, Cap. 11 of the laws of Tanzania*). Kifungu cha 3(1) kinaeleza kuwa katika kila Wilaya kutaanzishwa Mahakama za Mwanzo; Kifungu cha 4(1) kinaeleza kuwa kutaanzishwa Mahakama za Wilaya katika kila Wilaya na Kifungu cha 5(1) kinampa mamlaka Jaji Mkuu kutoa amri ya kuanzisha Mahakama za Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mlimba, Tarafa ya Mlimba ipo Mahakama ya Mwanzo inayoendelea kutoa huduma hadi hivi sasa. Serikali inatambua kuwa miundombinu ya Mahakama hiyo hairidhishi na hivyo katika mwaka wa fedha 2017/2018 tumepeanga kujenga Mahakama ya Mwanzo mpya katika Tarafa ya Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umbali na ukubwa wa Wilaya ya Kilombero yenyewe Majimbo ya Kilombero na Mlimba na itajitahidi kuhakikisha kwa kadri ya uwezo utakavyokuwa kujenga Mahakama za Mwanzo za kutosha katika Wilaya nzima ya Kilombero ili kusogea huduma za Mahakama na utoaji haki karibu zaidi na wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, swalii la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kwamba kuna mpango wa kujenga Mahakama pale Mlimba, lakini sijui itachukua muda gani; ingawa hapo anaposema kwamba ni Mahakama, ni

kibanda tu cha TAZARA wameazima na mara nyingi Mahakimu huwa hawapo muda mrefu sana. Labda kwa sababu hakuna Mahakama ambayo inatambulika rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mahakama eneo la Utengule, kule alikotoka *Chief Kiwanga*, kwenyewe hakuna kabisa Hakimu. Kwa hiyo, watu wanapata shida sana katika kupata huduma. Je, pamoja na kuwa na mpango wa Serikali kujenga hiyo Mahakama hapo Mlimba ambapo ni Makao Makuu ya Jimbo, Serikali iko tayari sasa kupeleka Mahakimu kwenye maeneo ambayo kuna Mahakama lakini hakuna Mahakimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Waziri huyu ameteuliwa hivi karibuni, je, yuko tayari sasa kufanya ziara kwenye Jimbo la Mlimba kuangalia hali halisi na miundombinu ili anapokwenda kwenye bajeti tuone kwamba anaikumbuka Mlimba na kuiwekea mafungu ambayo yanastahili ili wananchi wapate haki zao? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan, nadhani utakuwa na wageni wengi sana Mawaziri huko Jimboni kwako safari hii. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ombi lake la kuhakikisha kuwa Mahakama za Mwanzo katika Wilaya ya Kilombero, yaani Jimbo la Mlimba na Kilombero zinapata Mahakimu ili kusogea huduma ya utoaji haki katika eneo hilo; hasa tukizingatia kuwa Wilaya ya Kilombero kama ilivyo Wilaya ya Loliondo, Kiteto, Manyoni ni Wilaya ambazo kijiografia maeneo yake ni makubwa sana na umbali ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa Wizara pamoja na Mahakama tutahakikisha Wilaya za aina hiyo, yaani Kilombero, Kiteto Loliondo na Manyoni, zinapata aina ya msisitizo katika kuhakikisha kwamba Mahakama zake za mwanzo zina Mahakimu wengi ili kupunguza umbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa unapotoka Mlimba mpaka kwenda Kilombero kilometra 260 ni mikoa kwa sehemu nyingine. Kwa hiyo, tutalizingatia kabisa katika kuhakikisha kwamba Mahakama hizo kutegemea na lkama iliyotolewa na Serikali, zinapata Mahakimu wa mwanzo wengi ikiwa ni pamoja na Utengule alipotoka Chifu Kiwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ziara ya kwenda Mlimba, naipokea kwa mikono miwili; huu ni wakati wa mavuno; kwa hiyo, nitapata mchele na pepeta; siyo kama takrima, lakini kama ukarimu wa watu wa Mlimba. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Hali inayojitokeza Mlimba ni sawasawa na inavyojitokeza Jimbo la Mbagala. Niliwahi kuuliza swali la msingi, nikaambiwa kwamba mwaka huu watajenga Mahakama katika Jimbo la Mbagala, lakini tatizo ni viwanja. Tayari tumeshapata viwanja eneo la Kijichi na Chamazi. Je, ni nini tamko la Serikali kuhusu kujenga Mahakama katika Jimbo la Mbagala? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mpango wa kujenga Mahakama ya Mwanzo huko Temeke; na sasa tutahakikisha tunajua Temeke sehemu gani? Hata hivyo, nimelipokea suala la Mbagala, tutalifanya kazi na kuona hii Mahakama ya Mwanzo ambayo imepangwa kujengwa Temeke mwaka 2017/2018 itakuwa sehemu ipi na kama siyo Mbagala, basi suala la Mbagala tutalichukulia kwa umakini unaostahili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Wilaya ya Mlele haina Mahakama kabisa, ni lini watajenga Mahakama ya Wilaya ya Mlele? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mipango iliyopo katika Mahakama, Wilaya ya Mlele imepangwa kujengewa Mahakama ya Wilaya mwaka 2017/2018 na nimalizie hapo hapo na Wilaya za Mpanda na Tanganyika mwaka 2019/2020. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi sana; inavyoonekana kila mahali kunahitaji Mahakama. Sasa kama tumetoka kuitisha bajeti, nadhani tukubaliane kwamba kila mahali Mahakama zitaenda.

Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina Mahakama moja iliyopo Lupembe na Mahakama hii jengo lake ni chakavu sana na ina nyufa nyingi, lakini pia ipo kwenye hifadhi ya barabara. Tayari wananchi wameshatoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Je, ni lini Serikali itanza ujenzi wa Mahakama hii? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maadam wameshapata ardhi na wameshachukua hatua za mwanzo, namwomba Mheshimiwa Hongoli tuonane ili njue taratibu nyingine zinazostahili kufuatwa ili tukamilishe jambo hilo na Mahakama iweze kuanza kujengwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Hongoli tuonane ili nipate taarifa hizo ili nami nizifikishe kwa Mtendaji wa Mahakama halafu tuone tunafanya vipi kwa sababu tayari maandalizi ya awali ya kiwanja na naamini kina hati; kama ni hivyo, basi hatua zinazofuata zitakuwa ni rahisi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa *justice delayed is justice denied* na kwa kuwa kauli mbiu ya mwaka huu katika Siku ya Sheria ilikuwa Umuhimu wa Utoaji Haki kwa Wakati ili Kuwezesha Ukuaji wa Uchumi; Mheshimiwa Waziri ni kwa nini kesi nyingi zinacheleweshwa wakati kauli mbiu yetu ni hiyo kwamba lazima kesi zifanywe kwa haraka ili watu wasikose haki yao kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo hilo nalo linahusu ujenzi wa Mahakama?

Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nina swali moja la nyongeza. Najua kwenye Wizara Mheshimiwa Waziri hana muda mrefu sana, lakini Mahakama ya Mkoa wa Manyara ilijojengwa pale Babati Mjini, Mtaa wa Negamsi ni Mahakama ya Mwanzo, ya Wilaya, mpaka ya Mkoa, kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa fidia zao, mpaka leo wameachia eneo hilo kwa Mahakama. Ni miaka 14 sasa tangu 2004. Pamoja na ugeni wake katika Wizara, je, yuko tayari kufuatilia kwa karibu ili wananchi wale, ndugu zake, wajomba zake wapate fidia zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na maoni aliyoyatoa na nitafuatilia

kuona fidia ya hao watu ambao walitoa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hizo, linafanyiwa kazi haraka. Nitatalifuatilia kwa karibu na najua watu wengine wanaweza kuwa wanashangaa ukaribu huo umetoka wapi? Ni kwa sababu katika mishipa yangu pia nina damu ya Kibarbaigi. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo maswali yametosha. Hatukuwa na maswali kwa Waziri Mkuu, ndiyo maana tumeenda kwa kirefu kidogo.

Kabla hatujaendelea na shughuli iliyo mbele yetu leo, niwaletee matangazo. Tutaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni. Kundi la kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 118 wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu na Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Mtakatifu Leo Mkuu na Walimu wao kutoka Igunga Mkoa wa Tabora. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 47 wa Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma kutoka Ukerewe Mkoani Mwanza. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; na kundi la kwanza ni wanafunzi 86 na Walimu sita wa *Black School of Linguistic and Literature* kutoka Mkoani Dodoma na wamekuja kujifunza uendeshaji wa Bunge. Sijui wako sehemu gani, ama pengine nafasi haijawatosha.

Kundi lingine ni wanafunzi 59 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Kikuyu 'B' ya Mkoani Dodoma na hawa wamekuja pia kujifunza namna ya uendeshaji Bunge. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia tunao, wanafunzi 83 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Martin Luther; na hawa pia wanatoka Mkoani Dodoma, nao wamekuja kujifunza namna ya uendeshaji wa Bunge. Karibuni sana. Naamini mkitoka hapa mtakuwa

mnaenda kujipanga ili mje muwe Wabunge hapo baadaye.  
*(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Ofisi ya Mheshimiwa Spika; Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mnatangaziwa kwamba leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Spika. Mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na shughuli iliyo mbele yetu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaruhusu miongozo, niwakumbushe tu. Miongozo maana yake ni kwamba kuna jambo halijawa sawasawa, kwa sababu tumekuwa tu na kipindi cha Maswali na Majibu. Kwa hiyo, miongozo iwe inahusu mambo hayo.

Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na maelekezo yako, lakini nimesimama hapa kwa kanuni ya 47, nadhani ni kanuni inayojulikana, sina sababu ya kuisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa mambo ambayo yamekuwa yakiendelea kutokea katika nchi yetu. Kumekuwa na mauaji yanayoendelea hasa katika Mkoa wa Pwani ambayo inaonekana vyombo vya usalama vimeshindwa kuyadhibiti. Mpaka ninavyozungumza hapa ni zaidi ya watu 36 pamoja na Polisi wameuawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili katika Bunge lako Tukufu tumeuliza, tumeoji, tumedadisi, Serikali imesema tuipe muda; na kila Serikali inapotoa matamko ya kusema wamejipanga, ndipo mauaji yanapozidi kutokea. Sisi kama Wabunge, tuna wajibu na tuna jukumu kubwa la kuisimamia Serikali; na kuisimamia Serikali ni pamoja na kuhakikisha ulinzi

wa raia. Jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha ina-preserve maisha ya watu wake inaowaongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji haya yanayoendelea hususan kwa Askari wetu, naomba suala hili Bunge lako lisimamishe shughuli zote tulijadili ili kuhakikisha tunaisimamia Serikali tuweze kukomesha mauaji haya yanayoendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili suala hili tuweze kulijadili. Naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali yetu mpaka sasa kwa asilimia 80 imehamia Dodoma. Sasa hivi ninavyoongea, kuna Wabunge zaidi ya 250 Dodoma; kuna Mawaziri na Manaibu Waziri zaidi ya 30; kuna Wakurugenzi na Naibu Wakurugenzi wa Wizara tofauti zaidi ya 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi unatakiwa kuimarishwa sana hasa nyakati za usiku ukizingatia na hali yenyewe inayoendelea katika nchi yetu. Hivi ninavyoongea, Kituo Kikuu cha Polisi cha Dodoma hakina umeme zaidi ya mwezi mmoja. Ninavyofahamu, Polisi, Ikulu wote umeme unalipwa kutokana na kodi za wananchi. Kwa nini Ikulu umeme haukatwi, lakini katika Vituo vya Polisi na Magereza, umeme unakatwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, Serikali itoe maelezo kutokana na hili. (*Makofii*)

**MHE. KHATIBU SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Leo nimechukua miongozo miwili Mheshimiwa Khatibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze na mwongozo uliyoombwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, kwa kuwa ameomba mwongozo na kanuni yetu ya 68(7) inataka jambo lililotokea Bungeni mapema. Kuzimwa kwa umeme kwenye Kituo cha Polisi hakujazimwa humu ndani, kwa hiyo, sisi hatuelewi umekatika kwa sababu zipo. Unaweza kuwa umezimwa ama huenda kuna hitilafu. Kwa sababu Bunge halina taarifa hiyo na halijatokea humu ndani, kitinakina uwezo wa kutoa mwongozo kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa amesimama kwa Kanuni ya 47, akitaka kutoa hoja ili Bunge liweze kuahirisha shughuli zake na kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa amelieleza jambo la dharura kwamba ni mauaji yanayotokea Kibiti, Mkoani Pwani na ametaja hapo takwimu za Maaskari na wananchi pla ambao wameshauawa mpaka sasa; na ametoa maelezo kwamba jambo hili limeshawahi kuulizwa na kuzungumzwa Bungeni na Serikali ilioa kauli kwamba inahitaji muda.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa analitaka Bunge liahirishe shughuli zake ili lijadili jambo hili; na kwa maelezo yake, ye ye anaona linakidhi vigezo vyta kuwa jambo la dharura.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47 inapaswa kusomwa na Kanuni ya 48 ambayo inaweka masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura. Masharti hayo katika Kanuni ya 48 ni lazima yaye yamethibitishwa, ndipo ambapo Bunge hili linaweza kuahirisha shughuli zake ili liweze kujadili jambo hilo. Kanuni ya 48(4) inasema hivi:

*“Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa Umma iwapo utatuvi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake.”*

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma hii fasili ya (4), inazungumza kuhusu maslahi ya umma, ni kwa sababu masharti yaliyotajwa kwenye hii Kanuni ya 48 yanatoa

mwongozo wa jambo gani linaweza kuitwa jambo la dharura ili Bunge liweze kuahirisha shughuli zake na kulijadili.

Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alivyosema, jambo hili ni zito, limelifika Taifa na lilishawahili kusemwa na Serikali ilitoa kauli. Kwa mujibu wa Kanuni ya 47(4), mimi nimeridhika kwamba Serikali inafuata utaratibu ule uliopo wa kisheria wa kushughulikia jambo hili. Kwa hiyo, Bunge halina uwezo wa kujadili jambo hili ambalo hata kama tukitaka kulijadili bado hata sisi tutatakiwa kujadili sheria zinasema nini na Serikali inapaswa kufanya nini. Kwa sababu hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 47(4), sitaruhusu jambo hili kujadiliwa badala ya kuendelea na mambo yaliyopo mbele yetu.

Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017**  
*(The Finance Bill, 2017)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Act, 2017*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijiini, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Aidha, katika kipindi chote cha majadiliano, Kamati ilitoa michango na changamoto

nyingi kwa Serikali kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato yatokanayo na kodi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Vilevile Serikali itaendelea kufanya kazi mapendekezo mengine. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ambaao walichangia katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni tarehe 20, Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wake wa Uandishi wa Sheria kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, wadau mbalimbali katika Sekta ya Fedha, Biashara na Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla, ambaao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho Sheria Mbalimbali za Kikodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 niliyowasilisha Bungeni tarehe 8, Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanya marekebisho sheria 15 zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru, tozo na mawasiliano kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali na kuboresha ukusanyaji wa kodi kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini; kupunguza Kodi ya Mapato kwa waunganishaji (*assemblers*) wa magari, matrekti na boti za uvuvi; na kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mashine mbalimbali zinazotumika kwenye viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula, nguo na ngozi ili kuchochaea uzalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini;

kuhamasisha uhaulishaji wa teknolojia; na kuongeza mapato ya Serikali.

Pili, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri katika huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa na mizigo nje ya nchi (*Ancillary Transport Services*). Hatua hii itahamasisha wasafirishaji kutoka nchi jirani kupitisha mizigo yao kwa wingi kwenye bandari zetu na hivyo kukuza uchumi wa nchi kutokana na kuongezeka kwa mapato ya bandari na kuongezeka kwa ajira nchini.

Tatu, kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari (*Annual Motor Vehicle License Fee*) ili ada hii ilipwe mara moja pekee gari linaposajiliwa. Aidha, Serikali inatoa msamaha (*tax amnesty*) wa kodi, riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote ya ada hiyo yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha huu utahusisha pia madeni ya ada ya vifaa vya kuzima moto (*fire extinguisher*) kwenye magari ambayo ilikuwa ikikusanya kwa pamoja na ada ya leseni ya magari.

Nne, kupunguza ushuru wa mazao (*produce cess*) unaotozwa na Halmashauri za Wilaya kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano ya thamani ya mauzo (*gross value*) hadi asilimia tatu kwa mazao yote. Aidha, mtu anayesafirisha mazao yake kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine yasiyozidi tani moja hatalipa ushuru huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuwawezesha wakulima kulipwa bei stahiki ya mazao yao na hivyo kuboresha mapato yao. Hatua hii inatarajiwa kuhamasisha uzalishaji wa mazao. (*Makofi*)

Tano, ni kuweka utaratibu wa kudhibiti utoaji wa madini migodini kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi au kwa ajili ya matumizi ndani ya nchi. Serikali itaaniszha maeneo maalum (*clearing houses*) migodini, viwanja vya ndege vya

Kimataifa, bandarini, mipakani na kadhalika, ambapo madini hayo yatahakikiwa na kupewa kibali cha kusafirisha madini ambacho kitatozwa ada ya asilimia moja (*clearing fee*) ya thamani ya madini hayo. Ili kuweka utaratibu mzuri wa utekelezaji wa hatua hii, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini atatangaza tarehe ya kuanza utekelezaji wa hatua hizi.

Sita, ni kutoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Nyumba ambazo hazijafanyiwa uthamini zitatozwa kwa kiwango maalum (*flat rate*) cha sh.10,000/= kwa nyumba na sh.50,000/= kwa nyumba za ghorofa kwa kila ghorofa. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba kodi stahiki inalipwa kwa majengo yote ili kuongeza mapato ya Serikali na kuweka usawa katika utozaji kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, sheria itaweka utaratibu wa kutotoza Kodi ya Majengo kwenye nyumba za wananchi maskini zilizojengwa kwa miti, udongo, nyasi au nyumba za tembe kwa kuweka tafsiri sahihi ya nyumba zinazopaswa kutozwa kodi hiyo.

Saba, Mamlaka ya Mapato Tanzania kupewa mamlaka ya kukusanya Kodi ya Majengo katika miji, majiji na miji midogo na mabango ya matangazo kwa Halmashauri zote nchini na mapato husika kuhifadhiwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatokanayo na kodi hii ili kuziwezesha Halmashauri kujitegemea kutokana na mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mapato yatakayokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuhifadhiwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Majengo na ushuru wa mabango ya matangazo, yatarejeshwa kwenye Halmashauri husika kwa ajili ya matumizi baada ya Halmashauri husika kuwasilisha Serikalini mahitaji halisi na Serikali kujiridhisha na mahitaji yao.

Nane, kuutambua kisheria mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vifaa na mifumo ya kielektroniki ili kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali, Mfumo uitwao *Government E-payment Gateway System* utatumika na Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali katika ukusanyaji wa mapato. (*Makofi*)

Tisa, kupanua wigo kwa kutoa fursa kwa Taasisi yoyote ya Kitanzania, Watanzania wanaoishi nje ya nchi, kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja baina ya Watanzania na raia wa nje, raia na kampuni au taasisi za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au raia na makampuni kutoka nchi nyingine kununua hisa za kampuni za mawasiliano, sambamba na sharti la kuuza asilimia 25 za hisa kwa wananchi wa Tanzania pekee.

Kumi, kuweka utaratibu wa kuwatambua rasmi washereheshaji kwenye sherehe, watoa huduma ya chakula (*Caterers*), wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi; mfano, Mama Lishe, wauzaji mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mboga mboga, ndizi, matunda na kadhalika, kwa kuwapatia vitambulisho maalum vyta kazi wanazozifanya. (*Makofi*)

Kumi na moja, kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa magari yanayotumika kwa ajili ya kubeba wagonjwa (*ambulance*) ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi wetu na hasa katika maeneo ya vijijini. Hatua hii itahusisha magari yanayoingizwa nchini yakiwa yametengenezwa mahususi kwa ajili ya kubeba wagonjwa na kwa ajili ya matumizi ya hospitali au Vituo vya Kutoa Huduma ya Afya vilivyoasajiliwa kisheria. Aidha, Serikali itatumia Utaratibu wa Hati ya Malipo ya Hazina (*Treasury Voucher System*) katika kutekeleza msamaha huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

- (1) Sheria ya Benki Kuu, Sura ya 197;

- (2) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya kielektroniki, Sura ya 306;
- (3) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
- (4) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
- (5) Sheria ya Kodi ya Mapato Sura, ya 332;
- (6) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
- (7) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
- (8) Sheria ya Usalama Kazini, Sura ya 295;
- (9) Sheria ya Bandari, Sura ya 166;
- (10) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;
- (11) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
- (12) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
- (13) Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Miji, Sura ya 289;
- (14) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148;
- (15) Sheria ya Mafunzo ya Ufundji Stadi, Sura ya 82; na
- (16) Sheria ya Reli, Sura ya 170.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maudhui ya Muswada; Muswada huu umegawanyika katika sehemu 16 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza yenye vifungu namba (1) na (2) inahusu masuala ya utangulizi yanayojumiusha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambapo itaanza kutumika tarehe 1, Julai, 2017 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197 ili kuweka sharti kwa taasisi za Serikali, kufungua akaunti na kuhifadhi mapato au fedha zake Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306 ili:

Moja, kupanua wigo wa mauzo ya hisa za asilimia 25 zitakazouzwa na Kampuni ya Mawasiliano kwenye Soko la Hisa kwa kutoa fursa kwa Watanzania au taasisi yoyote ya Kitanzania, Watanzania wanaoishi nje ya nchi, kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja baina ya Watanzania na raia wa nje, raia na kampuni au taasisi za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au raia na makampuni kutoka nchi nydingine yoyote. (*Makofii*)

Pili, ni kuondoa sharti la kuuza hisa katika Soko la Hisa kwa kampuni ndogo za mawasiliano zenye Leseni ya *Application Service* na kubaki na kampuni kubwa zenye Leseni ya *Network Facility* au *Network Service*; na

Tatu, ni kuwezesha Mamlaka ya Masoko na Dhamana baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya masoko ya dhamana kutoa maelekezo ya namna kampuni iliyoshindwa kufikia mauzo ya hisa asilimia 25 itakavyoweza kufikia mauzo ya kiwango husika kwa kadri hali ya soko itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kufanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru (*specific duty rates*) vinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa kiwango cha mfumuko wa bei cha asilimia tano. Sababu yake ni kuwa pale ambapo ushuru wa bidhaa unatozwa kwa kiwango maalum (*specific rate*), ushuru huo hauakisi mfumuko wa bei na hivyo hupunguza mapato. Njia bora inayotumika kuondoa upungufu huo ni kurekebisha viwango maalum vya ushuru ili kuendana na kiwango cha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ni tofauti na pale ambapo ushuru wa bidhaa hutozwa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa (*ad valorem rate*) ambapo hapana sababu ya kurekebisha viwango vya ushuru kwa kuwa thamani ya bidhaa inazingatia mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, marekebisho haya ninayopendekeza ni kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kifungu cha 124(2) kinachoelekeza kuwa marekebisho ya viwango vya ushuru yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuvioanisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, kwa kuzingatia mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi wa Viwanda, kiwango cha ushuru kwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini kimepunguzwa au kubakia ilivyo sasa. Mabadiliko ninayopendekeza ni kama ifuatavyo:-

(1) Ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi kutoka sh.58/= kwa lita hadi sh.61/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.3/= kwa lita.

(2) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa yaliyoagizwa kutoka nje kutoka sh.58/= kwa lita hadi sh.61/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la

sh.3/= kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa nchini utabaki kuwa sh.58/= kwa lita.

(3) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (*juice*) iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini (*local juices*) utashuka kutoka sh. 9.5 kwa lita na kuwa sh.9/= kwa lita.

(4) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (*juice*) iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini (*imported juices*) kutoka sh.210/= kwa lita hadi sh.221/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.11/= kwa lita.

(5) Ushuru wa bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa (*beer from local unmalted cereals*) kutoka sh.429/= kwa lita hadi sh.450/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.21/= kwa lita.

(6) Ushuru wa bidhaa kwenye bia nyingine zote, kutoka sh.729/= kwa lita hadi sh.765/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.36/= kwa lita.

(7) Ushuru wa bidhaa kwenye bia zisizo na kilevi, ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu kutoka sh.534/= kwa lita hadi sh.561/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.27/= kwa lita.

(8) Ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 utashuka kutoka sh.202/= kwa lita na kuwa sh.200/= kwa lita.

(9) Ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka sh.2,236 kwa lita hadi sh.2,349 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la sh.113/= kwa lita.

(10) Ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi kutoka sh.3,315/= kwa lita

hadi sh.3,481/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh.166/= kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyozalishwa nchini, utabaki kuwa sh.3,315/= kwa lita.

(11) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungu zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka sh.11,854/= hadi sh.12,447/= kwa sigara 1000; ikiwa ni ongezeko la sh.593 kwa kila sigara 1000.

(12) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zenye kichungu zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 25 kutoka sh. 28,024/= hadi sh.29,425/= kwa kila sigara 1000, ikiwa ni ongezeko la sh.1,401/= kwa kila sigara 1000.

(13) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zenye sifa tofauti na mbili zilitangulia kutoka sh.50,700/= hadi sh. 53,235/= kwa kila sigara 1000, ikiwa ni ongezeko la sh. 2,535/= kwa kila sigara 1000.

(14) Ushuru wa bidhaa kwenye tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara yaani *cut filer* kutoka sh.25,608/= hadi sh.26,888/= kwa kilo, ikiwa ni ongezeko la sh.1,280/= kwa kilo.

(15) Ushuru wa bidhaa wa sigara unabaki kuwa asilimia 30. (*Makofi*)

(16) Kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya *petrol*, *diesel*/na mafuta ya taa kwa kiasi cha sh.40/= kwa lita moja kutoka kiwango cha sasa cha sh.399/= kwa lita hadi sh.379/= kwa lita kwa mafuta ya *petrol* kutoka kiwango cha sasa cha sh.215/= kwa lita hadi sh.255/= kwa lita kwa mafuta ya *diesel*/na kutoka kiwango cha sasa cha sh.425/= kwa lita hadi sh.465/= kwa lita kwa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kufidia ada ya mwaka ya leseni ya magari yaani *Annual Motor Vehicle Licence Fee* ambayo inapendekezwa kufutwa kwa

kuwa imekuwa inalipwa hata kwa magari ambayo hayatumiki na hivyo kuwa kero kubwa kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania, kukusanya kodi inayotozwa chini ya sheria hiyo. Mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yatawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali; na Serikali itaweka utaratibu wa kuzirejesha fedha hizo kwenye Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Baada ya Bodi hiyo kuwasilisha Serikalini mahitaji na matumizi na Serikali kuhakiki na kujiridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita, kama ilivyorekebishiwa kupitia jedwali la marekebishi, inapendekeza marekebishi katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha (3) ili kufanya marekebishi mbalimbali ya kiuandishi kwenye tafsiri ya maneno "*business licence area*" na "*rehabilitation fund*" ili kuleta maana iliyokusudiwa na kuwezesha utekelezaji wa sheria wenye ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa kubainisha ndani ya sheria, tafsiri ya maneno "*licensed dealer*" ili kuwezesha utekelezaji wa pendeleko la kutoza Kodi ya Zasio kwa wachimbaji wadogo wa madini kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 12 ya Muswada.

(b) Kurekebisha Kifungu cha 11 (4), kwa kuongeza Aya mpya ya (f) ili kuzuia ukwepajji kodi ya zasio unaotokana mikataba ya utoaji huduma inayowalazimisha watumiaji wa huduma kulipa kodi ya zasio kwa niaba ya watoa huduma na kisha kudai kodi hiyo kama gharama ya uzalishaji.

(c) Kufanya marekebishi ya kiuandishi kwenye 14(2), kwa kuweka usahihi wa rejea kwa kufuta rejea ya

Kifungu cha 36 kilichowekwa kimakosa na kuweka kifungu cha 37.

(d) Kurekebisha Kifungu cha 19(2) kwa kuongeza aya mpya ya (e) ili kuzuia ukwepaji kodi utokanao na hasara zinazopatikana kwenye biashara hasa kwa walipa kodi wanaofanya biashara ya madini. Vile vile kurekebisha kifungu kidogo cha (4) kwa kuongeza tafsiri ya maneno "*speculative transation*" ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa marekebishesho yaliyopendekezwa kwenye kifungu cha 19(2).

(e) Kurekebisha kifungu cha 63 kwa kufuta aya ya (f) na kuiandika upya ili kupanua wigo wa kutoza Kodi ya Zuo kwenye malipo ya mapato yatokanayo na huduma ya bima (*re-insurance*) ambayo hivi sasa hayatozwi kodi. Lengo la marekebishesho hayo ni kuwezesha Serikali kupata mapato kwenye biashara hii.

(f) Kuongeza Kifungu cha 83(b) na kuongeza aya mpya ya (g) kwenye Kifungu cha 86(1) ili kutoza kodi ya zuio kwa kiwando cha 5% kwenye bei ya kuuzia (*total market value*) ambayo itakuwa ni Kodi ya Zuo ya Mwisho (*Final Withholding Tax*) kwa wachimbaji madogo wadogo wa madini wa aina zote isipokuwa chumvi, mchanga na kokoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki kutoka katika Sekta ya Madini.

(g) Kufanya marekebishesho ya kiuandishi kwenye kifungu cha 88(5) kwa kuongeza neno "*business*" ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa sheria.

(h) Kurekebisha Kifungu cha 90(4) ili kutoa unafuu wa gharama za usafirishaji wa maua kwa kutumia ndege ili kukuza Sekta ya Kilimo nchini.

(i) Kurekebisha kifungu cha 91(2)(e) ili kuweka sharti kwa mlipa kodi kuwasilisha *return* ya kodi ya mapato

itakayoambatana na hesabu zilizokaguliwa na kuidhinishwa na Mkaguzi wa Hesabu.

(j) Kurekebisha jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kwanza kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Cooperative Income Tax*) toka asilimia 30 mpaka asilimia 10 kwa miaka mitano, kuanzia mwaka mwekezaji atakapoanza uzalishaji kwa kuunganishaji wa magari, matreta na boti za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuongeza ajira na kuhamasisha wahaulishaji wa teknolojia (*technology transfer*). Aidha, Serikali itaingia Mkataba wa Makubaliano ya Utekelezaji (*Performance Agreement*) kwa kila muunganishaji ambapo utaainisha wajibu wa kila upande.

Pili, ni kurekebisha muda uliotolewa katika kutoza kodi mbadala (*Alternative Minimum Tax*) kwa kampuni zinazopata hasara kwa miaka mitatu mfululizo badala ya miaka mitano mfululizo kama ilivyobainishwa hivi sasa katika aya ya 3(3). Lengo la hatua hii ni kuoanisha na kifungu cha nne cha Sheria hiyo kilichobainisha kwamba kodi hiyo inatozwa kwa miaka miaka mitatu mfululizo.

Tatu, kwenye aya ya nne kwa kuongeza aya ndogo ya (d) ili kubainisha kwamba kiwango cha kodi ya zuio kwa wachimbaji wadogo wa madini ni asililimia tano.

(k) Kurekebisha aya ya 3(9)(b) ya jedwali la tatu ili kuongeza kiwando cha juu kinachotumika kama gharama ya kukokotoa uchakavu wa magari yasiyo ya kibiashara (*non commercial motor vehicles*) kutoka shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuhuisha gharama za magari hayo ziendane na gharama halisi za soko. Marekebishi aya yamezingatia kwamba kiwango cha sasa cha shilingi milioni 15 ni cha muda mrefu na hakiakisi bei halisi ya magari kwa sasa katika soko.

(l) Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa kuitia jedwali la marekebisheso, inapendekeza kurekebisha katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha 31(a) ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango ya matangazo kwa nchi nzima ambao hivi sasa unakusanywa na Halmashauri.

(b) Kufuta kifungu cha 67 na kukiandika upya ili kufanya marekebisheso ya kiwango cha faini kwa makosa ya watakaokiuka masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa kutoka kiasi kinachotozwa hivi sasa kisichozidi sh.50,000/= na kifungo kisichozidi miezi 12 hadi kiasi kisichopungua sh.200,000/= na kisichozidi sh.1,000,000/= au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miaka miwili.

(c) Kurekebisha jedwali la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili:-

Moja, kupunguza ushuru wa mazao (*Produce Cess*) unaotozwa na Halmashauri za Wilaya kutoka kiwango cha sasa cha 5% ya thamani ya mazao hadi 3% kwa mazao ya biashara na mazao ya chakula kama iliyobainishwa kuitia jedwali la marekebisheso.

Pili, ni kutotoza ushuru wa mazao kwa yeoyote anayesafirisha mazao yake kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine isiyozidi tani moja isitozwe ushuru. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wakulima kulipwa bei stahiki ya mazao yao na hivyo kuboresha mapato yao. Hatua hii inatarajiwa kuhamasisha uzalishaji wa mazao.

Tatu, ni kufuta ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye vibali vyatya machinjio isipokuwa Ada ya Machinjio, Ada ya Ulaguzi wa Nyama na Ada ya Vibali vyatya Kuanzisha Maduka ya Dawa.

Nne, kufuta ushuru wa mabango yanayoelekeza mahali huduma za jamii kama Shule, Hospitali au Zahanati; na tano, ni kufuta ushuru wa Huduma (*Service Levy*) kwenye nyumba za kulala wageni ambazo zinatozwa ushuru wa hotel.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura 123 kama ifuatavyo:-

(a) Ni kubainisha kuwa sehemu hii itaanza kufanya kazi pindi Waziri wa Nishati na Madini atakapotangaza kwenye Gazeti la Serikali ili kutoa nafasi ya maandalizi ya kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo husika.

(b) Kurekebisha Kifungu cha 18 na 19(3) na kuongeza Kifungu cha 18(a) na 90(a) ili:-

Kwanza, kuzuia uondoaji wa madini kutoka migodini na kusafirisha moja kwa moja nje ya nchi au kwa matumizi ya hapa nchini hadi hapo madini hayo yatakapokaguliwa kwenye vituo maalum na kulihiwa Ada ya Ukaguzi;

Pili, kuweka sharti la ulipaji wa Ada ya Ukaguzi wa Madini ya kiwango cha 1% ya thamani ya madini husika kabla ya kusafirisha moja kwa moja nje ya nchi au kwa matumizi ya hapa nchini.

Tatu, ni kuanzisha maeneo maalum ya ukaguzi na kudhibitishwa (*clearing centers*) katika viwanda vya ndege, migodini, bandarini, mipakani na sehemu nyingine zozote ambazo zitatangazwa na Waziri wa Nishati na Madini.

(c) Kurekebisha Kifungu cha 112(2) kwa kuongeza aya ya (t) ili kuwezesha waandaaji wa kanuni kubainisha taratibu za ukaguzi wa madini kabla ya kusafirishwa. Aidha, kupitia jedwali la marekebisho. Sehemu hii imefanyiwa marekebisho ya kiuandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali ya marekebisho, inapendekeza makerebiso katika Kifungu cha 17 cha Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297 ili kuondoa sharti la kulipa Ada ya Usalama mahali pa kazi kwa shule binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 67 cha Sheria ya Bandari, Sura 166 ili kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kkusanya Tozo ya Bandari (*wharfage*). Aidha, mapato husika yatahifadhiwa kwenye akaunti itakayofunguliwa Benki Kuu; fedha hizo zitarejeshwa Mamlaka ya Bandari kwa matumizi na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha (6) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kwa kuongeza Kifungu cha 6(a) ili:-

Kwanza, kutambua ndani ya Sheria ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Wizara na Taasisi za Serikali, uitwao *Government E-payment Gateway System*; na

Pili, kuweka sharti kwa Wizara na Taasisi na Serikali kutumia mfumo huu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato kwa utaratibu utakaowekwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza marekebisha Sheria ya Mamlaka ya Mapato, Sura 399 ili kurekebisha Kifungu cha 16 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (8) ili kuwawezesha Maafisa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuiwakilisha mamlaka kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwenye mashauri mbalimbali ya kimahakama au upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia jedwali za marekebisho, sehemu (b) ya jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399 imerekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya 50 ili kuhuisha Sheria ya Bandari, Sura 166. Marekebisho haya yana lengo la kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya Tozo ya Bandari (*wharfage*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu, kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya marekebisho ya kiuandishi katika Kifungu cha 8(1), 47(1), 54, 81(4) na 95 ili kuleta maana iliyokusudiwa.

(b) Kuongeza Kifungu cha 22(a) ili kuwatambua wafanyabiahara wadogo na kuwapa vitambulisho. Lengo la hatua hii ni kuwatambua watoa huduma za chakula, (*Caterers*) washereheshazi (*Masters of Ceremony*) katika shughuli mbalimbali na wafanyabiashara wadogo wasio rasmi. (*Makofi*)

(c) Kurekebisha Kifungu cha 52 ili kwanza kufanya marekebisho ya kiuandishi; na pili, kumwezesha Kamshina Mkuu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa maamuzi katika pingamizi mbalimbali za kikodi (*Tax Objections*) ambazo ni zaidi ya ukokotoaji kodi.

(d) Kupitia jedwali ya marekebisho, mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 53(1) kupitia lbara ya 52 yamefutwa, ili utaratibu ulipo hivi sasa kuhusu aina ya rufani zinaweza kuwasilishwa kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi Tanzania na mlipa kodi ubaki kama ulivyo.

(e) Kurekebisha Kifungu cha 64(2) ili kwanza kufanya marekebisho ya kiuandishi na pili, kwa kuongeza aya mpya ya (e) ili kuwezesha taratibu za ukamataji na udhibiti wa makosa ya kodi kutumika kwa makosa yanayohusisha matumizi ya mashine za hesabu za kieletroniki (*Electronic*

*Fiscal Devices - EFDs).* Lengo la hatua hii ni kuimarisha na kuongeza matumizi ya mashine hizo katika biashara mbalimbali na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

(f) Kufuta Kifungu cha 70 ili kufanya marekebisho kiuandishi na kuongeza vifungu vidogo vya (2) na (3) ili kumpa mamlaka Kamshina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kusamehe riba inayotozwa kwa walipa kodi wanaochelewa kulipa kodi iwapo ataona kuna sababu ya msingi ya kusamehe riba husika. Aidha, Kamshina amepewa mamlaka ya kupunguza riba isiyozidi asilimia 50. Hivi sasa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, ndiye mwenye mamlaka ya kusamehe riba husika.

(g) Kurekebisha Kifungu cha 71 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3) ili kuweka muda wa ukomo wa kudai marejesho ya kodi ambayo italipwa zaidi ya kiwango halisi. Hatua hii inakusudia kuweka utaratibu mzuri wa kurejesha madai husika ili kuondoa usumbufu wa walipa kodi.

(h) Kurekebisha Kifungu cha 75 kwa kufuta Kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya ili kuleta maana iliyokusudiwa na kuondoa utata kuhusu utaratibu wa ukokotoaji wa riba.

(i) Kurekebisha Kifungu cha 76 kwa kufuta Kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya ili kuweka riba ya kiwango kilichopo kisheria (*Statutory Rate Compounded Monthly*) kwa mlipa kodi ye yeyote atakayechelewa kulipa kodi baada yakumalizika kwa muda uliopangwa (*due date*). Aidha, ulipaji wa riba husika hautaathiriwa kwa sababu ya ucheleweshaji wa mashauriano Mahakamani na kadhalika.

(j) Kuongeza Kifungu cha 92(a) ili kubainisha kwamba fedha atakazotozwa mlipa kodi kama faini na adhabu chini ya sheria yoyote ya kodi zitakusanywa na Kamishna Mkuu wa *TRA* kama kodi ama madeni mengine ya Serikali.

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(k) Kurekebisha Jedwali la kwanza ili kwanza kufanya marekebisho ya kiuandishi katika aya ya (1), (2) na ya (3), lakini pili kuongeza aya ndogo mpya ya (e) kwenye aya ya 2(1) ili kuwezesha notisi za madai ya kodi ya majengo zitolewazo na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kutambulika kuwa ni notisi ya ukokotoaji kodi (*tax assessment notices*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Nne, kama ilivyorekebishesha kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura ya 289, kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha vifungu vya (3) na (6) ili:-

(i) Kuweka tafsiri ya maneno *rate, ratable area* na *ratable property* ili kurahisisha utekelezaji wa sheria.

(ii) Kuweka tafsiri sahihi ya nyumba zinazopaswa kutozwa kodi ili kutotoza kodi ya majengo kwenye nyumba za wananchi maskini zilizojengwa kwa miti, udongo, nyasi au nyumba za tembe. (*Makofii*)

(iii) Kubainisha kwamba *TRA* itakusanya kodi ya majengo kwenye Majiji, Mijini na Miji Midogo.

(b) Kurekebisha kifungu cha 16 ili:-

(i) Kutoza kodi ya majengo kwa nyumba zote katika Majiji, Miji na Miji Midogo kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Nyumba ambazo hazijafanyiwa uthamini zitatozwa kwa kiwango maalum (*flat rate*) cha Sh.10,000 kwa nyumba na Sh.50,000 kwa nyumba za ghorofa kwa kila ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba majengo yote yanayostahili kulipa kodi hii yanalipa ili kuongeza mapato ya Serikali na kuweka usawa katika utozaji wa kodi na kuweka tafsiri ya maneno mbalimbali.

(ii) Kwa majengo ya ghorofa yenyе nyumba zinazojitegemea zaidi ya moja (*apartments*) kila nyumba itatozwa kodi ya majengo kwa kujitegemea.

(iii) Kubainisha kwamba kodi ya majengo itakayokusanya na *TRA* itahifadhiwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, itarejeshwa kwenye Halmashauri husika kulingana na bajeti ya Halmashauri husika.

(iv) Kubainisha tafsiri ya majengo yatakayotozwa kodi ya majengo kwa kuondoa nyumba za tembe, nyasi na nyingine zinazofanana na hizi. Aidha, kupitia Jedwali la Marekebisho, Ibara ya 66(a) ya Muswada imefutwa ili kurejesha sharti kwa Waziri wa Fedha na Mipango kufanya mashauriano na Waziri wa TAMISEMI wakati wa kuweka viwango vya kodi ya majengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tano, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha 59, kwanza kwa kufanya marekebisho ya kiuandishi na pili kurekebisha aya ya (3) kwa kuongeza aya ndogo ya (e) ili kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri (0) katika huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa, mizigo nje ya nchi (*ancillary transport services*).

Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za usafirishaji katika bandari zetu na kuifanya Tanzania kuwa njia bora zaidi ya kupitisha bidhaa zinazotoka nje ya nchi

kwenda kwenye nchi nyingine hususani zisizo na bandari (*land locked countries*). Hatua hii itahamasisha wasafirishaji kutoka nchi jirani kuitisha mizigo yao kwa wingi kwenye bandari zetu na hivyo kukuza uchumi wa nchi kutokana na kuongezeka kwa mapato ya bandari na kuchangia kuongezeka kwa ajira nchini. (*Makofii*)

(b) Kurekebisha kifungu cha 66 kwa kuongeza kifungu cha (7) ili kubainisha kwamba endapo siku ya kulipa kodi au kuwasilisha *return* za kodi itaangukia siku za Jumamosi, Jumapili au siku nyingine za mapumziko, ulipaji wa kodi au uwasilishaji wa *return* za kodi utafanyika siku ya kazi itakayofuatia baada ya siku hizo za mapumziko kupita.

Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha sheria hii na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na kuondoa mkanganyiko wa siku ya kulipa kodi na kuwasilisha *return* ili kuwaondolea usumbufu walipa kodi.

(c) Kurekebisha Kifungu cha 74(2) kwa kufuta maneno *twelve months* na kuweka *eighteen months* ili kuwianisha muda wa kufuta madeni sugu kuwa miezi kumi na nane na kuondoa mkanganyiko wa kipindi cha kufuta madeni sugu ambapo Kifungu cha 74(3) kinabainisha miezi kumi na nane wakati Kifungu cha 74(2) kinabainisha miezi kumi na mbili.

(d) Kurekebisha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Misamaha kama ifuatavyo:-

(i) Kwenye Kifungu cha (3) kwa kufuta aya ya 19 na kuiandika upya ili kuondoa msamaha kwenye tumbaku iliyosindikwa.

(ii) Kuongeza aya mpya ya 32 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyakula vyatia mifugo

(compounded animal feeds) vinavyotengenezwa hapa nchini, vinavyotambulika kwenye HS Code 2309. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za kununua vyakula hivyo kwa wafugaji. (*Makof*)

(iii) Ni kuongeza aya ya 33 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mayai ya kutotolesha vifaranga (*fertilized eggs for incubation*).

Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji wa vifanga na kukuza sekta ndogo ya ufugaji ili iweze kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. (*Makof*)

(iv) Kufanya marekebisho ya kifungu kidogo cha (8) kwa kuongeza aya ndogo ya 10 ili kutoa msamaha kwenye magari yaliyotengenezwa maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. (*Makof*)

(v) Kurekebisha Sehemu ya Pili ya Jedwali la Misamaha ya kodi kwa kuongeza aya mpya ya 17, 18, 19, 20 na 21 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani:-

Kwanza, kwenye bidhaa za mtaji na hivyo kupunguza gharama za ununuzi au uingizwaji wa mashine za mitambo ya kuzalishia na hivyo kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Aidha, hatua hii itahusisha viwanda vya mafuta ya kula, nguo, ngozi, madawa ya binadamu na mifugo. (*Makof*)

Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika sekta za viwanda, kilimo cha mazao na mifugo na kukuza ajira na uchumi wa nchi. Aidha, hatua hii itawezesha viwanda vidogo na vya kati kupata unaifuu wa gharama za kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mashine na mitambo watakayonunua kwa ajili ya kusindika na kutengeneza

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

bidhaa mbalimbali. Mitambo na mashine zote zitakazosamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani zitaainishwa kwa kutumia *HS Codes*.

Pili, ni kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa magari ya kubeba wagonjwa yatakayoingizwa na vituo vya afya vilivyo sajiliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Sita, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura ya 82 ili kufuta tozo ya mafunzo ya ufundi stadi kwa shule za awali, msingi na sekondari pamoja na vyuo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Saba, inapendekeza marekebiso katika Kifungu cha 20A cha Sheria ya Reli, Sura ya 170 ili kutoa msamaha wa tozo wa maendeleo ya reli kwenye mafuta ya ndege (*Jet A1*). Lengo la marekebiso haya ni kuvutia Mashirika ya Ndege za Kimataifa kujaza mafuta hapa nchini badala ya nchi jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya bajeti zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia kanuni na matangazo ya Serikali (*Government Notices*) kwa mujibu wa matakwa ya sheria husika na hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kufuta ada ya ukaguzi wa viwango, mionzi na wakala wa vipimo kwenye mbolea inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania, Tume ya Mionzi Tanzania na Wakala wa Vipimo Tanzania. (*Makof*)

(ii) Kufuta ada ya ukaguzi wa viwango kwa mazao ya biashara kama pamba, chai, korosho na kahawa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania. (*Makof*)

(iii) Kuweka utaratibu wa namna mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki (*Electronic*

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*Revenue Collection Payment System (ERCS) utakavyofanya kazi.*

(iv) Kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari ili ada husika ilipwe mara moja tu pale gari linaposajiliwa na kuongeza viwango vya ada husika.

(v) Kufuta ada ya kufanya Tathmini ya Mazingira (*Environmental Impact Assessment*) kwa wawekezaji wote wa viwanda. (*Makofi*)

(vi) Vyombo vya uvuvi vilivyosajiliwa nchini kulipa tozo kwa kutumia shilingi za Kitanzania badala ya fedha za kigeni. (*Makofi*)

(vii) Kufuta ada ya zima moto inayotozwa katika shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayoyapendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria bajeti iliyokwisha kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**SPECIAL BILL SUPPLEMENT**

No. 1

20<sup>th</sup> June, 2017

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.3. Vol.98 dated 20<sup>th</sup> June, 2017  
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government*

---

THE FINANCE ACT, 2017

ARRANGEMENT OF PARTS

*Part Title*

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

- PART II AMENDMENT OF THE BANK OF TANZANIA ACT,  
(CAP.197)
- PART III AMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND POSTAL  
COMMUNICATIONS ACT, (CAP.306)
- PART IV AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT,  
(CAP.147)
- PART V AMENDMENT OF THE GAMING ACT, (CAP.41)
- PART VI AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT, (CAP.332)
- PART VII AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT FINANCE ACT,  
(CAP.290)
- PART VIII AMENDMENT OF THE MINING ACT, (CAP.123)
- PART IX AMENDMENT OF THE OCCUPATIONAL HEALTH AND SAFETY ACT,  
(CAP. 297)
- PART X AMENDMENT OF THE PORTS ACT, (CAP.166)
- PART XI AMENDMENT OF THE PUBLIC FINANCE ACT, (CAP.348)
- PART XII AMENDMENT OF THE TANZANIA REVENUE AUTHORITY ACT,  
(CAP. 399)
- PART XIII AMENDMENT OF THE TAX ADMINISTRATION ACT,

*The Finance Act, 2017*

---

(CAP. 438)

PART XIV AMENDMENT OF THE URBAN AUTHORITIES (RATING) ACT, (CAP. 289)

PART XV AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT, (CAP.148)

PART XVI AMENDMENT OF THE VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING ACT, (CAP.82)

*The Finance Act, 2017*

---

**NOTICE**

---

This Bill to be submitted to the National Assembly was published as a Bill Supplement No.3 of 2<sup>nd</sup> June, 2017 and was First Read in the National Assembly on 14<sup>th</sup> day of June, 2017. This Bill is now re-published for purposes of Second Reading and Third Reading.

Dar es Salaam,  
19<sup>th</sup> June, 2017

**JOHN W. H. KIJAZI**  
*Secretary to the Cabinet*

**A BILL**

*for*

**An Act to impose and alter certain taxes, duties, levies, fees and to amend certain written laws relating to the collection and management of public revenues.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

**PART I**  
**PRELIMINARY PROVISIONS**

Short title

**1.** This Act may be cited as the Finance Act, 2017.

Commenceme  
nt

**2.** This Act shall come into operation on the 1<sup>st</sup> day of July, 2017.

**PART II**  
**AMENDMENT OF THE BANK OF TANZANIA ACT,**  
**(CAP.197)**

Construction  
Cap.197

**3.** This Part shall be read as one with the Bank of Tanzania Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

*The Finance Act, 2017*

---

Amendment of  
section 32

- 4.** The principal Act is amended in section 32 by-
- (a) deleting the word "may" appearing in subsection (1) and substituting for it the word "shall";
  - (b) adding immediately after subsection (2) the following:
    - "(3) All Government and public authorities shall open and deposit all their moneys with the Bank.
    - (4) The Bank may make regulations for the better carrying out of the provisions of this section."

PART III  
AMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND  
POSTAL COMMUNICATIONS ACT,  
(CAP.306)

Construction  
Cap. 306

- 5.** This Part shall be read as one with the Electronic and Postal Communications Act hereinafter referred to as the principal Act.

Amendment of  
section 3

- 6.** The principal Act is amended in section 3 by deleting the interpretation of the word "local shareholder".

Amendment of  
section 26

- 7.** Section 26 of the principal Act is amended in section 26-

- (a) in subsection (1) by deleting paragraph (a) and substituting for it the following:
  - "(a) in the case of network facilities or network service licensee, have a minimum of public shareholding of twenty five percent of its issued and paid up share capital, as an ongoing obligation throughout the life of its licence";
- (b) in subsection (2) by deleting the word "local" and substituting for it the word "public";
- (c) by deleting the words " application services" wherever they appear in subsections (3), (4) and (5);
- (d) by inserting a new subsection (6) as follows:
  - (6) Where after conducting an initial

*The Finance Act, 2017*

---

public offer a licensee referred to in section 26(1)(a) fails to obtain the twenty five percent of its issued and paid up share capital, the Capital Markets and Securities Authority shall, upon consultation with the Minister responsible for Capital Markets and after taking into account conditions prevailing in the market, issue directives on how the licensee may obtain the twenty five percent."

**PART IV**  
**AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT,**  
**(CAP.147)**

Construction  
Cap.147

**8.** This Part shall be read as one with the Excise (Management and Tariff) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of  
Fourth  
Schedule

**9.** The principal Act is amended in the Fourth Schedule by introducing new rates in respect of excisable items as follows:

**"FOURTH SCHEDULE**

*(Made under section 124(2))*

Headin g	H.S. Code No.	Description	Un it	Old Excise Rate	New Excise Rate
20.09		Fruit juices (including grape must) and vegetable juices, unfermented and not containing added spirit, whether or not containing added sugar or other sweetening matter.	<i>l</i>	Tshs. 9.50 per litre	Tshs. 9.00 per litre
		Locally produced fruit juices manufactured from domestic fruits under heading 20.09			
		Other fruit juices under the	<i>l</i>	Tshs. 210.00	Tshs.

*The Finance Act, 2017*

		heading 20.09		per litre	221.00 per litre
22.01		<b>Waters, including natural or artificial mineral waters and aerated waters, not containing added sugar or other sweetening matter or flavoured; ice and snow.</b>			
	2201.10.00	-Mineral waters and aerated waters			
		Locally produced, bottled	/	Tshs. 58.00 per litre	Tshs. 58.00 per litre
		Imported, bottled	/	Tshs. 58.00 per litre	Tshs. 61.00 per litre
	2201.90.00	-Other	/		
		Locally produced, bottled	/	Tshs. 58.00 per litre	Tshs. 58.00 per litre
		Imported, bottled	/	Tshs. 58.00 per litre	Tshs. 61.00 per litre
22.02		<b>Waters, including mineral waters and aerated waters, containing added sugar or other sweetening matter or flavoured, and other non-alcoholic beverages, not including fruit vegetable juice of heading 20.09</b>			
	2202.10.00	- Waters, including mineral waters and aerated waters, containing added sugar or other sweetening matter or flavoured	/	Tshs. 58.00 per litre	Tshs. 61.00 per litre
		- Other			
	2202.91.00	-- Non-alcoholic beer	/	Tshs. 534.00 per litre	Tshs. 561.00 per litre
	2202.99.00	-- Other		Tshs. 534.00 per litre	Tshs. 561.00 per litre
22.03		<b>Beer made from malt</b>			
	2203.00.10	--Stout and porter	/	Tshs. 729.00 per litre	Tshs. 765.00 per litre
	2203.00.90	--Other	/	Tshs. 729.00 per litre	Tshs. 765.00 per litre

*The Finance Act, 2017*

22.04		<b>Wine of fresh grapes, including fortified wines; grape must other than that of heading 20.09</b>		
2204.10.00	- Sparkling wine			
	With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 202.00 per litre	Tshs. 200.00 per litre
	Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre	Tshs. 2,349.00 per litre
		-Other wine; grapes must with fermentation prevented or arrested by the addition of alcohol:		
	2204.21.00	-- In containers holding 2 litres or less		
	2204.21.00	With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 202.00 per litre
		Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre
		-- In containers holding more than 2 litres but not more than 10 litres		
	2204.22.00	With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 202.00 per litre
		Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre
		-- Other		
	2204.29.00	With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 202.00 per litre
		Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre
	2204.30.00	- Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre
22.05		<b>Vermouth and wine of fresh grapes flavoured with plants or aromatic substances</b>		

*The Finance Act, 2017*

	2205.10.00	- In containers holding 2 litres or less			
		With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 202.00 per litre	Tshs. 200.00 per litre
		Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre	Tshs. 2,349.00 per litre
	2205.90.00	- Other	/	Tshs. 2,236.00 per litre	Tshs. 2,349.00 per litre
22.06		<b>Other fermented beverages (for example, cider, perry, mead, sake); mixtures of fermented beverages and mixtures of fermented beverages and non-alcoholic beverages, not elsewhere specified or included.</b>			
	2206.00.10	--- Cider	/	Tshs. 2,236.00 Per litre	Tshs. 2,349.00 Per litre
	2206.00.20	--- Opaque beer (for example Kibuku)			
		Beer made from 100% local unmalted cereals	/	Tshs. 429.00 per litre	Tshs. 450.00 per litre
22.08		<b>Undenatured ethyl alcohol of an alcoholic strength by volume of less than 80% vol; spirits, liqueurs and other spirituous beverages.</b>			
	22.08	All locally produced products of this heading	/	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,315.00 per litre
		Other imported products of this heading as follows:			
	2208.20.00	-Spirits obtained by distilling grape wine or grape marc	/	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
	2208.30.00	-Whiskies	/	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
	2208.40.00	-Rum and other spirits obtained by drilling fermented sugar – cane products	/	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre

*The Finance Act, 2017*

	2208.50.00	- Gin and Geneva	<i>l</i>	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
	2208.60.00	- Vodka	<i>l</i>	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
	2208.70.00	- Liqueurs and cordials	<i>l</i>	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
		-Other			
	2208.90.10	--- Distilled Spirits ( e.g. Konyagi, Uganda Waragi)	<i>l</i>	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
	2208.90.90	--- Other	<i>l</i>	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,481.00 per litre
24.02		<b>Cigars, cheroots, cigarillos and cigarettes, of tobacco or of tobacco substitutes.</b>			
	2402.10.00	- Cigars, cheroots and cigarillos, containing tobacco	<i>k</i> <i>g</i>	30%	30%
		-Cigarettes containing tobacco			
	2402.20.10	--- Of length not exceeding 72mm length including the filter tip			
		Without filter tip and containing domestic tobacco exceeding 75%	<i>m</i> <i>il</i>	Tshs. 11,854.00 per mil	Tshs. 12,447.00 per mil
		With filter tip and containing domestic tobacco exceeding 75%	<i>m</i> <i>il</i>	Tshs. 28,024.00 per mil	Tshs. 29,425.00 per mil
		Other	<i>m</i> <i>il</i>	Tshs. 50,700.00 per mil	Tshs. 53,235.00 per mil
	2402.20.90	---Other			
		Without filter tip and containing domestic tobacco exceeding 75%	<i>m</i> <i>il</i>	Tshs. 11,854.00 per mil	Tshs. 12,447.00 per mil
Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura ya 82 kwa lengo la kusamehe tozo la Elimu ya Ufundı stadi kwa mashule na vyuo binafsi ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za uendeshaji na hivyo kuwawezesha kutoa elimu iliyo bora zaidi kwa gharama nafuu kwa wazazi.

Dodoma,

**PHILIP I. MPANGO**

16 Juni, 2017  
*Mipango*

*Waziri wa Fedha na*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu mwingine. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 8 Juni 2017, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa kupata mapato ya kugharamia bajeti yake kwa mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti imeujadili kwa kina Muswada huu kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge waliyoyatoa wakati wa mjadala wa Bajeti ya Serikali pamoja na maoni na mapendekezo ya wadau waliyoyatoa wakati wa mjadala wa Muswada huu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya mashauriano, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyachukua maoni na mapendekezo yaliyotolewa na hatimaye kufikia hatua ya kuuchapisha tena Muswada huu ili uweze kukidhi mabadiliko hayo pamoja na Waheshimiwa Wabunge waweze kuusoma na kuuelewa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeongezewa marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu, Sura 192; Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura 306; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297 na Sheria ya Bandari, Sura 166.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa usikivu wake mkubwa na kuchukua maoni mengi ya Kamati na hatimaye kuuandika upya Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sheria hizi, ni matokeo ya mjadala wa mchakato mzima wa Bunge la Bajeti na hivyo sasa Bunge lako Tukufu linakwenda kupitishia Muswada huu ili Serikali iweze kukusanya mapato yake kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 pamoja na marekebisho yake una lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Hivyo, Bunge lako Tukufu linaombwa kuhalalisha kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zitakazoanza kukusanya na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Muswada. Kamati ya Bajeti imepokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya kuboresha Muswada huu. Kamati pia imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu. Baada ya kujiridhisha na maudhuhi husika, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango na Watendaji wa Wizara yake pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake kuhusu marekebisho ya Sheria Kumi na Tano zilizopo kwenye Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchambua Muswada huu, Kamati imetoea maoni ya jumla ambayo yana lengo la kuishauri Serikali iweze kuyafikiria kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mapato kwa Serikali. Hivyo, taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya mashauriano hayo na naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2017. Sheria ya Benki Kuu, Sura 192. Kamati ya Bajeti imeridhia marekebisho ya sheria hii, Kifungu cha 32 ambacho kinaweka masharti kwa taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kufungua akaunti ya fedha zake Benki Kuu ya Tanzania. Hatua hii inazidi kuongeza udhibiti wa matumizi ya fedha za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura ya 306. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kufanya marekebisho Sheria ya *EPOCA* kifungu cha tatu (3) na 26 ambapo kwa sasa itaondoa sharti lililopo kwa mujibu wa sheria ya kuuza hisa husika kwa raia wa Tanzania pekee na hivyo sasa hisa hizo zitauzwa pia kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi; kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja balna ya Watanzania na raia wa nje; raia na kampuni au taasisi za nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au raia na kampuni kutoka nchi nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, marekebisho haya yameondoa kampuni ndogo za mawasiliano ambazo zina leseni ya *application service* kwenye sharti la kuuza hisa kwenye soko la hisa ili kubaki na kampuni kubwa za mawasiliano zenye leseni ya *network facility* au *network service*. Kamati inapongeza hatua hii kwani inakuza kampuni ndogo za mawasiliano ambazo nyingi ni za Watanzania wenzenetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kampuni ya simu itakayoshindwa kufikia mauzo ya asilimia 25 kutohana na kutofaulu kwa toleo la umma, Kamati inashauri kuwa kwenye maelekezo yatakayotolewa na Waziri mwenye dhamana kuhusu namna kampuni husika itakavyoweza kutoa hisa na kufikia asilimia 25, basi yaelekeze namna bora ya kuuza hisa kwa awamu mbili kulingana na mwenendo wa soko bila kuathiri takwa la kisheria la mauzo ya asilimia 25. Aidha, Kamati inasisisiza kuwa Serikali ikamilishe haraka taratibu zote za kisheria zitakazoruhusu kuandikishwa kwa hisa husika kwenye soko la hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha viwango maalum vya ushuru vinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa kiwango cha mfumuko wa bei cha asilimia tano5. Utaratibu huu ni tofauti na pale ambapo ushuru wa bidhaa hutozwa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti inakubaliana na marekebisho ya baadhi ya viwango vya ushuru vilivyowasilishwa na Serikali kupitia taarifa ya Bajeti ya Serikali iliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yake kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikubaliani na hatua ya Serikali ya kuongeza Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji baridi kutoka Sh.58/= kwa lita hadi Sh.61/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.3/= kwa lita. Kamati inashauri Serikali kutoendelea kuongeza Ushuru wa Bidhaa kwa vinywaji baridi vinavyozalishwa ndani ili kuiwezesha sekta hii kuendelea kukua na kuleta manufaa makubwa kwa Taifa hususani kuongeza ajira, kukuza uchumi na kuongeza ukusanyaji wa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali haikupandisha ushuru wa vinywaji baridi. Hatua hiyo iliwezesha sekta hii kukua na kupanua uwekezaji kwa kiasi takribani shilingi bilioni 800 katika kipindi cha miaka mitatu. Uamuzi huo wa Serikali uliweza kuongeza ukuaji wa mapato ya Serikali. Aidha, Ushuru huu wa Bidhaa kwa upande wa nchi za SADC unatozwa Tanzania (asilimia tano) na Angola (asilimia tatu) tu, nchi nyingine hazitozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuongeza Ushuru wa Bidhaa kiasi cha Sh.40/= kwa lita kwenye mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. Hatua hii imeweza Serikali kufidia ada ya mwaka ya leseni

ya magari (*Annual Motor Vehicle License Fee*) ambayo ilikuwa inalipwa hata kwa magari ambayo hayatumiki na hivyo kuwa kero kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti imeridhishwa na hatua ya Serikali katika kushughulikia suala la utozaji wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 kwa kampuni zinazoagiza sukari ya viwandani kama vile kampuni za vinywaji na madawa na baadaye Serikali kurejesha asilimia 15 baada ya kuthibitika kuwa imetumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inapendekeza utaratibu huu uangaliwe upya ili kuvinusuru viwanda kufilisika kutokana na madeni makubwa na malimbikizo ya riba. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali kurejesha kiasi cha takribani shilingi billioni 20 kwa kampuni zilizoingiza sukari za viwandani kwa ajili ya uzalishaji wa vinywaji na madawa. Kamati inatambua kuwa Serikali inatekeleza hatua hii ya kiutawala ili kuhakikisha sukari ya viwandani inatumika kama ilivyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati bado inaishauri Serikali kupunguza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 kwenye malighafi ya kutengeneza dawa ya meno (*laminates na tubes*) hadi asilimia 10. Hatua hii itasaidia kukuza uzalishaji wa viwanda vya kutengeneza dawa ya meno, mfano *Whitedent* ili viweze kushindana na viwanda vingine vilivyomo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji vya matunda yaani juisi na mvinyo unaozalishwa hapa nchini. Hatua hii itahamasisha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi husika pamoja na kukuza uzalishaji wa viwanda husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41. Kamati inapongeza Serikali kufanya marekebisho kwenye sheria hii kwa Kifungu cha 31, 31A na

32 ili Mamlaka ya Mapato iweze kukusanya kodi hizo kwa niaba ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inapendekeza na kukubaliana na Serikali kuongeza kodi kwenye michezo ya kubahatisha ili ongezeko hilo litakalopatikana liende kwenye Mfuko wa Mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Sehemu ya Sita ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kwa kurekebisha Kifungu cha tatu (3), 11, 14 na 19 cha sheria hii ili kufanya marekebiso mbalimbali ya kiuandishi kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa pendekezo la kutoza Kodi ya Zuio kwa wachimbaji wadogo wa madini pamoja na kuzuia ukwepajji wa Kodi ya Zuio itokanayo na mikataba ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebiso ya Kifungu cha 69 cha sheria husika ili kupanua wigo wa kutoza Kodi ya Zuio kwenye malipo yatokanayo na huduma ya bima ambayo hivi sasa haitozwi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na marekebiso ya kuongeza Kifungu cha 83B kwenye sheria husika ili kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia tano kwenye bei ya kuuzia ambayo itakuwa ni Kodi ya Zuio ya mwisho kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa kwenye marekebiso ya Sheria ya Madini itakayokuja lazima iainishe masoko ya vito vyta thamani ya ndani na kimataifa ili kusimamia vizuri pendekezo hili la kutoza kiwango cha asilimia tano kwenye bei ya kuuzia kwa wachimbaji wadogo. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kutafsiri upya neno la *industrial mineral* ambapo kwa sasa halitajumuisha madini ya chumvi, mchanga, mchanga wa bahari na kokoto ambayo kimsingi hayapaswi kutozwa kodi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inakubaliana na marekebisho ya Vifungu vya 86, 88, 90 na 91 vya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kurekebisha Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ambapo sasa kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni kinashuka kutoka asilimia 30 hadi 10 kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa uwekezaji kwa waunganishaji magari, matrektta na boti za uvuvi ili kuongeza ajira katika sekta hizi pamoja na kuhamasisha maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kushusha pia kiwango cha Kodi ya Mapato ya Kampuni kwa sekta ya viwanda vinavyohusu uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo pamoja na viwanda vya ngozi. Aidha, Serikali itoe msamaha wa kodi (*zero rate*) kwa viwanda vinavyotengeneza dawa za kilimo. Hatua hizi zote zitasaldia kukuza uchumi wa viwanda pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Kifungu cha 31A ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango nchi nzima ambao hivi sasa unakusanywa na Halmashauri. Kamati inapongeza hatua hii. Hata hivyo, inatoa angalizo kuwa pamoja na vigezo vingine, viwango vya ada za mabango vizingatie na aina ya biashara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inaanza kukusanya Kodi ya Majengo na Kodi ya Mabango ambazo hapo awali zilikuwa zinakusanywa na Halmashauri. Kamati inaona hatua hii ni nzuri. Hata hivyo, kwa kuwa hapo awali vyanzo hivi vilikuwa ni mapato ya Halmashauri husika, Kamati inapendekeza Serikali ihakikishe kuwa fedha zitakazokusanywa kwenye maeneo haya zinapelekwa kwenye Halmashauri husika kwa kuzingatia muda pamoja na bajeti zao kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho ya Jedwali la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa

ambayo inatoa fursa ya kupunguza na kufuta ada na tozo mbalimbali zinazohusu kilimo, machinjio na huduma kwenye nyumba za kulala wageni. Kamati inapongeza Serikali kwa kukubaliana na pendelekezo la Kamati la kutoza viwango sawa vya asilimia tatu kwa mazao ya chakula na biashara ili kuondoa utata. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini, Sura 123. Kamati inapongeza na kukubaliana na mapendelekezo ya Serikali ya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwa Kifungu vya 18, 19, 90A na 112 ambayo kimsingi yanafanya marekebisho ya kiuandishi, kuweka viwango vya tozo pamoja na kuwezesha uandaaji wa kanuni na taratibu za ukaguzi wa madini kabla ya kusafirishwa. Hata hivyo, kwa upande wa *clearance fee* ya kiwango cha asilimia moja ya thamani ya mzigoto, Kamati inapendelekeza kodi hii iongezewe kwenye mrabaha na hivyo kuongezeka kutoka asilimia nne hadi tano ya mrabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuondoa sharti la kulipa ada ya usalama mahali pa kazi kwa wamiliki wa shule binafsi. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama ya uendeshajji kwa shule husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Bandari, Sura 166. Kamati inatambua kuwa shughuli za kupakua, kuhifadhi na kusafirisha mizigo bandarini ni jukumu la Bandari. Kamati haina pingamizi na hatua ya Serikali kuleta kifungu kipyaa kidogo cha 67 cha Sheria ya Bandari ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa bandari na kuweka akaunti itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Kamati inashauri kuwa fedha zitakazokusanya na Mamlaka ya Kodi Tanzania zirudishwe kama zilivyokusanya kwa Mamlaka ya Bandari ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348. Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta marekebisho ya Kifungu cha sita (6) cha sheria hii ili kuweka mfumo wa kieletroniki (*Government E-payment Gateway System*) wa

ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Taasisi za Serikali. Hatua hii itaongeza ukusanyaji wa mapato pamoja na udhibiti wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, Sura ya 399. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 16 cha sheria hii kwa kuwawezesha maafisa wa Mamlaka ya Mapato kuiwakilisha mamlaka kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato. Hatua hii itasaidia kupunguza mlolongo wa mashauri ya kimahakama yanayowasilishwa na wadau wa Kodi kutoka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438. Sheria hii inakusudiwa kufanyiwa marekebisho ya kiuandishi katika Kifungu 8(1), 22A, 47(1), 52, 81(4) na 95 ili kuleta maana iliyokusudiwa. Pamoja na marekebisho haya Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wasio rasmi na wanaofanya biashara kwa kuwapatia vitambulisho. Aidha, Serikali imewatambua pia watoa huduma ya chakula, washereheshaji na wengine ili kuongeza wigo wa mapato na kupunguza sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 53 cha sheria hii, Kamati inapongeza Serikali kwa kukubali kifungu hiki kisifanyiwe marekebisho na hivyo kuendelea kuwa kama awali ambapo wadau wa kodi wana uhuru wa kupeleka mashauri yao katika Bodi ya Rufaa za Kodi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inakubaliana na marekebisho ya Kifungu na 75, 76 na 78 vinavyohusu utaratibu wa ukokotoaji wa riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya

marekebisho ya kiuandishi ya sheria hii ili kuanza kutoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote katika Majiji, Manispaa na Miji kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati inaipongeza hatua hii, hata hivyo, inatoa angalizo kuwa viwango vitakavyopangwa vizingatie uhalisia wa hali ya nyumba husika pamoja na matumizi yake. Aidha, tunapongeza Serikali kwa kukubali kwamba zoezi zima liwe shirikishi kwa kuishirikisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ilivyokuwa awali ili kutoa fursa ya kutambua maeneo husika pamoja na kuondoa usumbufu kwa wenyewe majengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 59 cha sheria husika kwa kuongeza muda wa kuhifadhi mizigo kutoka nje inayosafirishwa kwenda nje kupitia bandari zillizopo kutoka siku saba (7) hadi 30. Hatua hii itapunguza gharama ya usafirishaji na hivyo kukuza ushindani katika bandari zetu na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuondoa tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mizigo ya mbolea, *sulphur* na kemikali kwa ujumla, badala ya kutoza dola moja (1) kwa tani iendelee na utaratibu wake wa kutoza dola 100 kwa *bill of lading*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho ya Kifungu cha 66 na 74 ili kutoa fursa ya kulipa kodi nje ya muda unaotakiwa na hivyo kukuza utii wa hiari katika kulipa kodi pamoja na kutoa kipindi kirefu cha ulipaji wa madeni sugu. Hatua hii itasaidia kuongeza utiifu katika ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kufanyiwa marekebisho Sehemu ya Kwanza ya Jedwali ili kusamehe kodi inayotozwa kwenye vyakula vya mifugo na mayai pamoja na mashine za kutotoleshea vifaranga. Aidha, Sehemu ya Pili ya Jedwali inatoa fursa ya msamaha wa kodi kwenye bidhaa za mitaji hususani katika

uingizaji wa mashine na mitambo ya uzalishaji wa mafuta ya kula yatokanayo na mimea, nguo, madawa, ngozi kwa lengo la kukuza viwanda na kuvutia uwekezaji. Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta mapendekezo haya ambayo kimsingi yanalenga kukuza sekta ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura ya 82. Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada huu inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura 82 kwa lengo la kusamehe tozo ya elimu ya ufundı stadi kwa shule na vyuo binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kusikiliza kilio cha wamiliki wa shule binafsi pamoja na vyuo. Hatua hii itawasaidia kupunguza gharama ya uendeshaji kwa taasisi hizo. Kamati inasisitiza pia Serikali kuangalia na tozo nyngine zilizobaki ili kuendelea kupunguza mzigo wa gharama za uendeshaji wa shule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti pia ilipitia na kuchambua maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango wakati akihitimisha hoja za Waheshimiwa Wabunge walijadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kukubali kufanyia kazi baadhi ya hoja za msingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo kwa namna moja au nyngine zinahusu Muswada huu. Hivyo Kamati inatoa pongezi kwa hatua zifuatazo:-

(i) Kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magari ya wagonjwa.

(ii) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye ada na vibali vya uwindaji vitolewavyo na Serikali.

(iii) Kuondoa tozo ya kuendeleza Mafunzo ya Ufundı Stadi na ada ya zimamoto kwa wamiliki wa shule binafsi.

(iv) Kuondoa tozo ya *Railway Development Levy* kwa upande wa mafuta ya ndege (*JET-A1*) ili kupunguza gharama ya mafuta hayo na hivyo kuweza kukuza sekta ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haina pingamizi na hatua iliyochukua Serikali ya kuondoa ada ya Tathmini ya Mazingira kwa wawekezaji wa viwanda. Hata hivyo, Kamati inashauri suala hili liangaliwe upya ili Serikali itoze kodi hii kwenye viwanda na miradi mikubwa kwa kuzingatia viwango itakavyoona vinafaa. Hatua hii itatoa fursa ya kufanya Tathmini ya Mazingira na hivyo kulinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Naiba Spika, mapendekezo mengine ya Kamati kama yalivyo kwenye taarifa yangu, naomba yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa ya kuweza kuwasilisha taarifa hii ndani ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliendesha Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupatia pamoja na Mheshimiwa George Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada huu hatua kwa hatua hadi kufikia hatua hii ya kutoa maoni Bungeni.

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Pia niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijukana na Mheshimiwa Cosato Chumi kwa ushiriki wao makini katika hatua zote za uchambuzi wa Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee, namshukuru Dkt. Kashilillah, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa ofisi yake kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Napenda kuwashukuru Idara ya Bajeti iklongozwa na Mkurugenzi, Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi - Sehemu ya Uchambuzi wa Bajeti; Ndugu Mathew Kileo, Mkurugenzi Msaidizi - Sehemu ya Vyanzo Vipya vya Mapato na Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Makatibu wa Kamati, Ndugu Godwin Godfrey, Ndugu Maombi Kakozi na Ndugu Lilian Masabala kwa utaalalm wao wa uchambuzi na kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa ushirikiano wanaonipatia na kunifanya kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki cha tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru tena Waziri wa Fedha na Mipango kwa usikivu mkubwa ambao ameuonesha kwa Kamati katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA  
FEDHA YA MWAKA 2017 (*THE FINANCE ACT, 2017*) KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 (The Finance Act, 2017).

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba tarehe 08 Juni 2017; Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa Kupata Mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imeujadili kwa kina Muswada huu kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa wabunge waliyoyatoa wakati wa mjadala wa Bajeti ya Serikali pamoja na maoni na mapendekezo ya Wadau waliyoyatoa wakati wa mjadala wa Muswada huu. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba, baada ya mashauriano, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyachukua maoni na mapendekezo yaliyotolewa na hatimaye kufikia hatua ya kuuchapisha tena Muswada huu ili uweze kukidhi mabadiliko hayo pamoja na Waheshimiwa Wabunge waweze kuusoma na kuuelewa vizuri. Muswada huu umeongezewa marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu, Sura 192; Sheria ya Posta na Mawaasiliano ya Kieletroniki, Sura 306; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297; Sheria ya Bandari, Sura 166.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hizi ni matokeo ya mjadala wa mchakato mzima wa Bunge la

Bajeti na hivyo sasa Bunge lako tukufu linakwenda kupitishia Muswada huu ili Serikali iweze kukusanya mapato yake kisheria.

## **2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 pamoja na marekebisho yake una lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Hivyo Bunge lako Tukufu linaombwa kuhalalisha kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zitakazoanza kukusanya na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2017.

## **3.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti, imepokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya kuboresha Muswada huu. Kamati pia imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu. Baada ya kujiridhisha na maudhuhi husika, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango na Watendaji wa Wizara yake pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake kuhusu marekebisho ya **Sheria Kumi na Tano** zilizopo kwenye Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua Muswada huu, Kamati imetoea maoni ya jumla ambayo yana lengo la kuishauri Serikali iweze kuyafikiria kwa mwaka wa fedha 2017/18 ili kuendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mapato kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo, taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya mashauriano hayo na ninaomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

## **4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2017.**

### **4.1 Sheria ya Benki Kuu, Sura 192**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti imeridhia marekebisho ya Sheria Benki Kuu, Sura ya 192 kifungu cha 32 ambacho kinaweka masharti kwa taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kufungua akaunti ya fedha zake Benki Kuu ya Tanzania. Hatua hii inazidi kuongeza udhibiti wa matumizi ya Fedha za Umma

### **4.2 Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura ya 306**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza hatua ya Serikali ya kufanya marekebisho Sheria ya EPOCA kifungu cha 3 na 26 ambapo kwa sasa itaondoa sharti liliopo kwa mujibu wa Sheria ya kuuza hisa husika kwa raia wa Tanzania pekee na hivyo sasa hisa hizi zitauzwa pia kwa watanzania wanaoishi nje ya nchi, kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja baina ya watanzania na raia wa nje, raia na kampuni au taasisi za nchi Wanachama wa jumuia ya Afrika Mashariki au raia na kampuni kutoka nchi nyingine yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, aidha marekebisho haya yameondoa kampuni ndogo za mawasiliano ambazo zina leseni ya '*application service*' kwenye sharti la kuuza hisa kwenye soko la hisa ili kubaki na kampuni kubwa za mawasiliano zenye leseni ya '*network facility*' au '*network service*'. Kamati inapongeza hatua hii kwani inakuza kampuni ndogo za mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Kampuni ya simu itakayoshindwa kufikia mauzo ya asilimia 25 kutokana na kutofaulu kwa toleo la umma (*unsuccessful public offer*), Kamati inashauri kuwa kwenye maelekezo (*directives*) yatakayotolewa na Waziri mwenye dhamana kuhusu namna kampuni husika itakavyoweza kutoa hisa na kufika asilimia 25; basi yaelekeze namna bora ya kuuza hisa kwa awamu

mbili (*gradually*) kulingana na mwenendo wa soko bila kuathiri takwa la kisheria la mauzo ya asilimia 25. Aidha Kamati inasisitiza kuwa Serikali ikamilishe haraka taratibu zote za kisheria zitakazoruhusu kuandikishwa kwa hisa husika kwenye soko la hisa.

#### **4.3      Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha viwango maalumu vya ushuru (specific duty rates) vinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petrol kwa kiwango cha mfumuko wa bei cha asilimia 5. Utaratibu huu ni tofauti na pale ambapo Ushuru wa bidhaa hutozwa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa (*advalorem rates*). Kamati ya Bajeti inakubaliana na marekebisho ya baadhi ya viwango vya ushuru vilivyowasilishwa na Serikali kupitia taarifa ya Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yake kwenye maeneo yafuatayo:-

a)      Kamati haikubaliani na hatua ya Serikali ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi kutoka shilingi 58 kwa lita hadi shilingi 61 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 3 kwa lita. Kamati inashauri Serikali kutoendelea kuongeza ushuru wa bidhaa kwa vinywaji baridi vinavyozalishwa ndani ili kuwezesha Sekta hii kuendelea kukua na kuleta manufaa makubwa kwa Taifa hususani kuongeza ajira, kukuza uchumi na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Mfano katika mwaka wa fedha 2015/16; Serikali haikupandisha ushuru wa vinywaji baridi, hatua hiyo iliwezesha Sekta hii kukua na kupanua wekezaji kwa kiasi takribani shilingi Bilioni 800 katika kipindi cha miaka mitatu. Uamuzi huo wa Serikali uliweza kuongeza ukuaji wa mapato ya Serikali. Aidha, ushuru huu wa bidhaa kwa upande wa nchi za SADC unatozwa Tanzania (asilimia 5) na Angola (asilimia 3) tu, nchi nyingine hazitozi.

b) Hatua ya Serikali ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshw (beer from local unmalted cereals) kutoka shilingi 429 kwa lita hadi shilingi 450 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 21 kwa *I i t a* haitasaidia kupata mapato yanayokusudiwa na Serikali. Kamati ilishauri Serikali kufanya marekebisho katika Jedwali la nne la Ushuru wa bidhaa kwa kuweka viwango tofauti vya ushuru wa bidhaa wa bia inayozalishwa kwa kutumia kimea kilichoooteshwa na ambacho hakijaoteshw (Malted and Unmelted), ili kutoa motisha kwa makampuni ya bia kutumia kimea cha ndani kilichoooteshwa na ambacho hakijaoteshw (*Malted and unmalted*). Hali ilivyo hivi sasa kimea kinachozalishwa ndani kinatozwa ushuru wa bidhaa sawa na kimea kinachoagizwa kutoka nje. Lengo ni kukuza uchumi wa viwanda na kutoa soko kwa mazao ya wakulima; Serikali haina sababu zozote za msingi za kukataa pendekezo hili.

c) Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuongeza ushuru wa bidhaa kiasi cha shilingi 40 kwa lita kwenye mafuta ya petrol (kutoka 339 hadi 379), dizeli (kutoka 215 hadi 255) na taa (kutoka 425 hadi 465). Hatua hii imewezesha Serikali kufidia ada ya mwaka ya leseni ya magari (Annual Motor Vehisicle Licence Fee) ambayo ilikuwa inalipwa hata kwa magari ambayo hayatumiki na hivyo *k u w a* kero kwa wananchi.

d) Kamati ya Bajeti imeridhishwa na ahadi ya Serikali katika kushughulikia suala la utozaji wa ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia 25 kwa kampuni zinazoagiza sukari ya viwandani kama vile kampuni za vinywaji na madawa na baadae Serikali kurejesha asilimia 15 baada ya kuthibitika kuwa imetumika ipasavyo kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, Kamati inapendekeza utaratibu huu uangaliwe upya ili kuvinusuru viwanda kufilisika kutoana na madeni makubwa na malimbikizo ya riba. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali kurejesha kiasi cha takribani shilingi bilioni 20 kwa kampuni zilizoingiza sukari za viwandani kwa

ajili ya uzalishaji wa vinywaji na madawa. Kamati inatambua kuwa Serikali inatekeleza hatua hii ya kiutawala ili kuhakikisha sukari ya viwandani inatumika kama ilivyokusudiwa.

e) Kamati bado inashauri Serikali kupunguza ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye malighafi za kutengeneza dawa ya meno (*Laminates na tubes*) hadi asilimia 10. Hatua hii itasaidia kukuza uzalishaji wa viwanda vya kutengeneza dawa ya meno (*white dent*) ili viweze kushindana na viwanda vingine vilivyomo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

f) Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kupunguza ushuru wabidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) na mvinyo unaozalishwa hapa nchini. Hatua hii itahamasisha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi husika pamoja na kukuza uzalishaji waa viwanda husika.

#### **4.4 Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria hii kwa kifungu cha 31,31A na 32 ili Mamlaka ya Mapato iweze kuanza kukusanya Kodi hizo kwa niaba ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati imependelekeza na kukubaliana na Serikali kuongeza kodi kwenye Michezo ya Kubahatisha ili ongezeko hilo litakalopatikana liende kwenye Mfuko wa Mazingira.

#### **4.5 Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Sita ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kwa kurekebisha kifungu cha 3, 11, 14 na 19 cha Sheria hii ili kufanya marekebisho mbalimbali ya kiuandishi kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa pendekezo la kutoza Kodi ya Zuo kwa wachimbaji wadogo wa madini pamoja na kuzuia ukwepajji wa kodi ya zuio itokanayo na mikataba ya utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 69 cha sheria husika ili kupanua wigo wa kutoza kodi ya zolio kwenye malipo yatokanayo na huduma ya bima (*reinsurance*) ambayo hivi sasa haitozwi kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na marekebisho ya kuungeza kifungu cha 83B kwenye Sheria husika ili kutoza kodi ya zolio kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye bei ya kuuzia (*total market value*) ambayo itakua ni Kodi ya Zolio ya mwisho (*final withholding tax*) kwa wachimbaji wadogo wa madini. Kamati inashauri kuwa kwenye marekebisho ya Sheria ya Madini itakayokuja lazima ianishe masoko ya vito vya thamani ya ndani na kimataifa ili kuhakikisha na kusimamia vizuri pendekezo hili la kutoza kiwango cha asilimia 5 kwenye bei ya kuuzia (*total market value*) kwa wachimbaji wadogo. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kutafsiri upya neno la *industrial mineral* ambapo kwa sasa halitajumuishwa madini ya chumvi, mchanga, mchanga wa bahari na kokoto ambayo kimsingi hayapaswi kutozwa kodi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati inakubaliana na marekebisho ya kifungu cha 86, 88, 90 na 91 cha Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kurekebisha **Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato** ambapo sasa kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Corporate Income Tax*) kinashuka toka asilimia 30 hadi 10 kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa uwekezaji kwa waunganisha magari, matrekti na boti ya uvuvi ili kuungeza ajira katika sekta hizi pamoja na kuhamasisha maendeleo ya teknolojia. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kushusha pia kiwango cha Kodi ya Mapato ya Kampuni kwa sekta ya viwanda vinavyohusu uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo (*agro-processing industry*) pamoja na viwanda vya ngozi. Aidha, Serikali itoe msamaha wa kodi (*zero rate*) kwa viwanda vinavyotengeneza madawa ya kilimo (*agro-chemistry processing industry*). Hatua hizi zote zitasaidia kukuza uchumi wa viwanda pamoja na Kilimo.

#### 4.6 Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria hii kifungu cha 31A ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango nchi nzima ambao hivi sasa unakusanywa na Halmashauri. Kamati inapongeza hatua hii hata hivyo inatoa angalizo kuwa pamoja na vigezo vingine, viwango vya ada za mabango vizingatia na aina ya biashara husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sasa Serikali inaanza kukusanya Kodi ya Majengo na Kodi ya Mabango ambazo hapo awali zilikuwa zinakusanywa na Halmashauri. Kamati inaona hatua hii ni nzuri, hata hivyo kwa kuwa hapo awali vyanzo hivi vilikuwa ni mapato ya Halmashauri husika, Kamati inapendekeza Serikali ihakikishe kuwa fedha zitakazokusanywa kwenye maeneo haya zipelekwe kwenye Halmashauri husika kwa kuzingatia muda pamoja na bajeti zao kama zilivyoidhinishwa kwenye Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na marekebisho ya Jedwali la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ambayo yanatoa fursa za kupunguza na kufuta ada na tozo mbalimbali zinazohusu kilimo, machinjio na huduma kwenye nyumba za kulala wageni. Pamoja na hatua hii nzuri Kamati inapendekeza kuwa ushuru wa mazao (crop cess) utozwe kwa kiwango sawa kwa mazao ya biashara na chakula, Aidha, Kamati inapendekeza kiwango kiwe asilimia 3. (Kwa marekebisho ya sasa ni kiwango cha asilimia 3 kwa mazao ya biashara na asilimia2 kwa mazao ya chakula).

#### 4.7 Sheria ya Madini, Sura 123

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza na kukubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwa kifungu cha 18, 19, 90A, 112 ambayo kimsingi yanafanya marekebisho ya kiuandishi, kuweka viwango vya tozo pamoja na kuwezesha uandaaji wa kanuni

na taratibu za ukaguzi wa madini kabla ya kusafirishwa. Hata hivyo, kwa upande wa *Clearance fee* ya kiwango cha asilimia 1 ya thamani ya mziggo, Kamati inapendekeza kodi hii iongezewe kwenye mrabaha na hivyo kuongezeka kutoka asilimia 4 hadi 5 ya mrabaha.

#### **4.8      Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuondoa sharti la kulipa ada ya usalama mahali pa kazi kwa wamiliki wa shule binafsi. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama ya uendeshaji wa shule husika.

#### **4.9      Sheria ya Bandari, Sura 166.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa shughuli za kupakua, kuhifadhi na kusafirisha mizigo bandarini ni jukumu la Bandari. Kamati haina pingamizi na hatua ya Serikali kuleta kifungu kipyaa kidogo cha 67 cha sheria ya Bandari ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa bandari (*wharfage*) na kuweka akaunti itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Kamati inashauri kuwa fedha zitakazokusanywa na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) zirudishwe kama zilivyokusanywa kwa Mamlaka ya Bandari ili iweze kutekeleza majukumu yake.

#### **4.10     Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta marekebisho ya kifungu cha 6 cha Sheria hii ili kuweka mifumo wa kieletroniki (*Government e-payment Gateway System*) wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Taasisi za Serikali. Hatua hii itaongeza ukusanyaji wa mapato pamoja na uthibiti wa fedha za umma.

#### **4.11     Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Kumi na mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria

ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, Sura ya 399. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 16 cha sheria hii ili kuwawezesha maafisa wa Mamlaka ya Mapato kuiwakilisha Mamlaka kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hatua hii itasaidia kupunguza mlolongo wa mashauri ya kimahakama yanayowasilishwa na wadau wa kodi kutoka sehemu mbalimbali.

#### **4.12 Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii inakusudiwa kufanyiwa marekebisho ya kiuandishi katika vifungu 8(1), 22A, 47(1), 52, 81(4) na 95 ili kuleta maana iliyokusudiwa. Pamoja na marekebisho haya Kamati inashauri kuwa:-

. . . Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wasio rasmi na wanaofanya biashara kwa kuwapatia vitambulisho. Aidha, Serikali imewatambua pia watoa huduma ya chakula (caterers), washereheshaji (Masters of Ceremony) na wengine ili kuongeza wigo wa kodi.

. . . Katika kifungu cha 53 cha sheria hii Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kifungu hiki kisifanyiwe marekebisho na hivyo kuendelea kuwa kama awali ambapo wadau wa kodi wana uhuru wa kupeleka mashauri yao katika Bodi ya Rufaa za Kodi Tanzania.

. . . Kamati inakubaliana na marekebisho ya kifungu cha 75, 76 na 78 vinavyohusu utaratibu wa ukokotoaji wa riba.

#### **4.13 Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289**

**Mheshimiwa spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya kiuandishi ya sheria hii ili kuanza kutoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote katika Majiji, Manispaa na Miji kwa viwango vitakavyopangwa na

Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati inapongeza hatua hii, hata hivyo inatoa angalizo kuwa viwango vitakavyopangwa vizingatie uhalisia wa hali ya nyumba husika pamoja na matumizi yake. Aidha, zoezi zima la ukusanyaji lifanywe katika njia shirikishi kati ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kama ilivyokuwa awali ili kutoa fursa ya kutambua maeneo husika pamoja na kuondoa usumbufu kwa wenyewe majengo.

#### **4.14 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwa kifungu cha 59 cha sheria husika kwa kuongeza muda wa kuhifadhi bidhaa/mizigo kutoka nje inayosafirishwa kwenda nje kupitia bandari zilizopo (*ancillary transport services*) kutoka siku 7 hadi 30. Hatua hii itapunguza gharama ya usafirishaji na hivyo kukuza ushindani katika bandari zetu na kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubalia na marekebisho ya kifungu cha 66 na 74 ili kutoa fursa ya kulipa kodi nje ya muda unaotakiwa na hivyo kukuza utii wa hiari katika kulipa kodi pamoja na kutoa kipindi kirefu cha ulipaji wa madeni sugu. Hatua hii itasaidia kuongeza *compliance* katika ulipaji kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya sehemu ya **Kwanza ya Jedwali** ili kusamehe kodi inayotozwa kwenye vyakula vya mifugo na mayai pamoja mashine za kutotoresha vifaranga. Aidha, **sehemu ya Pili ya Jedwali** inatoa fursa ya msamaha wa kodi kwenye bidhaa za mitaji hususani kwenye uingizaji wa mashine na mitambo ya uzalishaji wa mafuta ya kula yatokanayo na mimea, nguo, madawa, ngozi kwa lengo la kukuza viwanda na kuvutia uwekezaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta mapendekezo haya ambayo kimsingi yanalenga kukuza uchumi wa viwanda.

**4.15 Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura ya  
82**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya kumi na sita ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mafunzo ya Ufundı Stadi, Sura 82 kwa lengo la kusamehe tozo ya Elimu ya Ufundı Stadi kwa mashule na vyuo binafsi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusikiliza kilio cha wamiliki wa shule binafsi pamoja na vyuo. Hatua hii itawasaidia kupunguza gharama ya uendeshaji wa taasisi hizo. Kamati inasisitiza Serikali kuangalia na tozo nyingine zilizobaki ili kuendelea kupunguza mzigo wa gharama za uendeshaji kwa wamiliki wa shule.

**4.16. Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango wakati akihitimisha hoja wa waheshimiwa wabunge waliochangia hotuba ya Bajeti ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango wakati akihitimisha hoja za Waheshimiwa wabunge waliojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18. Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Serikali kwa kukubali kufanyia kazi baadhi ya hoja za msingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusiana na Muswada huu. Hivyo Kamati inapenda kutoa pongezi kwa hatua zifuatizo:-

- i) Kutokutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye magari ya kubeba wagonjwa (ambulance);
- ii) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye ada na vibali vya uwindaji vitolewavyo na Serikali;
- iii) Kuondoa tozo ya kuendeleza Mafunzo ya Ufundı (SDL) na Ada ya Zimamoto kwa wamiliki wa shule binafsi
- v) Kuondoa tozo ya *Railway Development Levy* (RDL) kwa upande wa mafuta ya ndege JET-A1 ili kupunguza

gharama ya mafuta hayo hapa nchini na hivyo kuweza kukuza sekta ya usafiri wa anga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haina pingamizi na hatua iliyochukua Serikali ya kuondoa ada ya tathmini ya mazingira kwa wawekezaji wa viwanda. Hata hivyo, Kamati inashauri suala hili liangaliwe upya na Serikali ili itoze kodi hii kwenye viwanda na miradi mikubwa kwa kuzingatia viwango itakayoona vinafaa. Hatua hii itatoa fursa ya kufanya tathmini ya mazingira na hivyo kulinda mazingira yetu.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa maoni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa hii, naomba kuwasilisha maoni ya jumla ambayo Serikali inatakiwa kuyafanya kazi:-

- a) Kupunguza Ushuru wa bidhaa (*Excise Duty*) wa asilimia 17 kwenye '*Electronic Communication Services*' hadi kufikia 14; Kwa sasa nchi za jirani mfano Kenya inatoza asilimia 10, Uganda inatoza asilimia 12, Burundi inatoza asilimia 0 na Rwanda inatoza asilimia 8.
- b) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kibenki na badala yake ushuru wa bidhaa uongezeke kwenye huduma za kibenki;
- c) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa za nguo zinazozalishwa kwa kutumia pamba ya ndani;

## 6.0 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru, Mhe. Dkt Philip I. Mpango, Mb Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Dkt Ashatu K. Kijaji, Mb Naibu Wazirina Mheshimiwa George M. Masaju, Mwanasheria Mkuu

wa Serikali kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa Muswada huu kwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati, pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

- 1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
- 2) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - M/Mwenyekiti
- 3) Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
- 4) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
- 5) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
- 6) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
- 7) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
- 8) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
- 9) Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
- 10) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
- 11) Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
- 12) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
- 13) Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
- 14) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
- 15) Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
- 16) Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mb
- 17) Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
- 18) Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
- 19) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 20) Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
- 21) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
- 22) Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb
- 23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 24) Mhe. Mussa A. Zungu, Mb
- 25) Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb

- 26) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
- 27) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
- 28) Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Dr. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Idara ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Lina Kitosi Mkurugenzi; Ndugu Michael Kadebe Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uchambuzi wa Bajeti; Ndugu Mathew Kileo Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Vyanzo vipyta vya Mapato; na Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Godwin Godfrey, Maombi Kakozi na Lilian Masabala kwa utaalamu wao wa uchambuzi na kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu.

Hawa A. Ghasia, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**  
22/06/2017

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa tutamsikiliza Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango.

**MHE. DAVID E. SILINDE- (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017.

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni hayo, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani na kukemea kwa nguvu zote tabia mbaya ya ubaguzi wa kisiasa dhidi ya Wabunge wa Vyama vya Upinzani iliyoanza kuzuka ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya Wabunge kuomba mwongozo wa Spika wakilenga kuishawishi Serikali isipeleke mgao wa fedha zilizotengwa katika bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Majimbo ya Wabunge wa Upinzani kwa sababu Kambi ya Upinzani ilipiga kura ya 'Hapana' wakati wa kupitisha bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kwamba, Katiba ya nchi yetu inasema nchi yetu ni ya kidemokrasia na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Katika misingi ya demokrasia, watu wana uhuru wa kuchagua kwa maana ya kukubali au kukataa. Hivyo, kuwaadhibu wananchi kwa kuwanyima fedha za miradi ya maendeleo ambazo Serikali hii imezikusanya kutoka kwao kwa sababu tu hawakuchagua chama fulani katika uchaguzi, ni dhambi kubwa ambayo ni Mwenyezi Mungu peke yake anaweza kusamehe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli kama hizi za ubaguzi wa wazi kutokana na itikadi za kisiasa, zinaashiria kwamba tumevimbiwa na amani na utulivu katika nchi yetu, tunu ambazo zimetupatia sifa kubwa duniani kama Taifa. Leo tumeanza kubaguana kwa tofauti zetu za kisiasa, lakini kesho tutaanza kubaguana kwa makabila yetu na keshokutwa tataanza kubaguana kwa dini zetu na hatimaye tutaingia kwenye machafuko makubwa katika historia ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili ni chombo kinachoaminiwa sana na wananchi na Wabunge wanaaminiwa na wanaleshimiwa sana na wananchi, kwa sababu hiyo, Bunge linapotoa kauli au Wabunge wanapotoa kauli huwa wananchi wanaamini na kuifanyia kazi. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Bunge litoe kauli

ya kukanusha masuala yote yaliyojadiliwa Bungeni yenye mrengo wa ubaguzi wa kisiasa kwamba hayakuwa rasmi na kwa maana hiyo yafutwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge ili wananchi wasije wakayachukulia kwamba ni jambo rasmi na kuanza kulitekeleza kwa kusababisha machafuko katika nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa Mnadhimu wa Serikali aliomba mwongozo akitaka kutoa ushawishi kwamba Wabunge wa Upinzani wasiulize maswali kuhusu utekelezaji wa bajeti katika Majimbo yao kwa kuwa walipiga kura ya 'Hapana', naye pia awaombe radhi Watanzania kwa kuwa Watanzania ndiyo walioamua kuchagua Wabunge wa Upinzani ili waisimamie Serikali na haki hiyo wanayo Kikatiba. Zaidi sana Watanzania hao hao waliochagua Upinzani ndiyo hao hao wanaolipa kodi kwa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Fedha uliowasilishwa na Serikali kwa ajili ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Kama ambavyo tulisema kuwa Serikali imeleta bajeti ya ajabu ambayo hajjawahi kutokea katika historia ya Tanzania, maajabu yaleyale yameendelea kujitokeza katika Muswada wa Fedha wa mwaka 2017. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeleta Miswada miwili ya Fedha jambo ambalo ni la ajabu na halijawahi kutokea. Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Fedha Na.3 wa 2017 wa tarehe 2 Juni, 2017 na Muswada wa pili ni Muswada wa Fedha Na.1 wa 2017 wa tarehe 20 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na Muswada wa kwanza wa tarehe 2 Juni, 2017 ambapo ulisomwa kwa Mara ya Kwanza hapa Bungeni tarehe 14 Juni, 2017 na kupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili kufanyiwa uchambuzi, Muswada wa pili wa tarehe 20 Juni, 2017 umeletwa jana tarehe 21 Juni, 2017 ukiwa na marekebisho ya Sheria mpya

sita ambazo hazikuwemo kwenye Muswada wa awali jambo ambalo halikutoa nafasi kwa Kamati na wadau kupitia sheria hizi mpya kabla hazijaletwa Bungeni kama inavyoelezwa katika Kanuni ya 84(3) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ingekuwa inazingatia Kanuni ilitakiwa kuleta sheria hizo mpya za kufanyia marekebisho katika Muswada kwa kufuata taratibu za Kikanuni kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 87(1) ambayo inaelekeza kuwa Muswada unatakiwa kwanza usomwe Bungeni kwa Mara ya Pili na hapo ndipo Serikali inaweza kuleta jambo jipya. Kilichofanya na Serikali ni kuwasilisha Muswada mpya wenye namba mpya, tarehe mpya ya kuchwapwa kwenye Gazeti la Serikali na pia amba haujasomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni. Kanuni 87(1) inasema, nakunukuu:-

*"Endapo Muswada uliokwishakusomwa mara ya Pili na hakuwa na mabadiliko, lakini kuna jambo au suala jipya limetokea linahitaji kuzingatiwa, Mtoa hoja anaweza kumwomba Spika wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa kwenye Kamati ya Bunge Zima kwamba, Muswada huo urejeshwe tena kwenye Kamati inayohusika".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata tabusana kuelewa maana ya udharura huu tena kwa masuala nyeti namna hii yanayohusu fedha za umma. Inatia shaka kwamba pengine kuna jambo linalofichwa na njia pekee ya kulificha jambo hilo ni kuwashtukiza Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta mapendekezo mapya katika dakika za mwisho kinyume na Kanuni zetu za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulioletwa leo kwanza haukuuata utaratibu wa Kibunge kwa maana ya kusomwa kwa Mara ya Kwanza na kupelekwa kwenye Kamati kwa ajili ya kupata maoni ya Kamati ya Bajeti lakini pili haukuletwa kwa Hati ya Dharura kama ilivyo desturi kwa Miswada inayohitajika kupitishwa kwa dharura. Aidha, Serikali haijaundoa Muswada wa awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, Muswada huu haujasomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Bunge ambayo inasema:-

*"Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa kwenye Gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha ya Shughuli ili Kusomwa kwa Mara ya Kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo".*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Muswada kusomwa kwa Mara ya Kwanza, Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge inaelekeza kwamba:-

*"Spika atapeleka Muswada huo kwenye Kamati inayohusika na Kamati hiyo itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo".*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa Kamati inayohusika imepelekewa Muswada huo lakini Kanuni ya 84(2) inaielekeza Kamati iliyopelekewa Muswada huo, kutoa matangazo au barua za mialiko kwa wadau ili watoe maoni yao mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kuchambua Muswada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mashaka kama Muswada huo ulioletwa leo umekidhi masharti ya Kanuni ya 84(2). Kutokana na ukiukwaji wa Kanuni uliofanywa katika uwasilishwaji wa Muswada huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba Muswada huu umeletwa kienyeji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kodi na ustawi wa biashara nchini. Mfumo wa kodi wa nchi yetu kwa mujibu wa taarifa ya *Tanzania Economic Updates, issue no.7* ya July 2015, ni mfumo mbaya sana ambao kwa upande mmoja kodi zake ziko juu sana na hivyo kuwakatisha tamaa walipa kodi au kwa maneno mengine unasababisha wafanyabiashara watafute mbinu za kukwepa kodi. Kwa

upande mwininge, mfumo wetu wa kodi una udhaifu katika makusanyo pale ambapo kodi stahiki inatakiwa kukusanya. Sasa hivi ndijo hali imekuwa mbaya baada ya kuundwa kwa kikosi kazi cha kukusanya kodi na hivyo *ku-by pass* mfumo wetu wa *TRA* jambo ambalo linatengeneza mazingira wezeshi kwa watu kutoa rushwa. Hiki ni kikosi hatari sana katika mfumo mzima wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na upungufu huo, pia mfumo wetu wa kodi hauna uhalisia wa kodi inayotakiwa kulipwa pamoja na hali halisi ya uchumi wa Tanzania ambayo ni nchi ya uchumi wa chini yaani *low income economy*. Taarifa hiyo hiyo inaonesha kuwa, kwa utafiti wa *Afrobarometer* ni kwamba asilimia 72 ya Watanzania wa kawaida wanashindwa kuelewa ni aina gani ya kodi na tozo wanatakiwa kulipa kwani makato wanayokatwa wanashindwa kufahamu yanahuisha mambo gani hasa kutokana na wingi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili ni hatari sana kwa mlipa kodi kwani mlipa kodi akishaanza kuona kwamba hatendewi haki katika mfumo mzima wa kulipa kodi kwa kulinganisha na aina ya biashara zake basi inamlazimu mhusika huyo aanze kutafuta njia mbadala ya kuokoa biashara yake isifilisike kwa kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya '*Doing Business*' ya mwaka 2015, inaonesha kuwa kati ya nchi 189, Tanzania inashika namba ya 148 katika vigezo ya urahisi wa ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wa Tanzania wanakabiliwa na wastani wa kodi 49 tofauti tofauti kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa kwa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo kiwango chake cha kodi 38 kwa mwaka. Aidha, taarifa hiyo inaonesha walipa kodi wanatumia muda wa saa 181 kila mwaka katika mchakato wa ulipaji wa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili bado ni tatizo katika kuongeza mapato yatokanayo na kodi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wataalam wengine wanatoa hoja kwamba, *the exclusive focus on administrative means does not mean of increasing the collection of taxes*. Msemo huu tunaweza kuuona kuwa ni kweli kwa maana kwamba wingi wa kodi na viwango vya kodi vilivyopo ndio vinapelekea watu wengi kukwepa au biashara kufungwa hili ni tatizo pia. Hivyo kuweka mifumo mizuri ya teknolojia ya mawasiliano (*IT*) katika ukusanyaji wa mapato bado haitoweza kuongeza mapato ya kodi kutokana na wingi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugatuaji wa masuala ya kodi kama ambavyo sheria zetu zilizopo zinavyosema ilikuwa ni mfumo wa kuhamisha ulipaji wa kodi na tozo mbalimbali kwa wananchi, kwani kufanya hivyo wananchi wanakuwa na imani kuwa kodi wanazolipa zinawaleta maendeleo moja kwa moja katika maeneo husika. Kitendo cha Serikali kuzinyang'anya Halmashauri baadhi ya vyanzo vya mapato kwa muktadha huo ni kuwaondolea imani Watanzania katika ulipaji wa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu za makosa ya barabarani kama moja ya chanzo cha mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepochea malalamiko kutoka kwa wananchi hasa wamiliki binafsi wa magari na madereva wanaoendesha magari ya usafiri wa umma na biashara zingine kuhusu utozaji wa faini zinazotokana na adhabu za makosa barabarani unaofanywa na Askari wa Usalama Barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kumekuwepo na tabia ya Jeshi la Polisi kutoa taarifa kwa umma kuhusu kiasi ambacho kimekusanywa kwa muda fulani kutokana na adhabu zinazotokana na makosa ya barabarani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa adhabu ya kulipa faini inatakiwa kuwa funzo kwa mkosaji na si chanzo cha mapato ya Serikali. Kwa sasa imefikia hatua watu binafsi wanaona karaha kumiliki magari na wengine wamefikia hatua ya kuacha kutumia magari kutokana na kero za Askari wa Usalama Barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifa zisizo rasmi kuwa imefikia hatua Askari wa Usalama Barabarani kupangisha idadi ya makosa ambayo wanatakiwa kuwasilisha faini kila siku ambapo ikitokea Askari hajafikia lengo basi haruhusiwi kwenda kushiriki mafunzo au kupanda cheo. Suala hili si la kupuuza hata kidogo, kwa sababu tunajenga Taifa la kubambikizia wananchi makosa ya barabarani kwa ajili ya kukusanya mapato na pia kushindwa kutoa funzo kwa madereva kwa makosa ambayo yanatosha tu Askari kutoa elimu kwa dereva kwa kosa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya kupunguza ajali za barabarani, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa jambo hili ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu malalamiko haya au Waziri wa Fedha alete marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ili Bunge na wananchi wajue kuwa Serikali imeweeka faini za makosa ya barabarani kama moja ya chanzo cha mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Muswada wa Fedha wa mwaka 2017. Baada ya kutoa utangulizi huo kuhusiana na mfumo wetu wa kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani imepitia Muswada huo ulioletwa wa Fedha kwa mwaka 2017 kuona ni kwa kiwango gani utaathiri maisha ya walipa kodi wa nchi hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu, Sura ya 197. Kifungu cha nne (4) cha Muswada kinachofanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 32 cha Sheria Mama kwa kuongeza vifungu vipyta tatu (3) na nne (4). Kifungu cha tatu (3) kinasomeka kama ifuatavyo:-

*"All government and public authorities shall open and deposit all their moneys with the Bank".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa na maoni tofauti juu ya uamuzi wa Serikali wa kuhamisha fedha zote za taasisi za Serikali kutoka kwenye mabenki ya biashara na kuhamishia Benki Kuu. Kwa uamuzi

huu, Benki Kuu itakuwa inashindana na mabenki ya biashara ilhali Benki Kuu inatakiwa kufanya kazi ya udhibiti tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kurejea kauli zilizotolewa na Maprofesa wawili wa uchumi na kunukuliwa katika Gazeti la Mwananchi la tarehe 13 Februari, 2016 kwamba, Serikali iangalie wenzetu wa Botswana na Namibia walifanya nini katika hili na kama Serikali inataki kuingia katika biashara basi ifungue benki yake ya kibiashara kama lilivyokuwa lengo la kuanzishwa kwa Benki ya *NBC* na akaunti za taasisi zote za Serikali zihamishiwe huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yalisemwa na Profesa Anderson. Wakati huohuo Profesa Gabagambi alihoji kuwa inakuwaje Serikali inahamisha fedha zake wakati huo huo hurudi tena Benki kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia hati fungani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja hizo, ni mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, kifungu hiki cha Muswada kinachopendekeza na Serikali kisikubaliwe na Bunge lako Tukufu. Kwa utaratibu huu unaopendekeza na Serikali dhana ya ushindani wa kibiashara hautakuwa na maana. Serikali iweke mfumo mzuri wa kudhibiti mashirika yanayotumia vibaya fedha zake zinapowekwa kwenye akaunti za benki za biashara na siyo kuzilundika fedha zote *BoT* ambazo hawafanyi biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147. Sehemu ya Pili ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 ya Sheria za Tanzania kwa kuweka viwango maalum (*specific rates*) vya Ushuru wa Bidhaa vinavyotumika kwenye baadhi ya bidhaa. Inaelezwa kwamba viwango hivyo vinavyorekebishwa ni kwa mujibu wa sheria hiyo kwa kiwango cha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo yamepelekea kupandishwa kodi kwenye bidhaa ambazo uzalishaji wake hutumia malighafi inayozalishwa ndani ya

nchi kama vile shayiri na tumbaku jambo ambalo ni dhahiri litapunguza bei za mazao hayo na hivyo kupunguza kipato cha wakulima wa mazao hayo. Kwa mfano, kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, Ushuru wa Bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini umepanda kutoka Sh.429/= kwa lita hadi Sh.450/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.21/= . Hali kadhalika, Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 umepanda kutoka Sh.11,854/= hadi Sh.12,447/= kwa kila sigara 1,000 ikiwa ni ongezeko la Sh.493/= kwa kila sigara 1,000. Aidha kwa sigara zenye vichungi, ushuru umepanda kutoka Sh.28,024/= hadi Sh.29,425/= kwa kila sigara 1,000, ikiwa ni ongezeko la Sh.1,401 kwa kila sigara 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa shayiri na tumbaku ni kama vile wamekuwa na bahati mbaya miaka yote. Nasema hivi kwa sababu kila mwaka kodi kwenye bia na sigara lazima ipande. Kwa kufanya hivyo, wamiliki wa viwanda vya bia na sigara ili wamudu kodi hizo na kuweza kupata faida ni lazima wawaminye wakulima wa mazao hayo kwa kutoa bei ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kupandisha kodi kwenye bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia malighafi inayozalishwa hapa nchini kwani kwa kufanya hivyo ni kuwadidimiza wazalishaji wa malighafi hiyo na ni kuua ari ya mapinduzi ya viwanda hapa nchini kwani ili viwanda viwepo na vizalishe ni lazima kuwe na sekta ya kilimo iliyoboreshwa, ambapo Wakulima wana motisha ya kuzalisha kutokana na bei nzuri ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza pia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari na badala yake kupandisha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa kiasi cha Sh.40/= kwa kila lita moja ili kufidia upungufu wa mapato ambao ungetokana na

kufutwa kwa ada hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema wakati wa uwasilishwaji wa Bajeti Mbadala kwamba hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania inawalipisha Watanzania maskini wasio na uwezo wa kumiliki magari kodi ya ada ya mwaka ya leseni za magari. Kuihamishia kodi hiyo kwenye Ushuru wa Bidhaa za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ambapo athari zake ni kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulieleza kwamba, kupanda kwa bei ya mafuta kutasababisha kupanda kwa nauli katika sekta ya usafirishaji jambo litakalosababisha kupanda kwa bei za vyakula; kupanda kwa bei za kusaga na kukoboa nafaka kwa kutumia mashine zinazotumia petroli au dizeli kwa wananchi waishio vijijini; kupanda bei kwa pembejeo za kilimo; kushindwa kupata nishati ya mwanga kwa wananchi walio vijijini kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa. Kwa maneno mengine bajeti hii imelenga kuwabebesha maskini mzigo wa kodi kwa matumizi ya anasa ya watu wa tabaka la kati na juu wenye uwezo mkubwa kifedha kwa kuweza kumiliki magari na vitu vingine vya thamani kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo yote tulibainisha kwamba, hakuna chombo chochote cha moto cha usafiri wa barabarani kinachotumia mafuta ya taa. Iweje mwananchi wa kawaida asiyemiliki gari atozwe ushuru huo kwenye mafuta ya taa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu, marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kwa kukifanyia marekebisho Kifungu cha 31A cha sheria hiyo ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kukusanya ushuru wa mabango ya matangazo nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono uamuzi wa Serikali Kuu kukusanya

ushuru wa mabango nchi nzima kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Sababu kubwa ya kupinga uamuzi huo ni kutokana na ukweli kwamba ushuru wa mabango ni chanzo cha pili cha mapato katika Halmashauri zetu za Miji, Majiji na Manispaa, chanzo cha kwanza kikiwa ni kodi ya majengo (*property tax*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzinyang'anya Halmashauri zetu vyanzo vyake vya mapato na kuvihamishia Serikali Kuu kunakwenda kinyume kabisa na dhana ya ugatuaji madaraka katika Serikali za Mitaa (*D by D*) ambayo kwa kipindi kirefu Serikali hii hii ya CCM imekuwa ikipigia upatu. Aidha, kuzinyang'anya Serikali za Mitaa vyanzo vyake vya mapato kutazidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwa sasa zitashindwa kujiendesha na hatimaye zitakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachilia mbali mapato yatokanayo na ushuru wa mabango ambayo yamechukuliwa na Serikali Kuu, hata hivyo, Serikali Kuu kupitia Waziri wa Fedha, imefuta ushuru wa huduma (*service levy*) kwenye nyumba za kulala wageni; imefuta ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mfano vibali vya machinjio, imefuta ada ya vibali vya kusafirishia mifugo na ada ya vibali vya kuanzisha maduka ya dawa; imefuta ada ya makanyagio minadani na kadhalika ambazo zilikuwa ni vyanzo vya mapato kwa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi kufutwa kwa ada hizo ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi ila haioni mantiki ya kufuta tozo hizo ambazo zilikuwa zinaziwezesha Halmashauri kimapato na hapo hapo kuvitaifisha vyanzo vingine vya mapato kama vile ushuru wa mabango na kodi ya majengo na kuziacha Serikali za Mitaa zikiwa hazina chanzo chochote cha maana cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Serikali Kuu ikaelewa kwamba Serikali za Mitaa ni zao la Katiba ya nchi yetu kwa mujibu wa lbara ya 143 na 145 ya Katiba na kwamba uwepo wa Serikali za Mitaa si hisani ya Serikali Kuu. Kwa sababu hiyo, kufanya jambo lolote linalolenga kuzipuuza au

kuzidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zipo Kikatiba ni kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21 cha Muswada kinaongeza Kifungu kidogo cha (c) kinachofanya marekebisho Kifungu cha 37 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuwatambua wafanyabiashara wadogo, wanaofanya biashara katika maeneo ambayo siyo rasmi kama vile mama lishe, wauza mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo wadogo kama mbogamboga, ndizi na kadhalika kwa kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazofanya. Ukitazama lengo la marekebisho haya yanayopendekezwa na Serikali, unaweza kufikiri kwamba Serikali ina nia njema na hawa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba wafanyabiashara hawa wamekuwa ndiyo wahanga wakubwa wa uonevu mkubwa unaofanywa na Serikali hii dhidi yao. Hawa ndiyo wamekuwa wakifukuzwa kama digidigi katika kila kona ya mji na kupigwa marufuku kuendesha shughuli zao za kujipatia kipato kwa maana kwamba wanachafua mandhari ya miji. Wamekuwa wakitendewa vibaya kana kwamba wao siyo raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu Serikali inaotaka kuanzisha na kuwatambua wafanyabiashara wadogo ni kwa lengo la kuwatoza kodi na ushuru tu na si kwa lengo la kuwasaidia kama ambavyo Serikali inavyotaka kuuaminisha umma. Kama kweli Serikali ilikuwa na nia hiyo, kwa nini haikufanya hivyo kwa miaka 50 iliyopita tangu imekuwepo madarakani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Serikali hii kuwageuka wafanyabiashara wadogo ambao ni wanyonge na maskini kwa lengo la kuwatoza kodi wakati imeshindwa kukusanya mapato makubwa yanayotokana na sekta ya madini. Shilingi trilioni 108 ambazo Serikali imedai imepoteza

katika sakata la Makinikia, kwa nini isijikite sasa katika kuzipata hizo kwanza kabla haijaanza kufikiria kodi kwenye vitumbua na maandazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishangaa sana Serikali kufikiria vyazo dhaifu nya mapato na kuviacha vile vikubwa ambapo Serikali itavisimamia vizuri, kusingekuwa na haja ya kuwatoza mama lishe au wauza mbogamboga ushuru wowote. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektoriniki, Sura ya 306. Dhana nzima ya kifungu cha sheria kinachofanyiwa marekebisho wakati Bunge linatunga sheria hiyo ilikuwa ni kuwapa umiliki Watanzania katika makampuni yanayomilikiwa na wageni. Kwa dhana hiyo iliyokuwepo ni dhahiri kwamba Kifungu cha saba (7) cha Muswada kinakinzana na dhana mama ya uwepo wa kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inawaomba Waheshimiwa Wabunge wajjulize ni kwa nini hasa kifungu hiki cha Muswada kinafuta tafsiri ya maneno "*local shareholder*". Bila kufahamu chimbuko lake ni dhahiri sheria hizi tunazozitunga wenzetu watakaokuja watatuona kama vile hatukustahili kuwawakilisha wananchi katika chombo hiki kitukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba kama mazingira ya ufanyaji wa biashara ni mazuri hakuna sababu hata moja ni kwa nini hisa za makampuni yanayojisajili katika soko la hisa zisinunulike. Kambi Rasmi ya Upinzani mbali ya sababu hiyo ya kushindwa kununulika kwa hisa na pia pale ambapo wanunuizi watarajiwa wanakuwa na wasiwasi kwamba mahesabu ya utendaji wa kampuni husika yana dalili ya udanganyifu. Kama vigezo hivyo vikienda sambamba, ni dhahiri hata milango ikifunguliwa kwa raia wasio Watanzania ununuizi wa asilimia 25 hauwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia mifumo yake ya ndani

ya udhibiti ni kwa kiwango gani ni *conducive* kwa wafanyabiashara nchini kufanya biashara. Hilo ndilo litakuwa suluhihisho la tatizo hili na siyo kuongeza wigo kwa wageni kwani kufanya hivyo kunaondoa dhana nzima ya uwepo wa kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho Kifungu ya Sheria ya Madini. Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 ya Sheria za Tanzania, kwa kuingiza kitu kinachoitwa ushuru wa ukaguzi (*inspection fee*). Ili kuelewa maana ya mapendekezo haya, ni muhimu tufahamu aina na kiwango cha kodi, ushuru, tozo na malipo mengine ambayo makampuni ya madini yanawajibika kulipa kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini kama ilivyo sasa, kodi au ushuru au tozo muhimu kuliko zote ni mrabaha. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 87(1) cha sheria hii, mwenye leseni ya kuchimba na/au kuuza madini anawajibika kulipa mrabaha kwa bei ya mauzo (*gross value*). Viwango vya mrabaha kwa mujibu wa kifungu hicho ni 1% kwa mawe ya thamani (*gemson*); 3% kwa ajili ya madini ya viwandani (*industrial minerals*), chumvi na madini ya ujenzi kama mchanga, kokoto, mawe na kadhalika. Aidha, kwenye leseni ya kuchimba madini ya vyuma kama vile dhahabu, shaba, fedha na madini ya kundi la *platinum* anawajibika kulipa mrabaha wa 4% kwa mawe ya vito na almasi pamoja na madini ya urani (*uranium*) kwa kiwango cha mrabaha ni 5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la sheria za kusimamia rasilimali zetu kurekebishiwa ikiwemo Sheria za Madini limekuwa likipigiwa kelele na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mingi. Serikali baada ya Taarifa ya Kamati ya Pili ya Makinikia imeahidi kuwa Sheria na Mikataba yote ya Madini italetwa Bungeni ili iweze kujadiliwa na kufanyiwa marekebisheso.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji kama marekebisheso haya

yanayopendekezwa katika Muswada huu wa *Finance Bill* ndiyo kero kubwa iliyokuwa inapigiwa kelele na Bunge na Serikali kwa muda huu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha tano (5), Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438, naomba iingie kama ilivyo katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho katika Sheria ya Bandari Sura 166, naomba na yenye kama ilivyo. Hata hivyo, niseme tu kidogo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona pendekezo hili la haja la kuondoa hizi tozo za bandari ni kifo cha mfa maji haishi kutapatapa. Kwa maana Serikali inakataa kusema ukweli kuwa mapato ya kodi yameshuka vibaya sana, kinachofuata ni Serikali kukusanya tozo na vyanzo vingine vinavyopatikana ili kuonekana kuwa mapato yameongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Kodi za Majengo ya Mamlaka za Miji, kipengele H, naomba na chenyewe kiingie kama kilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mjadala wa bajeti kwa asilimia kubwa ulijikita katika Sheria ya Usalama wa Barabarani, Sura 168, kwa bahati mbaya sana hadi tunatayarisha maoni haya pamoja na Muswada mpya wa Fedha ulioletwa hakuna marekebisho ya sheria hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata ufanuzi ni kwa namna gani ada ya mwaka ya leseni ya magari (*Annual Motor Vehicle Licence fee*) imefutwa. Vinginevyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaweza kuamini kwamba Serikali imewahadaa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kuwa ili Serikali iweze kutekeleza wajibu wake kwa jamii ni lazima kodi zilipwe, jambo hili ni lazima lifanyike. Katika kufanya hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa litakuwa ni jambo la muhimu kuhakikisha kuwa

viwango vya kodi vinakuwa rafiki na kodi zinakuwa chache kiasi kwamba hakutakuwa na mlipa kodi kujishauri ni jinsi gani atalipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Muswada wa Fedha ambao ndio Sheria ya Fedha ni ridhaa ambayo Serikali inaipata kutoka kwa wananchi kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa wako tayari kulipa kodi kama ambavyo inapitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, kama Waheshimiwa Wabunge wanatoa ridhaa yao kuwa tozo na ushuru mbalimbali ziongezwe, ambazo kwa muktadha wake zitaongeza gharama kwa malighafi zinazotoka kwa wakulima, maana yake ni kudidimiza kilimo ambacho kinatoa ajira kwa Watanzania zaldi ya asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema kuwa, “*boys in the backroom*” ukiwa na maana kuwa kuna kundi la watu wanaofanya maamuzi hawaonekani lakini maamuzi yao yanakuwa na athari kubwa kwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imetumia usemi huu kutokana na ukweli, sisi kama Waheshimiwa Wabunge ndio tunaotunga sheria kwa mujibu wa sheria, Serikali kazi yake ni kuleta mapendekezo tu. Hata hivyo, kwa kuwa kuna “*boys in the backroom*” Bunge linakuwa ni chombo cha kufuata maelekezo tu. Hii ni hatari sana katika mustakabali wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa sasa ni muda muafaka kwa chombo hiki kikuu cha kutunga sheria kusimamia mamlaka yake ya kikatiba na kisheria. Imebidi kusema haya kwa uchungu mkubwa kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wamelalamika kuhusiana na kuondoa ongezeko la Sh.40/= katika lita moja ya mafuta ya taa lakini Serikali inasema kuwa uwiano kati ya mafuta ya taa na diseli ukiwa mkubwa maana yake

unaruhusu uchakachuaji wa mafuta ya diseli. Kwa kigezo hiki maana yake ni kwamba wananchi wetu waendelee kuumia ili kuwaridhisha wachache. (*Makof*)

*Mheshimiwa Naibu Spika, majibu hayo ya Serikali yanaonesha kuwa bado kuna udhaifu mkubwa kwa upande wa Serikali katika kuzuia udanganyifu unaofanywa na watu wasio na nia njema katika uchumi wa Taifa letu. (Makof)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imepewa mamlaka ya kukusanya kodi kwa Sheria hii ya Fedha tunayopitisha hapa; na kwa kuwa Serikali inapokusanya kodi hiyo haikusanyi kwa wanachama wa CCM pekee, bali inakusanya kwa watu wote wanaostahili kulipa kodi bila kuwabagua kwa itikadizao za kisasa, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwahakikishla wananchi kwamba haitawabagua kwa misingi ya itikadi za kisasa katika kuwapelekea maendeleo kwa kuwa haikuwabagua wakati inakusanya kodi kutoka kwao. (Makof)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba, sisi sote ni Watanzania, tunajenga Taifa moja, Upinzani wetu haujawahi hata siku moja kuwa na maana ya kubomoa nchi. Siku zote tunatoa mawazo yetu kwa lengo la kuisaidia Serikali kufanya vizuri zaidi katika kujengenya nchi. Kama wananchi wakiamua kutupa ridhaa ya kuongoza nchi hii watatupima vilevile kwa viwango gani tunaweza kujengenya nchi hii vizuri zaidi na sio kuibomoa. Wanaoingiza statement za ubaguzi wa kisasa sasa hivi wanapanda mbegu mbaya sana ya kuligawa Taifa na wanapaswa kupingwa na watu wote wenye nia njema ya kudumisha umoja na amani ya nchi yetu. (Makof) [Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha. Hotuba yetu yote kama ilivyo iingie katika Hansard. (*Makof/Vigelegelo*)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB), KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2017 (THE FINANCE ACT, 2017) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Mwaka 2016)*

---

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni hayo, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani na kukemea kwa nguvu zote tabia mbaya ya ubaguzi wa kisiasa dhidi ya wabunge wa vyama vya Upinzani iliyoanza kuzuka ndani ya Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya wabunge kuomba mwongozo wa Spika wakilenga kuishawishi Serikali isipeleke mgawo wa fedha zilizotengwa katika bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika majimbo ya wabunge wa upinzani kwa sababu Kambi ya Upinzani ilipiga kura ya hapana wakati wa kupitisha bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, leleweke kwamba, Katiba ya nchi yetu inasema kwamba nchi yetu ni ya kidemokrasia na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Na katika misingi ya demokrasia; watu wana uhuru wa kuchagua - kwa maana ya kukubali au kukataa. Hivyo, kuwaadhibu wananchi kwa kuwanyima fedha za miradi ya maendeleo ambazo Serikali hii imezikusanya kutoka kwao kwa sababu tu hawakuchagua Chama fulani katika uchaguzi, ni dhambi kubwa ambayo ni Mwenyezi Mungu peke yake anaweza kusamehe.

**Mheshimiwa Spika**, kauli kama hizi za ubaguzi wa wazi kutokana na itikadi za kisiasa, zinaashiria kwamba tumevimbwiwa na amani na utulivu katika nchi yetu – tunu ambazo zimetupatia sifa kubwa duniani kama Taifa. Leo tumeanza kubaguana kwa tofauti zetu za kisiasa, lakini kesho tutaanza kubaguana kwa makabila yetu, na keshokutwa tataanza kubaguana kwa dini zetu na hatimaye tutaingia kwenye machafuko makubwa katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili ni chombo kinachoaminiwa sana na wananchi. Na wabunge wanaaminiwa na wanaleshimiwa sana na wananchi. Kwa sababu hiyo, Bunge linapotoa kauli au wabunge wanapotoa kauli huwa wananchi wanaamini na kufanya kazi. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba; Bunge litoe kauli ya kukanusha masuala yote yaliyojadiliwa Bungeni yenye mrengo wa ubaguzi wa kisiasa kwamba hayakuwa rasmi na kwa maana hiyo yafutwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge ili wananchi wasije wakalichukulia kwamba ni jambo rasmi na kuanza kulitekeleza na kusababisha machafuko katika nchi. Aidha, kwa kuwa Mnadhimu wa Serikali aliomba mwongozo akitaka kutoa ushawishi kwamba wabunge wa upinzani wasiulize maswali kuhusu utekelezaji wa bajeti katika majimbo yao kwa kuwa walipiga kura ya hapana; naye pia awaombe radhi watanzania kwa kuwa watanzania ndio walioamua kuchagua wabunge wa upinzani ili waisimamie Serikali na haki hiyo wanayo kikatiba; na zaidi sana watanzania hao hao waliochagua upinzani ndio hao hao wanaolipa kodi kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Fedha uliowasilishwa na Serikali kwa ajili ya kupitishwa na Bunge kuwa Sheria rasmi ya Fedha kwa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kama ambayo tulisema kuwa Serikali imeleta Bajeti ya ajabu ambayo haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania, maajabu yaleyale yameendelea kujitokeza katika Muswada wa Fedha wa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeleta miswada miwili ya fedha jambo ambalo ni la ajabu na halijawahi kutokea. Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Fedha Namba 3 wa 2017 wa tarehe 2 Juni, 2017, na Muswada wa pili ni Muswada wa Fedha Namba 1 wa 2017 wa tarehe 20 Juni, 2017

**Mheshimiwa Spika**, Tofauti na Muswada wa kwanza, wa tarehe 2 Juni, 2017 ambao ulisomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni tarehe 14 Juni, 2017 na kupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili kufanyiwa uchambuzi; Muswada wa pili wa tarehe 20 Juni, 2017 umeletwa jana tarehe 21 Juni, 2017 ukiwa na marekebisho ya sheria mpya sita ambazo hazikuwemo kwenye muswada wa awali, jambo ambalo halikutoa nafasi kwa Kamati na wadau kuititia sheria hizi mpya kabla hazijaletwa Bungeni kama inavyoiezwa katika Kanuni ya 84 (3) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kama Serikali ingelikuwa inazingatia Kanuni ilitakiwa kuleta Sheria hizo mpya za kufanya marekebisho katika Muswada kwa kufuata taratibu za Kikanuni kama inavyoelekezwa katika kanuni ya 87 (1) ambayo inaelekeza kuwa Muswada unatakiwa kwanza usomwe Bungeni kwa mara ya pili na hapo ndipo Serikali inaweza kuleta jambo jipya. Kiliochhofanywa na Serikali ni kuwasilisha Muswada mpya wenye namba mpya, tarehe mpya ya kuchwapwa kwenye gazeti la Serikali na pia ambao haujasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni.

Kanuni 87(1)hiyo inasema, naomba kunukuu "**Endapo Muswada ulikwishesomwa mara ya pili na hakuwa na mabadiliko, lakini kuna jambo au suala jipya limetokea na linahitaji kuzingatiwa, Mtoa hoja anaweza kumwomba Spika wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa kwenye Kamati ya Bunge zima kwamba, Muswada huo urejeshwe tena kwenye Kamati inayohusika**"

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata tabu sana kuelewa maana ya udharura huu. Dharura

hii tena kwa masuala nyeti namna hii yanayohusu fedha za umma, inatia shaka kwamba pengine kuna jambo linalofichwa na njia pekee ya kulificha jambo hilo ni kuwashtukiza Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta mapendekezo mapya katika dakika za mwisho kinyume na Kanuni zetu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada ulioletwa leo, kwanza haukuftuata utaratibu wa kibunge kwa maana ya kusomwa kwa mara ya kwanza na kupelekwa kwenye Kamati kwa ajili ya kupata maoni ya Kamati ya Bajeti, lakini pili hata haukuletwa kwa hati ya dharura kama ilivyo desturi kwa miswada inayohitajika kupitishwa kwa dharura. Aidha, Serikali haijaoundoa Muswada wa awali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kifupi, muswada huu haujasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Bunge ambayo inasema kwamba *“Muswada wowote wa Sheria ambaa umetangazwa kwenye Gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha ya Shughuli ili kusomwa kwa mara ya kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo”*.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muswada kusomwa kwa mara ya kwanza; Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge inaelekeza kwamba, "Spika atapeleka Muswada huo kwenye Kamati inayohusika na Kamati hiyo itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo. Inawezekana kabisa kwamba Kamati inayohusika imepelekewa Muswada huu; lakini Kanuni ya 84(2) inaelekeza Kamati iliyopelekewa Muswada huo, kutoa matangazo au barua za mialiko kwa wadau ili watoe maoni yao mbele ya kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kuchambua muswada huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mashaka kama Muswada ulioletwa leo umekidhi masharti ya Kanuni ya 84 (2). Kutokana na ukiukwaji wa Kanuni uliofanyika katika uwasilishwaji wa Muswada huu, Kambi

Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba Muswada huu umeletwa kienyeji, na kwa maana hiyo, unakosa sifa za kujadiliwa na kupitishwa na bunge lako tukufu.

## **2. MFUMO WA KODI NA USTAWI WA BIASHARA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa kodi wa nchi yetu kwa mujibu wa taarifa ya “**Tanzania Economic Updates, issue no.7 ya July 2015**” ni mfumo mbaya sana ambao kwa upande mmoja kodi zake ziko juu sana na hivyo kuwakatisha tamaa walipa kodi au kwa maneno mengine unasababisha wafanyabiashara watafute mbinu za kukwepa kodi. Kwa upande mwingine mfumo wetu wa kodi una udhaifu katika makusanyo pale ambapo kodi stahiki inatakiwa kukusanya. Sasa hivi ndio hali imekuwa mbaya baada ya kuundwa kwa kikosi kazi cha kukusanya kodi na hivyo **ku-by pass** mfumo wetu wa TRA, jambo ambalo linatengeneza mazingira wezeshi kwa watu kutoa rushwa. Hiki ni kikosi hatari sana katika mfumo mzima wa kukusanya kodi.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na mapungufu hayo pia mfumo wetu wa kodi hauna uhalisia wa kodi inayotakiwa kulipwa pamoja na hali halisi ya uchumi wa Tanzania ambayo ni nchi ya uchumi wa chini “**low income economy**”. Taarifa hiyo hiyo inaonesha kuwa, kwa utafiti wa Afrobarometer ni kwamba asilimia 72 ya Watanzania wa kawaida wanashindwa kuelewa ni aina gani ya kodi na tozo wanatakiwa kulipa, kwani makato wanayokatwa wanashindwa kufahamu yanahuisha mambo gani hasa, kutokana na wingi wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inalionna jambo hili ni hatari sana kwa mlipa kodi, kwani mlipa kodi akishaanza kuona kwamba hatendewi haki katika mfumo mzima wa kupia kodi kwa kulinganisha na aina ya biashara zake, basi inamlazimu mhusika aanze kutafuta njia mbadala ya kuokoa biashara yake isifilisike kwa kulipa kodi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya 'Doing Business' ya mwaka 2015, inaonesha kuwa kati ya nchi 189 Tanzania inashika namba ya 148 katika vigezo ya urahisi wa ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wa Tanzania wanakabiliwa na wastani wa kodi 49 tofauti tofauti kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa kwa nchi za Afrika- Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo kiwango chake ni kodi 38 kwa mwaka. Aidha taarifa hiyo inaonesha walipa kodi wanatumia muda wa masaa 181 kila mwaka katika mchakato wa ulipaji wa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili bado ni tatizo katika kuongeza mapato yatokanayo na kodi<sup>1</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, kuna wataalam wengine wanatoa hoja kwamba, "*The exclusive focus on administrative means does not mean of increasing the collection of Taxes*". Msemo huo tunaweza kuuona kuwa ni kweli kwa maana kwamba wingi wa kodi na viwango vya kodi vilivyopo ndilo vinapelekea watu wengi kukwepa au biashara kufungwa hilo ni tatizo pia, hivyo kuweka mifumo mizuri ya teknolojia ya mawasiliano (IT) katika ukusanyaji bado haitoweza kuongeza mapato yatokanayo na kodi.

**Mheshimiwa Spika**, ugatuaji wa masuala ya kodi kama ambavyo sheria zetu zilizopo zinavyosema ilikuwa ni mfumo wa kuhamasisha ulipaji wa kodi na tozo mbalimbali kwa wananchi, kwani kufanya hivyo wananchi wanakuwa na imani kuwa kodi wanazolipa zinawaaletea maendeleo moja kwa moja katika maeneo husika. Kitendo cha Serikali kuzinyang'anya halmashauri baadhi ya vyanzo vya mapato kwa muktadha huo ni kuwaondolea imani watanzania katika ulipaji wa kodi.

### 3. ADHABU ZA MAKOSA YA BARABARANI NI CHANZO CHA MAPATO?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea malalamiko kutoka kwa wananchi hasa wamiliki binafsi wa magari na madereva wanaoendesha magari ya

---

<sup>1</sup> The World Bank Group Macroeconomics and Fiscal Management Global Practice Africa Region

usafiri wa umma na biashara zingine kuhusu utozaji wa faini zinazotokana na adhabu za makosa ya barabaranii unaofanywa na askari wa usalama barabaranii.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha kumekuwa na tabia ya Jeshi la Polisi kutoa taarifa kwa umma kuhusu kiasi ambacho kimekusanya kwa muda Fulani kutokana na adhabu zinazotokana na makosa ya barabaranii. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa adhabu ya kulipa faini inatakiwa kuwa funzo kwa mkosaji na si chanzo cha mapato ya serikali. Kwa sasa imefikia hatua watu binafsi wanaona karaha kumiliki magari na wengine wamefikia hatua ya kuacha kutumia magari kutokana na kero za askari wa usalama barabaranii.

**Mheshimiwa Spika**, zipo taarifa zisizo rasmi kuwa imefikia hatua askari wa usalama barabaranii kupangiwa idadi ya makosa ambayo wanatakiwa kuwasilisha faini kila siku ambapo ikitokea askari hajafikia lengo basi haruhusiwi kwenda kushiriki mafunzo au kupanda cheo. Suala hili si la kupuuzia hata kidogo, kwa sababu tunajenga taifa la kubambikia wananchi makosa ya barabaranii kwa ajili ya kukusanya mapato na pia kushindwa kutoa funzo kwa madereva kwa makosa ambayo yanatosha tu askari kutoa elimu kwa Dereva kwa kosa la kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya kupunguza ajali za barabaranii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa jambo hili ndani ya Bunge lako tukufu kuhusu malalamiko haya au Waziri wa Fedha alete marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabaranii ili Bunge na wananchi wajue kuwa Serikali imeweka faini za makosa ya barabaranii kama chanzo cha kodi.

#### 4. MAPITIO YA MUSWADA WA FEDHA 2017

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa utangulizi huo kuhusiana na mfumo wetu wa kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani

inapitia muswada ulioletwa wa fedha wa mwaka 2017 kuona ni kwa kiwango gani utaathiri maisha ya walipa kodi wa nchi hii kama ifuatavyo:-

**A. MAREKEBISHO YA SHERIA YA BENKI KUU SURA YA 197 (AMMENDMENT OF THE BANK OF TANZANIA ACT, CAP. 197**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 4 cha muswada kinafanya marekebiso kifungu cha 32 cha sheria mama kwa kuongeza vifungu vipyta vya "3 na 4". Kifungu cha 3 kinasomeka kama ifuatavyo; *"All Government and Public authorities shall open and deposit all their moneys with the Bank"*.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa na maoni tofauti juu ya uamuzi wa Serikali wa kuhamisha fedha zote za taasisi za Serikali kutoka kwenye mabenki ya biashara na kuhamishia Benki Kuu, kwamba uamuzi huu kwani Benki Kuu itakuwa inashindana na mabenki ya Biashara wakati ambapo Benki Kuu inatakiwa kufanya kazi ya uthibiti tu.

Kwa kurejea kauli zilizotolewa na ma-Professor wawili wa uchumi na kunukuliwa katika gazeti la Mwananchi la tarehe 13 Februari 2016 kwamba Serikali iangalie wenzetu wa Botswana na Namibia walifanya nini katika hili, na kama Serikali inataka kuingia katika biashara basi ifunge benki yake ya biashara kama liliyokuwa lengo la kuanzishwa kwa benki ya NBC na akaunti za taasisi zote za Serikali zihamishiwe huko. Hayo yalisemwa na Prof. Anderson. Wakati huohuo Prof. Gabagambi alihoji kuwa inakuwaje Serikali inahamisha fedha zake wakati huo huo hurudi tena benki kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia hati fungani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hoja hizo ni mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba kifungu hiki cha muswada kinachopendekezwa na Serikali kisikubaliwe na Bunge lako Tukufu. Kwa utaratibu huu unaopendekezwa na Serikali dhana ya ushindani wa kibashara hautakuwa na maana.

Serikali iweke mfumo mzuri wa kudhibiti mashirika yanayotumia vibaya fedha zake zinapowekwa kwenye akaunti za Benki za Biashara na sio kuzilundika fedha BOT ambao hawafanyi biashara.

#### **B. MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA SURA YA 147**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebiso kwenye Sheria ya ushuru wa bidhaa, Sura ya 147 ya Sheria za Tanzania kwa kuweka viwango maalum (Specific rates) vya ushuru wa bidhaa vinavyotumika kwenye baadhi ya bidhaa. Inaelezwa kwamba viwango hivi vinarekebishwa kwa mujibu wa sheria hiyo na '**kwa kiwango cha mfumuko wa bei'**

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo hayo, yamepelekea kupandisha kodi kwenye bidhaa ambazo uzalishaji wake hutumia malighafi inayozalishwa ndani ya nchi kama vile shayiri, na tumbaku jambo ambalo ni dhahiri litapunguza bei za mazao hayo, na hivyo kupunguza kipato cha wakulima wa mazao hayo. Kwa mfano kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 ushuru wa bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini umepanda kutoka shilingi 429 kwa lita hadi shilingi 450 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 21 kwa lita. Hali kadhalika ushuru wa bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 umepanda kutoka shilingi 11,854 hadi shilingi 12,447 kwa kila sigara elfu moja ikiwa ni ongezeko la shilingi 493 kwa kila sigara elfu moja. Aidha kwa sigara zenye vichungi ushuru umepanda kutoka shilingi 28,024 hadi shilingi 29,425 kwa kila sigara elfu moja, ikiwa ni ongezeko la shilingi 1,401 kwa kila sigara elfu moja

**Mheshimiwa Spika**, wakulima wa shayiri na tumbaku ni kama vile wamekuwa na bahati mbaya miaka yote. Nasema hivi kwa kila mwaka lazima kodi kwenye bia na sigara ipande. Kwa kufanya hivyo, wamiliki wa viwanda vya

bia na sigara, ili wamudu kodi hizo na kuweza kupata faida ni lazima wawaminye wakulima wa mazao hayo kwa kutoa bei ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kupandisha kodi kwenye bidhaa zinazosalishwa kwa kutumia malighafi inayozalishwa hapa nchini, kwani kwa kufanya hivyo ni kuwadidimiza wazalishaji wa malighafi hiyo, na ni kuua ari ya mapinduzi ya viwanda hapa nchini kwani ili viwanda viwepo na vizalishe lazima kuwe na sekta ya kilimo iliyoboreshwa, ambapo wakulima wana motisha ya kuzalisha kutokana na bei nzuri za mazao yao.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza pia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari (Annual Motor Vehicle Licence) na badala yake kupandisha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli, dizeli na taa kwa kiasi cha shilingi 40 kwa kila lita moja ili kufidia upungufu wa mapato ambao ungetokana na kufutwa kwa ada hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema wakati wa uwasilishwaji wa bajeti mbadala kwamba; Hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania inawalipisha watanzania maskini wasio na uwezo wa kumiliki magari kodi ya ada ya mwaka ya leseni za magari (Annual Motor Vehicle Licence Fee) kwa kuihamishia kodi hiyo kwenye ushuru wa bidhaa za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa ambapo athari zake ni kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi masikini. Tulleleza kwamba, kupanda kwa bei ya mafuta kutasababisha kupanda kwa nauli katika sekta ya usafirishaji jambo litakalosababisha kupanda kwa bei za vyakula, kupanda kwa bei za kusaga na kukoboa nafaka kwa kutumia mashine zinazotumia petrol au dizeli kwa wananchi waishio vijijini, kupanda bei kwa pembejeo za kilimo, kushindwa kupata nishati ya mwanga kwa wananchi waishio vijijini kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa nk. Kwa maneno mengine bajeti hii imelenga kuwabebesha

wananchi maskini mzigo wa kodi kwa matumizi ya anasa ya watu wa tabaka la katika juu wenye uwezo mkubwa kifedha wa kuweza kumiliki magari na vitu vingine vya thamani kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya hayo, tulibainisha kwamba, hakuna chombo chochote cha moto cha usafiri wa barabaranii kinachotumia mafuta ya taa; iweje mwananchi wa kawaida asiyemiliki gari atozwe ushuru huo kwenye mafuta ya taa?

#### C. MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA, SURA YA 290

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kufanya marekebisco katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kwa kukifanyila marekebisco kifungu cha 31A cha sheria hiyo, ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango ya matangazo nchi nzima.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono uamuvi wa Serikali Kuu kukusanya ushuru wa mabango nchi nzima kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Sababu kubwa ya kupinga uamuvi huo ni kutohakana na ukweli kwamba ushuru wa mabango ni chanzo cha pili cha mapato katika halmashauri zetu, chanzo cha kwanza kikiwa ni kodi ya majengo (property tax).

**Mheshimiwa Spika**, kuzinyang'anya halmashauri zetu vyanzo vyake vya mapato na kuvihamishia Serikali Kuu kunakwenda kinyume kabisa na dhana ya ugatuaji madaraka katika Serikali za mitaa (D by D) ambayo kwa kipindi kirefu Serikali hii hii ya CCM imekuwa ikipigia upatu. Aidha, kuzinyang'anya Serikali za Mitaa vyanzo vyake vya mapato kutazidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwa sasa zitashindwa kujiedhesa na hatimaye zitakufa.

**Mheshimiwa Spika**, ukiachilia mbali mapato yatokanayo na ushuru wa mabango ambayo yamechukuliwa na Serikali Kuu, hata hivyo, Serikali Kuu kupitia Waziri wa

Fedha, imefuta ushuru wa huduma (Service Levy) kwenye nyumba za kulala wageni; imefuta ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mfano vibali vya machinjio, imefuta ada ya vibali vya kusafirishia mifugo na ada ya vibali vya kuanzisha maduka ya dawa; imefuta ada ya makanyagio minadani nk. ambazo zilikuwa ni vyanzo vya mapato kwa halmashauri zetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi kufutwa kwa ada hizo ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi. Ila haioni mantiki ya kufuta tozo hizo ambazo zilikuwa zinaziwezesha halmashauri kimapato na hapo hapo kuvitaifisha vyanzo vingine vya mapato kama vile ushuru wa mabango na kodi ya majengo na kuziacha Serikali za Mitaa zikiwa hazina chanzo chochote cha mapato.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu Serikali Kuu ikaelewa kwamba Serikali za Mitaa ni zao la Katiba ya nchi yetu kwa mujibu wa ibara **ya 143 na 145** ya Katiba hiyo, na kwamba uwepo wa Serikali za Mitaa si hisani ya Serikali Kuu. Kwa sababu hiyo, kufanya jambo lolote linalolenga kuzipuza au kuzidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zipo kikatiba ni kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 21 cha muswada kinaongeza kifungu kidogo cha "c" kinachofanyia marekebisho kifungu cha 37 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, ili kuwatambua wafanyabiashara wadogo, wanaofanya biashara katika maeneo ambayo siyo rasmi kama vile mama lishe, wauza mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mbogamboga, ndizi, na kadhalika kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazofanya.

**Mheshimiwa Spika**, ukitazama lengo la marekebisho yanayopendekezwa na Serikali, unaweza kufikiri kwamba Serikali ina nia njema na hawa wafanyabiashara wadogo. Ikumbukwe kwamba wafanyabiashara hawa wamekuwa ndio wahanga (victims) wakubwa wa uonevu mkubwa

unaofanywa na Serikali hii ya CCM dhidi yao. Hawa ndio wamekuwa wakifukuzwa kama digidigi katika kila kona ya mji na kupigwa marufuku kuendesha shughuli zao za kujipatia kipato kwa maana kwamba wanachafua mandhari ya miji. Wamekuwa wakitendewa ubaya kana kwamba wao sio raia wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu huu Serikali inaotaka kuanzisha wa kuwatambua wafanyabiashara wadogo ni kwa lengo la kuwatoza kodi na ushuru tu na si kwa lengo la kuwasaidia kama ambavyo Serikali inavyotaka kuuaminisha umma. Kama kweli Serikali ilikuwa na nia hiyo, kwa nini haikufanya hivyo kwa miaka 50 iliyopita tangu imekuwepo madarakani?

**Mheshimiwa Spika**, ni aibu kwa Serikali hii kuwageukia wafanyabiashara wadogo ambao ni wanyonge na maskini kwa lengo la kuwatoza kodi wakati imeshindwa kukusanya mapato makubwa katika sekta ya madini. Shilingi triliioni 105, ambazo Serikali imedai imepoteza katika sakata la Makinikia, kwa nini isijikite katika kuzipata hiso kwanza kabla haijaanza kufikiria kodi kwenye vitumbua na maandazi?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishangaa sana Serikali hii kufikiria vyazo dhaifu vya mapato na kuviacha vile vikubwa ambapo kama Serikali itavisimamia vizuri, kusingekuwa na haja ya kuwatoza mama lishe au wauza mbogamboga ushuru wowote.

**D. MAREKEBISHO YA SHERIA YA POSTA NA MAWASILIANO YA KIELEKTORINIKA SURA YA 306.  
(AMMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS ACT, CAP. 306)**

**Mheshimiwa Spika**, dhana nzima ya kifungu cha sheria kinachofanyiwa marekebisho wakati Bunge linatunga sheria hiyo ilikuwa ni kuwapa umiliki watanzania katika makampuni yanayomilikiwa na wageni. Kwa dhana hiyo iliyokuwepo ni dhahiri kwamba kifungu cha 7 cha muswada kina kinzana na dhana mama ya uwepo wa kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inawaomba waheshimiwa wabunge wajiulize ni kwanini hasa kifungu hiki cha muswada kinafuta tafsiri ya maneno “*local shareholder*”. Bila kufahamu chimbuko lake ni dhahiri sheria hizi tunazozitunga wenzetu watakaokuja watatuona kama vile hatukustahili kuwawakilisha wananchi katika chombo hiki kitukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba kama mazingira ya ufanyaji wa biashara ni mazuri hakuna sababu hata moja ni kwanini hisa za makampuni yanayojisajili katika soko la hisa zisinunulike. Kambi Rasmi ya Upinzani mbali ya sababu hiyo ya kushindwa kununulika kwa hisa na pia pale ambapo wanunuvi watarajiwa wanakuwa na wasiwasi kwamba mahesabu ya utendaji wa kampuni husika yana dalili za udanganyifu.

**Mheshimiwa Spika**, kama vigezo hivyo vikienda sambamba ni dhahiri hata milango ikifunguliwa kwa raia wasio watanzania ununuvi wa asilimia 25 hauwezi kufikiwa. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia mifumo yake ya ndani ya uthibiti ni kwa kiwango gani ni “**conducive**” kwa wafanyabiashara nchini kufanya biashara. Na hilo ndilo litakuwa suluhisho la tatizo hilli na sio kuongeza wigo kwa wageni, kwani kufanya hivyo kunaondoa dhana nzima ya uwepo wa kifungu hicho.

#### **E. MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MADINI, SURA YA 123 YA SHERIA ZA TANZANIA**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 ya Sheria za Tanzania, kwa kuingiza kitu kinachoitwa ‘ushuru wa ukaguzi’ ('inspection fee'). Ili kuelewa maana ya mapendekezo haya, ni muhimu tufahamu aina na kiwango cha kodi, ushuru, tozo na malipo mengine ambayo makampuni ya madini yanawajibika kulipa sasa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria ya Madini kama ilivyo sasa, kodi au ushuru au tozo muhimu kuliko zote

ni mrahaba (royalty). Hivyo basi, kwa mujibu wa kifungu cha 87(1) cha Sheria hii, mwenye leseni ya kuchimba na/au kuuza madini anawajibika kulipa mrahaba kwa bei ya mauzo (gross value). Viwango vya mrahaba kwa mujibu wa kifungu hicho ni 1% kwa mawe ya thamani (gem); 3% kwa ajili ya madini ya viwandani (industrial minerals), chumvi na madini ya ujenzi kama mchanga, kokoto, mawe n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, mwenye leseni ya kuchimba madini ya vyuma (metallic minerals) kama vile dhahabu, shaba, fedha (silver) na madini ya kundi la platinum (platinum group of minerals), anawajibika kulipa mrahaba wa 4%. Kwa mawe ya vito (gemstones) na almasi pamoja na madini ya urani (uranium), kiwango cha mrahaba ni 5%.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Sheria za kusimamia rasilimali zetu kurekebishwa ikiwemo Sheria ya Madini limekuwa linapigiwa kelele na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mingi. Serikali baada ya Taarifa ya Kamati ya pili ya Makinikia (pamoja na mapungufu yake) imeahidi kuwa Sheria na Mikataba yote ya Madini italetwa Bungeni ili iweze kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji kama marekebisho haya yanayopendekezwa katika muswada huu ndiyo kero kubwa iliyokuwa inapigiwa kelele na Bunge na Serikali kwa muda wote huu?

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo marekebisho haya yaliyoletwa ndani ya Bunge ambayo kimsingi yamelenga kuongeza Asilimia moja ya ushuru wa ukaguzi yanapingana vikali na sheria hiyo hiyo ya madini ambayo kimsingi inamlinda mwekezaji kwa kiasi kikubwa mathalani kupitia "Financial stability Clause" kifungu cha 10 ambacho kinazuia ongezeko lolote la kodi ambalo linaweza kuyumbisha Mtaji wa mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa badala ya kukimbilia kuongeza

asilimia moja ya "Inspection" ili iweze kuongeza mapato ya Serikali, Serikali ilete muswada wa kurekebisha Sheria zote zinazosimamia uwekezaji katika sekta ya madini ili yafanyike marekebisho ambayo yatalinufaisha taifa kuliko kufanya marekebisho haya ambayo yanaanza kuleta mgongano wa sheria yenye na si kuioanisha.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya marekebisho hayo ya Sheria, Serikali ilete mikataba yote ya sekta ya madini ili ipitiwe upya na Bunge kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**F. MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI SURA YA 438 {AMMENDMENT OF THE TAX ADMINISTRATION ACT, (CAP.439)}**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 43 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 76 cha sheria kwa kuweka kifungu kipyaa 76(4) kinachosomekwa kuwa;

**"(4) Interest payable under this section or under any tax law shall not be affected or waived for the reason of delay due to court proceedings or any other dispute resolution process"**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu hiki kinataka kuingilia uhuru wa Mahakama pale mlalamikaji anapopeleka shauri lake mahakamani. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki kitawanyima haki wafanyabiashara ambao kwa njia moja au nyingine wanaweza wasitendewe haki na pia kinaondoa nguvu ya mahakama katika kutoa haki, kwa kuzuia jambo linalobishaniwa hadi uamuzi ufikiwe au utolewe. Hii ni kwasababu hakuna mantiki yoyote ya kupeleka shauri Mahakamani endapo mtuhumiwa hajaridhika halafu mtuhumiwa huyo alazimike kulipa faini kabla Mahakama haijathibitisha kosa lake. Endapo shauri linaendelea ni vema mtuhumiwa asilipe faini mpaka pale itakapothibitika kutenda haki. Katiba yetu inatambua kwa uwazi kabisa hakuna chombo chochote kinachoruhusiwa kuingilia uhuru wa Mahakama. Hivyo, Kambi Rasmi inaitaka

Serikali kubadili kifungu hiki na badala yake kitoe uhuru kwa Mahakama kama Katiba ya nchi inavyotaka.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 44 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 78 cha sheria, kwa kufuta kifungu cha "3" na kuweka kifungu kipyaa kinachosomeka kwamba;

*"(3) A penalty under this section shall, in case of income tax, apply separately for a failure to file a tax return that is an estimate or provisional amount, and failure to file a tax return incorporating the final amount"*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inakiona kifungu hiki kuwa kitakuwa ni kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara wadogo ambaao wanataka kurasimisha biashara zao, badala ya kufanya hivyo itawabidi waendelee kukaa kwenye sekta isiyo rasmi na Serikali itaendelea kupoteza hata kile kidogo ambacho ingekikusanya. Kwa maana nyingine ni kuwa kifungu hiki sio rafiki katika kuongeza wigo kwa wafanyabishara kurasimisha biashara zao. Tukumbuke kwamba kufanya biashara kwa mazingira ya nchi hii uanza kwa kubahatisha na pia elimu ya utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu ya biashara ni wafanyabishara wachache wenye elimu hiyo.

#### **G. MAREKEBISHO YA SHERIA YA BANDARI SURA YA 166 (AMMENDMENT OF THE PORTS ACT, CAP.166)**

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli kwamba tozo kadhaa zinazotozwa katika bandari, mbali ya kodi inayokusanywa na TRA ikiwa ni moja wapo ya vyanzo vyaa mapato kwa ajili ya uendeshaji wa bandari husika.

*"wharfage" means a charge imposed in respect of all goods and goods in containers that are (i) loaded or unloaded from a vessel at a public port facility; (ii) unloaded overside from vessel to water or loaded from water to vessel, landed from or placed in the water or loaded on or unloaded from a vehicle within the limits of a public port.*

Hivyo basi, kwa kuwa *"Wharfage charges"* ni mojawapo ya tozo zinazotozwa katika bandari zetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kitendo cha TRA kukusanya tozo hizo na kuwekwa Benki Kuu katika akaunti maalum itakayofunguliwa ni kitendo cha kupunguza ufanisi wa bandari, kwani ufanisi wa bandari unategemea kwa kiasi kikubwa ni kwa kiwango gani inavyojitosheleza kimapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona pendekezo hili la Serikali ni kama *"kifo cha mfa maji haishi kutapatapa"*, kwa maana kuwa inakataa kusema ukweli kuwa mapato ya kodi yameshuka vibaya sana, kinachofuata ni Serikali kukusanya tozo na vyanzo vingine vinavyopatikana ili kuendelea kuonekana kuwa mapato ya kodi yameongezeka.

#### **H. MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA MAJENGO YA MAMLAKA ZA MIJI [AMENDMENT OF THE URBAN AUTHORITIES (RATING) ACT]**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inafanyia marekebisho Sheria ya Kodi za Majengo ya Mamlaka za Mihi sura 289 ambapo pamoja na mambo mengine inatoza kodi ya majengo, kwa majengo yaliyofanyiwa tathmini na yasiyofanyiwa tathmini kwa kima cha chini cha shilingi 10,000 na majengo ya ghorofa shilingi 50,000.

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 64 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 3 cha Sheria. Kifungu hicho kinatoa maana ya neno 'rateable property' (nyumba zinazotozwa) kikilenga kuwaondoa katika tozo wananchi wanaomiliki nyumba za tope, tembe na nyininge zinazofanana na hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa nyumba hizo zimeondolewa katika tozo lakini pia ni muhimu sana Serikali ingefanya makadirio ambayo hayatawaumiza hata wale wasio na kipato lakini wamebahatika kupata misaada ya kujengewa nyumba za tofali. Wapo wananchi wengi amba

wamejengewa nyumba kwa misaada kutoka kwa ndugu, jamaa, marafiki, mashirika, taasisi za dini, wafadhili n.k kutokana na hali zao za kuchumi. Kitendo cha kuwajumuisha katika kodi sio jambo zuri kwani linazidisha hali ya umaskini katika kaya hizo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia namna bora zaidi ya kufanya ukadiriaji kwa kuangalia pia kipato halisi cha kaya hizo badala ya kujikuta ikiwatoza kodi hata wale wenye hali duni sana kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kifungu cha 38 ilifuta vifungu vya 31A na 31B vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura Namba 290 ambayo ilitoa mamlaka kwa Halmashauri kukusanya kodi ya majengo kwa mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kueleza kwa kina umuhimu wa kodi hiyo kubaki katika Halmashauri zetu, Serikali ilitia pamba masikioni na matokeo yake wakashindwa kukusanya kodi hiyo kwa ukamilifu na kuziacha Halmashauri kukosa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa kodi hii irudishwe na kukusanya na Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi zao na kwa ukweli kwamba ngazi hiyo ya utendaji ndiyo illio na taarifa sahihi kuhusu nyumba ambazo zimesamehewa kulipa tozo na nyumba ambazo zinastahili kulipa kodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa kodi ya majengo kwa maeneo ya vijijini haitakuwa tofauti na kodi ya kichwa ambayo ilifutwa mwishoni mwa miaka ya tisini. Hii ni kwa sababu yapo maeneo ambayo wananchi wanapata misaada kupitia mfuko wa TASAF. Hii haitakuwa na maana kwa sababu Serikali itakuwa imetoa mkate kwa mkono mmoja na kuuchukua kwa mkono mwingine. Hivyo utozaji wa kodi hii ya majengo haina tofauti na kodi ya kichwa iliyofutwa miaka hiyo ya tisini.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuja na majibu kuwa marekebisho katika sehemu hii yanagusa mamlaka za majiji, Manispaa na Miji pekee na sio Vijiini lakini ukitosha Sheria yenye inayofanyiwa na marekebisho kifungu cha tafsiri kinagusa Miji na Mamlaka za Wilaya ambayo ipo chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ambayo inaweka utaratibu wa namna Vijiini na Vitongoji vinyoyeweza kutangazwa kuwa mamlaka za Miji Midogo, ambapo kimsingi vijiji ni sehemu ya sheria hiyo. Serikali kwa hili imelipotosha Bunge.

## **5. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mjadala wa bajeti kwa asilimia kubwa ulijikita katika Sheria ya Usalama wa Barabarani, Sura 168. Kwa bahati mbaya sana hadi tunatayarisha maoni haya pamoja na muswada mpya wa fedha ulioletwa hakuna marekebisho ya sheria hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufanuzi ni kwa namna gani ada ya mwaka ya Leseni ya Magari (**Annual Motor Vehicle Licence fee**) imefutwa? Vinginevyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaweza kuamini kwamba Serikali “**imewahadaa watanzania**”.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inafahamu kuwa ili Serikali iweze kutekeleza wajibu wake kwa jamii ni lazima kodi zilipwe, jambo hili ni lazima lifanyike. Katika kufanya hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa litakuwa ni jambo la muhimu kuhakikisha kuwa viwango vya kodi vinakuwa rafiki na kodi zinakuwa chache kiasi kwamba hakutakuwa na mlipa kodi kujishauri ni jinsi gani atalipa kodi husika.

**Mheshimiwa Spika**, tunafahamu kwamba muswada wa fedha ambao ndio Sheria ya Fedha ni ridhaa ambayo Serikali inaipata kutoka kwa wananchi kuitia kwa waheshimiwa wabunge kuwa wako tayari kulipa kodi kama ambavyo inapitishwa na Bunge. Kwa muktadha huo kama waheshimiwa wabunge wanatoa ridhaa yao kuwa tozo na

shuru mbalimbali ziongezwe, ambazo kwa muktadha wake zitaongeza gharama kwa malighafi zinazotoka kwa wakulima, maana yake ni kudidimiza kilimo ambacho kinatoa ajira kwa watanzania zaidi ya asilimia 75.

**Mheshimiwa Spika**, kuna usemi unaosema kuwa “**boys in the backroom**” ukiwa na maana kuwa kuna kundi la watu wanaofanya maamuzi lakini hawaonekani sehemu yoyote lakini maamuzi yao yanakuwa athari kwa kundi kubwa la watu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imetumia usemi huo kutokana na ukweli kuwa, sisi waheshimiwa ndio tunaotunga sheria kwa mujibu wa sheria, Serikali kazi yake ni kuleta mapendekezo tu. Lakini kwa kuwa kuna “**boys in the backroom**” bunge linakuwa ni chombo cha kufuata maelekezo tu. Hii ni hatari sana katika mustakabari wa Tanzania ijayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa sasa ni muda mwafaka kwa chombo hiki kikuu cha kutunga sheria kusimamia mamlaka yake ya kikatiba na kisheria. Imebidi kusema haya kwa uchungu mkubwa kwa kuwa waheshimiwa wabunge wamelalamika kuhusiana na kuondoa ongezeko la sh.40 katika lita moja ya mafuta ya taa, lakini Serikali inasema kuwa uwiano kati ya mafuta ya taa na diseli ukiwa mkubwa maana yake unaruhusu uchakachuaji wa mafuta ya diseli. Kwa kigezo hiki maana yake ni kwamba wananchi wetu waendelee kuumia ili kuwardihisha wachache.

**Mheshimiwa Spika**, majibu hayo ya Serikali yanaonesha kuwa bado kuna udhaifu mkubwa kwa upande wa Serikali katika kuzuia udanganyifu unaofanywa na watu wasio na nia njema na uchumi wa nchi yetu. Kwa Waheshimiwa wabunge kukubali hoja hiyo ya uchakachuaji na kuacha maslahi mapana ya wananchi wetu waliyoyaonesha wakati wakichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni jambo la ajabu kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**DAVID ERNEST SILINDE (MB)**  
**k.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-**  
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**  
**22.06.2017**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo ambayo yalikuja baadaye, lakini kabla sijayasoma hayo matangazo, Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ukiacha maneno ya mwanzo, haya ya mwisho hayako kwenye nakala ya hotuba niliyonayo mezani na kwa kuwa Kanuni zetu zinataka tusome hotuba tulizozileta, haya ya mwishoni hayako kwenye hii niliyonayo mimi. Kama kuna ambaye anayo ambayo yamo hayo, basi yatabaki kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Kama hayapo, utaratibu wetu wa kikanuni ufuatwe, yale ambayo hayajawekwa kwenye maandishi haya hayatakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo niliyonayo ni ya wageni; kuna wageni ambaao inaonekana majina yao hayakuja hapa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Ntimizi, wageni hawa wanatoka kwenye Jimbo lake Kata ya Lutende. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Ntimizi. (*Makofii*)

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Japhary Michael ambaao wanatoka Kanisa la *FPCT*, Majengo, Moshi Mjini. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa William Mganga Ngeleja ambaye ni Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, tangazo hili linahusu mashindano ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Novemba na Desemba 2017. Mheshimiwa

Ngeleja anawatangazia Wabunge wanamichezo kwamba maandalizi ya mashindano ya michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo yatafanyika nchini Tanzania mwishoni mwa mwezi Novemba hadi mwanzoni mwa mwezi Desemba, 2017 tayari yameanza. Ili kuimarisha vikosi vya timu ya Bunge, Uongozi wa Bunge *Sports Club*, unawahimiza Wabunge wanamichezo ambao hawajajsajili kujisajili kwa viongozi ambao watatajwa majina yao hapa.

Kwa upande wa soka, watu ambao wanaweza kuwaandikisha Waheshimiwa Wabunge, ni Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Omary Mgumba. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kushiriki kwenye mchezo wa soka wakajiandikishe kwa Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Omary Mgumba.

Kwa upande wa mpira wa pete, Waheshimiwa wanaotaka kucheza mpira wa pete wakajiandikishe kwa Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha. Kama Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha watakuwa hawajamuona basi wanaweza wakajiandikisha wakati wa mazoezi asubuhi.

Aina ya tatu ya mashindano ni wavu kwa upande wa wanaume na hawa wanatakiwa wajiandikishe kwa Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

Pia kwa upande wa wavu wanawake, Mheshimiwa Saumu Heri Sakala.

Vile vile kwa upande wa *basketball* wanawake na wanaume Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

Upande wa riadha wanawake na wanaume Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, ambaye naamini mwaka huu atajipanga kukimbia. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, upande wa kuvuta kamba, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama na upande wa gofu Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba kuhusu programu ya mazoezi itatangazwa kabla ya Mkutano huu wa Bunge kuahirishwa. Kwa hiyo, kwanza zoezi la mwanzo mnaombwa Waheshimiwa Wabunge mijandikishe ili timu zetu ziweze kubaki na makombe hapa nchini, maana nchi zetu za Afrika Mashariki zote zitakuja hapa, ni vizuri tukijipanga vizuri.

**WABUNGE FULANI:** Ngumi je?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanauliza kama kuna mchezo wa ngumi, ngumi watu wataumizana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na zoezi linalofuata. Uwasilishaji umekwisha na tayari nimepata majina hapa ya wachangiaji kutoka vyama vyote kwa mujibu wa uwiano tullonao. Tutaanza na wachangiaji kutoka Chama cha Mapinduzi na tutaanza na wafuatao: Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

Hawapo, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala, wajiandae Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Japhet Hasunga. Mheshimiwa Dkt. Dioorus Kamala.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu muhimu ulio mbele yetu. Ni Muswada muhimu kwa sababu bajeti tuliyopitisha na miongozo mingine inayoendana na hiyo bajeti, utekelezaji wake utategemea nguvu za kisheria za sheria ambayo tutaipitisha leo na ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini gazeti la *Citizen* la leo limeandika habari ambayo sitatumia muda mrefu kuisoma. Kuna wakati nilishazungumza hapa Bungeni kwamba suala la mitumba linapoelekea litatuletea changamoto kubwa. Kwa sababu kuna *petition* imepitishwa kule Amerika ambayo sasa inalenga kuzuia biashara kati ya

nchi za Afrika Mashariki na Amerika na kuondoa kabisa nchi za Rwanda, Tanzania na Uganda na nchi nyinginezo katika *list* ya AGOA.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni jambo kubwa hilo, kwa sababu tunapoijenga Tanzania ya viwanda na yote mengine tuliyopitisha, tunapoondolewa kwenye orodha ya AGOA maana yake sasa kutakuwa na mtikisiko lakini hata bajeti yetu ambayo tulitarajia kuna baadhi ya kodi tutakusanya, hatutazikusanya. Kwa hiyo, ni jambo ambalo nitaomba wahuksika walitazame na waone ni hatua zipezinaweza zikachukuliwa na kama kuna lolote tunaweza tukafanya, basi tulifanye ili kuweka mambo sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nilisema na hili ni la jumla, mwaka 2007 nchi za Afrika Mashariki tulikubaliana kwamba bajeti ya nchi za Afrika Mashariki itasomwa siku moja na wakati wa kuisoma ni uleule. Lengo ni kwamba tulipooanza kutekeleza *Customs Union* asilimia kubwa ya maamuzi ya kibajeti yanafanyika katika vikao vya Afrika Mashariki. Maana yake ni kwamba muda mwingi tunaoutumia hapa tunazungumza kodi zile tu ambazo tunakuwa hatuamui sisi wenyewe na zilizo nyingi zinaamuliwa katika ngazi ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikubaliana iwe siku moja, lakini kinachoendelea kutokea hivi sasa ni kwamba baadhi ya nchi zinaamua kusoma bajeti zinavyotaka. Nyote mnafahamu na mnatambua kwamba bajeti ya mwaka huu ni kwamba Rwanda, Uganda na Tanzania ndiyo pekee tulisoma kwa siku moja wallobaki hawakuweza kusoma kwa siku moja kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lina *implication* kwenye masuala ya sera. Jambo hili lina *implication* kwamba mambo yote unayokuwa unayatoa kisera hapa ya kodi na hatua wengine wenye akili wanakuwa wameshajipanga kwenye magodauni yao ili kufanya mambo ambayo yatasabotage kile ambacho unajipanga. Kwa hiyo, nimeona niliseme hilo kwa sababu lina *implication* kubwa kisera na

kwenye utekelezaji wa bajeti siyo baadaye tunalaumia tu, haitiskelezezi lakini kumbe kuna mambo ambayo tungeweza kuyajua na tukayafanya kazi yanetusaidia kwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho la jumla ni kwamba ukiisoma hii *amendment*, mimi siyo mwanasheria nitangaze hiyo *interest* siyo mtaalam wa sheria, nilipoitwa kusoma na nikapewa nafasi kabisa kwa bahati mbaya nillitwa sehemu nyengine na nikapewa *offer* kubwa zaidi kwa hiyo nikaachana na sheria. Nilipewa *offer* kubwa zaidi kwamba niende sehemu nisome digrii ya kwanza na nikimaliza pengine nisome ya pili na nisome ya tatu na nipate na ajira. Kwa hiyo, nikaamua kuachana na haya mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho nakisema na naomba wataalam wetu waandishi wa sheria watusaidie, ni la jumla hili tuone kama inawezekana, unaposoma hizi *amendments* zote kwa mfano *amendment of section 63*, huu ni mfano tu, inasema:-

*"The Principal Act is amended in section 63 by-*  
*(a) deleting paraghaph (d)".*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili kwa wanasheria waliobobeza ni jambo jema kwao na kwa wale ambaowana ofisi zao Wabunge zenye nyaraka zote, maana ofisi ya Mbunge ni kwamba unakuwa na wasaidizi, unakuwa na nyaraka zote na kila kitu, kwa hiyo ukitaka kitu chochote unapata. Hata hivyo, sisi hapa sote hakuna mwenye ofisi hapa Dodoma na sote hapa hakuna ambaye anaweza akasema anajua hiyo *Principal Act* inasema nini, inabidi uende *library* utafute uiangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kushauri kwamba kama itawezekana wataalam wetu wa kuandika sheria pale wanapotaja kifungu kinachoondolewa wakitaje chote pale

ili ninapopitisha hapa nijue kinachoondoka ni hiki na kinachowekwa ni hiki vinginevyo ni jambo gumu kueleweka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mtaalam wa sheria unajua kwamba inakuwa ngumu sana unapokuwa unapitisha *amendment* lakini unachopitisha hukijui. Ni kama unafanya mchezo tu lakini waliobobe a wao wanajua na wenye nyaraka zote na wanaotunza hivi vitu wanakuwanavyo. Mwingine anaweza kusema nyie Wabunge mnakuwa wazembe, lakini hali halisi ndiyo hiyo, hivyo, inabidi tuangalie tuone tunafanyaje kurekebisha hali hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia kwa haraka ni kwamba ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha kuna kitu kinaitwa *stay of application*. *Stay of application* unakuta mtu anaomba na tunakubaliana ndani ya Afrika Mashariki kwamba fulani anaruhusiwa asitekeleze jambo fulani, wanakubaliana kwamba fulani ameruhusiwa asitekeleze hili kwa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kingine wataalam wanaita *duty remission* wanakwambia hiyo kodi uikusanye au kama huikusanyi itakusanya baadaye irejeshwe. Hata hivyo, uzoefu umeonesha hata zile kodi zinazosemwa zitakusanya, Waziri wa Fedha atakuwa anaelewa wala hawazikusanyi tena, ikishatoka imetoka, hazitakusanya na wala hazitarejeshwa. Mambo haya ukiyatazama maana yake ni kwamba tuna tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaelewa na Waziri wa Fedha anaelewa kuna kitu kinaitwa *Uganda list* ambapo Uganda tuliipa msamaha mkubwa sana wa kodi na matokeo yake ni kwamba kuna vitu vingi vinaingia Uganda na vinatakiwa viuzwe Uganda tu lakini vinaishia kuja hata Tanzania. Unapokuwa unafanya hivyo maana yake huku tunapoimba wimbo wa kujenga viwanda tutakuwa hatuwezi kuvijenga kwa sababu mtu atakwambia kuna vitu vyaa gharama nafuu vinakuja. Kwa hiyo, ni eneo la kuangalia,

sijui tutafanyaje lakini ni eneo gumu sana ambalo nimeona niliseme hapa ili tuone tunajipanga namna gani, kwa sababu vinginevyo tutaishia kusema bajeti haitekelezeki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja. Tunataka kujenga mtambo mzuri wa *liquid gas cylinder*, lakini wakati tunakubaliana kufanya hivi na hapa Tanzania kuna watu wameshawekeza wanazalisha hizi *cylinder*, kuna nchi moja sitaitaja kidiplomasia yenye we imeamua kufuta asilimia 25 ya kodi imeweka zero. Maana yake yenye we inataka hizi *cylinder* zisitoke ndani ya East Africa maana yake zisitoke Tanzania, maana yake *initiative* zetu za kuwezesha kuwa na viwanda ndani ya Tanzania hazitawezekana, sasa hii inaleta tabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye sekta ya chuma. Hapa Tanzania kuna viwanda vingi vimewekeza kwenye chuma lakini wakati tunasema ukitoa chuma kilichokuwa *processed* kutoka nje basi tulipe asilimia 10 na tumeeleza kwenye sera zetu za kodi lakini wengine wao wanasema ni sifuri. Wanaweka sifuri kwa sababu wana *interest* ya kuvitoa nje, wakivitoa nje wakaleta kwao maana yake viwanda vya chuma vilivyopo Tanzania havitaendelea, maana yake hata hiyo Mchuchuma tunayozungumza, hata hao wawekezaji hatutawapata. Haya ni mambo ambayo lazima tuijilize mara kwa mara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma yako mambo mengi hayaishii tu kwenye bidhaa za chuma yanaenda kwenye *textile*, ngozi, *garments* na vitu vingine vingi. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa ambapo tusipoitazama, tukachukua juhudzi za makusudi, basi hatutaweza kujenga uchumi wetu kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia utalii ni jambo muhimu na tumechukua *measures* za kusaidia kuboresha utalii lakini nadhani katika bajeti ijayo pia tujipange kuchukua hatua kubwa zaidi. Kwa sababu ukiangalia hapa Tanzania tuna changamoto ya kuwa na taasisi nyingi zinazoshughulikia

ku- *regulate* utalii. Wenzetu Kenya wao wameanza kuwa na taasisi moja tu inayoshughulika utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia tumetenga shilingi ngapi za kusaidia utalii, sioni ikijitokeza moja kwa moja lakini ukiangalia kwa wenzetu unakuta wao wametenga kwa mfano shilingi bilioni moja kwa ajili ya *tourism recovery*, wametenga pia shilingi bilioni nyingine moja kwa ajili ya kutunza yale masoko ya zamani yaendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilishangazwa na wataalam wetu wa utalii walikuja na mkakati wao wa kutangaza utalii pale Brussels nikauliza mbona Ubelgiji haimo? Wakasema hii haipo kwa sababu hapa utalii tulishaanza tunaenda sehemu mpya. Nikawaambia usiende tu sehemu mpya ukasahau ya zamani, ya zamani kama unayo mfano Uingereza, Ujerumania lazima uendelee kuwatunza, usiache tu ukakimbilia pengine. Haya nayasema tu kwa sababu pamoja na kwamba bajeti yetu tumeiweka vizuri, lakini najua lazima tujipange kuweka vizuri zaidi katika bajeti ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa muda ulionipa na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Fedha wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuja na Muswada mzuri sana. Naipongeza Serikali kwa sababu wenzetu wa upande wa pili wamesema bajeti ya mwaka huu ni bajeti

ya ajabu na wamesema maneno mengi. Nami nataka niseme kweli ni ya ajabu bajeti ya mwaka huu. Ni bajeti ya ajabu kwa sababu ni bajeti ambayo imesikia kilio cha Watanzania, ni bajeti ambayo imezingatia maoni ya Wabunge, maoni ya wananchi wote yaliyotolewa katika sehemu mbalimbali, ni bajeti inayokwenda kutatua matatizo ya nchi hii, ni bajeti ya ajabu kweli kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naipongeza sana Serikali kwa usikivu wake. Ukisoma Muswada huu kwa asilimia 80 umezingatia sana maoni ya Kamati ya Bajeti, maoni ya Wabunge yamezingatiwa, ni mambo machache tu ambayo yamebaki ambayo bado tutaendelea kurekebisha kadri muda unavyoendelea. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali na nasema ni bajeti nzuri na Muswada ni mzuri, ni Muswada ambaao umezingatia sana maoni yetu. (*Makoffii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu mchango wa asilimia 15 wa mashirika ya umma. Kwa mujibu wa sheria tuliweka kwamba mashirika yote ya umma yachangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali asilimia 15. Hata hivyo, hatukuweka tahadhari kwamba wanapochangia ni utaratibu gani utumike katika kukokotoa kodi ya mapato, wakati yale mashirika yatakapokuwa yanatengeneza vitabu vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa ilivyo ule mchango ambaao unatolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali wanapoenda kukokotoa kodi ya mapato (*corporate tax*) kwenye zile taasisi, mchango huu hauhesabiki kama sehemu ya gharama ya taasisi husika. Hivyo inasababisha mapato ya taasisi yaonekane ni makubwa kwa sababu hii inawekwa pemberi, halafu ndiyo wanapiga kodi ile *corporate tax*. Matokeo yake ni kwamba kunakuwa na *double taxation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linaweza likatatuliwa *administratively* tu. Linaweza likatatuliwa kwa kurekebisha kipengele hicho kwenye yale mashirika ya umma na kufanya kwamba ule mchango unaokuwa umetangulia wa asilimia 15 uwe ni *tax deductible* utolewe iwe ni sehemu ya gharama

ya yale mashirika kabla ya kufikia hatua ya kukokotoa kiasi kinachotakiwa kutozwa *corporate tax*. Hii itasaidia sana mashirika ya umma yaweze kuendelea kufanya kazi sawasawa na hivyo hakutakuwa na *double taxation*. Huo ni ushauri ambao naipatia Serikali safari nyingine waweze kuliangalia ili kusudi waweze kurekebisha kipengele hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo wamefafanua kuhusu *property tax* ambavyo itakuwa inatozwa. Kwenye sheria hii wamesema kwamba watakuwa wanatoza Halmashauri za Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji, naipongeza sana kwa kuondoa Halmashauri za Wilaya. Kodi hii ingeenda mpaka kwenye Halmashauri zile za Wilaya ingeleta matatizo au malalamiko mengi sana kule vijijini, lakini kwa kuziondoa zile Halmashauri za Wilaya imekaa vizuri sana, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongezea hapo napenda kushauri kwamba mfumo ule wa kulipa kodi uwemzuri kabisa. Kwa kuwa wamesema tutakuwa tunatumia mtindo wa kielektroniki basi wauimarishe ili wananchi wapewe namba rasmi za kuweza kulipa moja kwa moja badala ya kuanza kuhangaika kupanga foleni na kusumbuka katika kuilipa hiyo *property tax* katika ofisi za TRA.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hilo, naipongeza Serikali kwa kuzifutia shule za watu binafsi pamoja na vyuo baadhi ya kodi, kwa kweli wamesikia vilivyo. Hili suala la *property tax* bado Serikali halijaliangalia sana, ningomba nalo iliangalie kwa sababu shule binafsi zile ardhi zinamiliki kwa *public use*. Kwa kuwa zinamiliki kwa *public use*, ina maana hata yale malipo ya *land rent* yafuate misingi ya *public use*. Pia *property tax* kuchaji madarasa kwa kweli inakuwa siyo vizuri sana, nalo hilo mngeliangalia pengine linaweza likasaidia sana katika kupunguza malalamiko ya hizi shule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu hii *industrial sugar* yaani

sukari inayotumika viwandani. Naipongeza Serikali kwa utaratibu waliouweka na kwamba kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana ya hawa wanaotumia sukari hii. Kumekuwa na ucheleweshaji sana wa *refund* lakini sasa hivi Serikali kwa kuwa imeamua kuja na *Escrow Account*, nashauri wahakikishe kwamba hii *account* inafunguliwa haraka kusudi waweze kuhakikisha kwamba vile viwanda vinarejeshewe mapema kadri inavyowezekana kusudi viendelee na uzalishaji bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa vile viwanda vinadai hela nyngi sana Serikalini jambo ambalo siyo suala zuri sana. Kwa hiyo, ni vizuri hii *account* ifunguliwe haraka waharakishiwe yale madai kusudi waweze kuondokana na hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu *wharfage* ambayo tumesema kwa mujibu wa sheria hii sasa itakuwa inakusanywa na *TRA*. Kama *TRA* watakusanya nakubaliana kabisa lakini ningeomba nishauri labda pengine zile bidhaa za nje zote *TRA* wanaweza kukusanya bila tatizo lolote kwa sababu wana-calculate kutokana na *value* ya zile bidhaa lakini bidhaa za ndani (*local goods*), nafikiri hii *wharfage* pengine *TRA* itabidi washirikiane sana na bandari katika kuhakikisha wanatoza kwa usahihi maana kuna usumbufu na kuna vibandari vingi vidogo. Hii pengine itasababisha *TRA* wakashindwa sana kufanya kazi hiyo, basi wakishirikiana na bandari wanaweza wakakusanya vizuri zaidi na zote zikatumika na zikaingia katika huo mfuko kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuipongeza Serikali ni hatua ambazo zimechukua katika kuhakikisha kwamba inapunguza kodi kwenye zile kodi za wawindaji wa kitalii, zile *hunting blocks* wamepunguza kodi mbalimbali, kwa kweli ni hatua nzuri sana ambazo zitasaidia hii sekta iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado VAT kwenye utalii haijaangaliwa, ni vizuri tukaifanyia utafiti, ni vizuri tukaiangalia kwa undani ili tuone madhara ambayo yanatokana na hii kodi ya utalii kusudi tuweze kuimarisha sekta hii na tuweze kupata mapato makubwa zaidi ili yaweze kusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama nilivyosema Muswada huu ni mzuri sana na utatusaidia sana katika kuleta maendeleo ya nchi na naamini vilio na michango yetu yote imezingatiwa. Ndiyo maana wengine walikuwa wanalamika wanasema mbona wameongeza sheria nyingi, sheria zimeongezeka baada ya Serikali kusikia vilio vya Wabunge. Baada ya kupata michango imebidi yale maeneo yote ambayo Wabunge wamechangia, yaingizwe katika Muswada huu ili kusudi Serikali iweze kwenda kutekeleza majukumu kwa kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kazi hii imekuwa ni nzuri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawapongeza sana Serikali, naomba tushikamane, twende tukafanye kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii ya *Finance Bill*. Awali ya yote, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, Muswada wa Sheria ya Fedha ni vema ukaletwa Bungeni siku ile wakati Waziri wa Fedha na Mipango anaposoma bajeti kuu kwa sababu na huu ni Muswada kama Miswada mingine tofauti tu ni kwamba huu ni Muswada wa Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba niipongeze sana Serikali kwa bajeti nzuri sana na kwa Muswada mzuri sana, Muswada huu ni kwa Watanzania na kwa manufaa ya Watanzania. Nikisema hivyo nina mifano michache kabisa kwamba Serikali hii sikuvi sasa imeweza kuwa na *zero rate* kwenye *auxiliary services*, imeweza kuondoa *exemption* kwenye *capital goods* kwenye zile sekta ambazo ni za kimikakati zaidi, imeweza pia kutuondolea *motor vehicle license*, imeweza kuondoa *SDL* kwenye mashule binafsi na mengi kwa kusikiliza kilio cha Watanzania kwa manufaa ya Watanzania. Nawapongeza sana sana katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, tuko katika sera ya viwanda na uchumi kwa Awamu yetu hii ya Tano, sasa jambo la kwanza ambalo tunatakiwa ni *ku-promote* viwanda vyetu na bidhaa zetu za ndani bila kuzididimiza na jambo la msingi ni kuziangalia na kuziboresha zaidi, kwa viwango ili tusiweze kudidimiza bidhaa zetu hizi za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu, viwanda vya vinywaji baridi, Serikali ilitaka kuongeza *excise duty* pale ya *five percent* na wao wakaomba isiwekwe, wakakubaliwa wakapata *relief*, waka-expand wakaongeza ajira. Mfano kule kwetu Mbeya kuna *Pepsi*, *Coca-Cola* na kadhalika, hivyo Serikali ikapata faida zaidi. *The more relief the better for the economy* wote tunaelewa hilo, vilevile ajira imeongezeka, bei inakuwa siyo kubwa, uchumi pia una-expand, pia kuna kuwa na *value chain* nzuri na vilevile inakuwa pana hata kwa akinamama lishe, kwa Machinga, na kadhalika, hiyo yote ni kwamba wasipoongeza hii kodi kwani pia hata ile *corporate tax* pamoja *income tax* pia vyote vinakuwa juu kwa pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwa wale wenye viwanda vikubwa, wanaotumia sukari ya viwandani, waliwekewa utaratibu wa kutozwa *bond* ile ya asilimia 15, hadi Serikali itakapotathmini matumizi sahihi ndiyo warejeshewe hiyo pesa. Cha ajabu pesa hii hairejeshwi.

Tunaambiwa *Escrow Account*, basi iweze kufunguliwa kwa haraka sana, kwa sababu mpaka dakika hii tunaongea kuna bilioni 20 za wafanyabiashara hazijareshwa kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, naamini sasa masuala ya uingizaji sukari yamekwisha, udhibiti wa mianya pia umeongezeka katika Awamu hii ya Tano, kwa hiyo hakuna longolongo. Kwa maana hiyo, naamini yote hayo yatafanyika na wafanyabiashara hawa naamini *Escrow Account* ikifunguliwa watarudishiwa fedha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Mpango wa Mipango pamoja na timu yako nzima na Serikali sikuvi, mmesikia kilio cha Watanzania, hii ni bajeti ya mfano kwa mara ya kwanza. Kama nilivyotoka kuzungumza katika *opening remarks* yangu, Watanzania wote huko mitaani wamefurahishwa na bajeti hii na kila mtu anashangilia wala siyo siri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote mazuri naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, kama tutakuwa bado na muda tutaendelea na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha na Wataalam wote wa Serikali, Kamati na nitumie nafasi hii tu kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, Kamati imekuwa na *engagement* ya *almost* siku mbili, tatu kuhusu masuala mengi yanayohusiana na Sheria ya Fedha na *alignment* ya malengo ya Serikali na bajeti iliyo somwa na Mheshimiwa Waziri na Serikali *ime-give in*

kwenye mambo mengi sana. Kwa hiyo, mimi tu binafsi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali katika maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kitu kimoja, Kanuni za Bunge siyo Msahafu wala Biblia, nitumie nafasi hii kuomba Ofisi ya Spika, dunia inabadilika, mazingira yanabadilika na Kanuni zetu zibadilike. Nimemsikiliza Ndugu yangu Silinde akionesha *challenge* za Kikanuni juu ya Muswada ulioletwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwenye *notice* hapa Waziri wa Fedha amesema *this Bill to be submitted to the National Assembly was published as a Bill Supplement No. 3, of 2nd June. Kwamba hii ni supplement ya ile Bill iliyokuwa imeletwa, why supplement?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaleta bajeti, Wabunge tunachangia siku saba, haina maana kwamba ndani ya siku saba Serikali isichukue mawazo yetu na mawazo yetu yanaathiri sheria, yanapoathiri sheria tuna *option* mbili, tukubaliane *model* ya kwamba Serikali ikija na bajeti hapa inakuwa ndiyo Msahafu tunafanya sisi tunakuwa *rubber stamp* ama mawazo yetu yanaenda kuwa *accommodated* na kuletwa kwenye Sheria ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kama kuna upungufu wa Kikanuni, ni wajibu wetu Wabunge ku-*demand* mabadiliko hayo, ili tuweze kufikia malengo na wajibu wa kufanya kazi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kwenye baadhi ya maeneo, moja ni eneo la *ku-regulate informal sector*. Tunawapa vitambulisho tunawa- *regulate* ma- MC na nani, ningombaa tutakapowa-*regulate* hawa *informal sector* kwa kuwa vyanzo vingi vya mapato tumevipeleka *Central Government through TRA*, nashauri, *TRA* ikae na Serikali za Mitaa na hapa ndipo Waziri wa Serikali za Mitaa afanye kazi *closely* na Wizara ya Fedha namna gani chanzo hiki kitaweza kuwa *regulated* katika *Local Government* ili baadhi ya mapato yabaki katika Serikali za Mitaa na baadhi ya mapato yaje ya-*support* Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya *Gaming Board*, *Gaming Board* ina vyanzo na vyanzo hivi nadhani Serikali iangalie, tumeshapitisha *Appropriation Bill* juzi tumefunga, lakini bado hatujawahi kuwa na asilimia 100 ya *ku-attain* bajeti yetu, ningomba tuongeze tozo inayoitwa *tax on collection* kutoka 6% to 12%, tuongeze tozo ya *tax on winning* kutoka 18% kwenda 25% kwenye *Gaming Board*, tuongeze *license fee*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hili ni eneo ambalo wanaita wenyewe, ni kodi za dhambi hatutaki kamali *i-grow* lakini *its growing is there, it is an opportunity*. Kwa hiyo, wakati mna-*loose morally* lazima *mgain economically*. Hivyo, ningeshauri vyanzo hivi vyat fedha vikusanywe na ikiwezekana *Central Government* na Hazina muangalie uwezekano wa kupeleka fedha hizi kwenye Mfuko wa Mazingira, *If it is possible* tupeleke fedha hizi kwenye Mfuko wa Mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna-*demand* maji, kuna fedha ile shilingi 40 na Serikali imetupa *commitment* ya kuhakikisha kwamba hela ya maji itaenda, *in a future ili maji yawepo lazima tu-protect mazingira*. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye *Income Tax Act*, kwenye hii *Bill* ilioletwa na Serikali *page number 14, item number two, section 27 item (b)* inasema *a corporation with a newly established plant for assembly motor vehicles* mpaka mwisho tumetoa *incentive* ya 10%. Naomba tuongeze *item (c) tuseme kwamba a corporation with a newly established on agro processing industries with the performance agreement with the Government will enjoy a 10% Corporate Tax for the period of five years*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu tuna-*grow industrialization*, Ukiangalia tumetoa *VAT exemption* kwenye *capital goods*, tusipotengeneza *structure* za kodi, kwa sababu Mwekezaji anapoingia kwenye nchi, jambo la muhimu analolitazama ni *tax regimes* kwanza. Najua kuna

*window ya TIC*, kuna window za EPZA na kadhalika, tukitengeneza *tax regimes* ambazo ziko wazi, wawekezaji wanaokuja kwenye sekta ya kilimo, leo ukimwambia mwekezaji wa korosho kwamba njoo u-process korosho yako Tanzania badala ya kui-process India, utapata VAT exemption kwenye *capital goods*, utapata 10% *corporate tax* badala ya 30%, utapata zero rated kwenye *chemical processing*, huyu mtu hatakuwa na sababu ya kwenda kuwekeza nje, pamoja na *incentive* tulizoziveka *TIC* na maeneo mengine ni rahisi sana kufanya namna hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maeneo ya *cotton*, ni vizuri hizi *incentive* zikawa *extended* kwenda kuwa-accommodate sehemu kubwa ya watu wetu. Kila siku tutakuja hapa tunasema asilimia Saba ya *GDP* uchumi wetu umekuwa kwa 7.5 hadi 7.8 kama *tax regimes* zetu hazi-attract *investment* ya viwanda kwenye eneo la killimo hatuwezi kufikia malengo tunayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nishauri kwenye *VAT exemption* ambayo tumetoa, ningombaa tuongeze kwenye *schedule Namba 21* tuweke *schedule Namba 22*, ili namba 22 tuongeze *chemical processing on agro industries*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba nawashukuru sana Serikali safari hii wame-give in kwenye mambo mengi. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie *Finance Bill* ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote niombe wale wanaotunza muda watutendee haki upande wa pili. Kumekuwa na tabia ya kukata muda, *last time* nilichangia

badala ya dakika 10 nilipewa dakika saba na nusu. Kwa hiyo, nami naona kabisa muda pale nimeanza ngapi, muache kutukata muda. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Muda huo unaouzungumza hayo uuhesabie pia, kwa sababu usihesabu saa hizi ukaanzia mahali ambapo umeweka wewe nukta, wakati umeanza kwanza na *preamble* ndefu kidogo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini na wa kwako pia utakuwa umehesabiwa utakuwa *deducted*. Nakubaliana na hoja yako lakini pia wa kwako *interaction* upunguze. (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Wewe endelea na mashindano, muda wako unazidi kwenda, hapa naruhusiwa kuongea na wewe, unaokatwa ni muda wa kwako wewe.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Nategemea kuchangia mambo matano. Mafuta ya taa, kodi ya majengo, ushuru wa hoteli, ushuru wa mazao na vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya haya, niseme machache ambayo yamejitokeza juzi. Kwa hali ya kawaida naamini Bunge letu linaongozwa kwa Kanuni pia, kura ya bajeti ni kura ya imani na iko wazi. Ninyi ni Serikali ni Chama mnachoongoza sisi ni Wapinzani tunaotegemea kuingia madarakani, hatuwezi tukaunga bajeti yenu, ni Kanuni ni wazi, hata keshokutwa ninyi mkawa upinzani mnaweza mkawa na mawazo yenu mbadala na msiunge ya kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilishangaa sana kwa mara ya kwanza, huu ni mwaka wangu wa sita au wa saba, haijawahi kutokea mwongozo mtu mmoja akiomba wanapewa watu wengine sita nyuma yake, *the same* mwongozo. Ndiyo maana ilitushangaza sana na bahati nzuri mlifanya zile siasa mkiwa mmeachia *television* wazi,

Watanzania wameona ubaguzi mnaoufanya wa wazi wazi. Hata kama mnakutana kwenye vikao vyenu vya *caucus* ni vizuri mkakumbuka *critical thinking and argumentation*, mmeletewa jambo lakini ni vizuri mkajiongeza, hivi kwa hali ya kawaida leo nchi nzima Miji mikubwa tunaongoza Wapinzani tukiamua kwa kauli zenu za ubaguzi ndugu zetu mlioko madarakani, tukaamua kukusanya zile kodi wenyewe, maendeleo tutashindwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya majengo mnayochukua ninyi, kodi ya mabango mnayochukua ninyi, kodi ya ardhi mnayochukua ninyi ambayo hamrudishi tutafanya maendeleo na wananchi wetu watapata barabara, watapata hospitali, watapata kila kitu. Mkajisahau, mkaona mfanye siasa za kibaguzi, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mnawaambia Watanzania kwamba mtakusanya kwenye miji yetu hamtoturudishia na *how if* sisi tukaenda kwa Watanzania tukawaambia msilipe kodi, maana ninyi ndiyo mmeanza na waliwaona. Leo ukiwaambia kwamba wasilipe kodi, kwanza mlishtawaambia kwa sababu mmesema hamtapeleka kwenye Majimbo ya Upinzani maana yake ni nini, mmewaambia wasilipe kodi. Ninyi ndiyo mnaleta matatizo kwenye Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfikirie ndiyo maana nikasema kwa wale ambao walisoma siasa; *critical thinking and argumentation, ways and methods of decision making*, maamuzi mliyofanya mmejichonganisha, mmejichora kwa Watanzania na ni aibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu mlishtaanza siku nydingi ndiyo maana hata hela za Mifuko ya Jimbo huku Wapinzani mmeanza kutukata, mmejiongezea ninyi. Mfuko wa Jimbo nikatolea mfano nikaombea mwongozo hapa, mmeshaanza iko wazi na hizi pesa mkianza kukusanya hamtotuletea, *we are ready* kwa hayo mnayotaka kuyafanya. Niwakumbushe tu, msifanye siasa za kitoto Watanzania

wanawaona, inatia uchungu, mnaligawa Taifa hili. Naomba hayo yatoshe na Mawaziri wala msiendelee kuyaongelea hapo ni aibu kwenu, mnaligawa Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mchangaji amesema Serikali ni sikuvi, eti ndiyo maana mkaleta sheria mkabadilisha badilisha sana, kwa sababu mmeaya-*accommodate* mawazo ya Wabunge, kama ndivyo hili la mafuta ya taa, limewashindaje? Hayo mafuta ya taa nani asiyejua kwamba *road/licence* haihusiani na mafuta ya taa? Hoja si ni kwamba Serikali ni sikuvi, mmeaya-*accommodate* mawazo ndiyo maana mkaleta yale marekebisho kwenye *Finance Bill*. Mafuta ya taa ndugu zenu wanawasha taa, vibatari, hakuna gari linalotumia mafuta ya taa, lipo? Mbona hili hamrekebishi kama Serikali ni sikuvi! Nawashauri tu kama ninyi ni wasikivu toeni hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii na *Finance Bill* hii maana yake kila Mtanzania atalipa kodi, wala msijifiche, maana yake ni nini? Hata yale ambayo mnasema mmefuta sijui *road licence, motor vehicle* mmehamisha hata kwa watu ambao hawana hayo magari. Kwa hiyo, hili la mafuta ya taa naomba nipate ufanuzi kama mlikuwa wasikivu kwa nini mpaka leo hamjafuta? Kwa hiyo, iondoke. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kuwatambua Wamachinga, MC, Mama Lishe, wauza mbogamboga, jamani! Lengo lenu ni jema kama mnavyosema, lakini siyo jema. Mmeshindwa tu kuandika mstari mmoja kwamba mnaenda kuwatoza kodi, hivi unawenza ukaniambia kwamba unataka kumtambua MC leo yuko kwenye *kitchen party*, kesho yuko kwenye harusi, kesho kutwa yuko kwenye msiba, kesho kutwa yuko kwenye ubarikio, eti unataka kumtambua! huyu *movement* yake unamtambuaje? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mama anayeuzwa mboga kichwani eti hata wauza mbogamboga hata aibu hamna mnaandika! Wengine, wanatembeza nyumba kwa nyumba unamtambuaje? Unampa kitambulisho ili iweje? Eti

wauza mitumba hawa, mnataka kuwatambua muwape vitambulisho kweli? Semeni mmeamua kupeleka kodi kwa hawa wafanyabiashara wadogowadogo, Mama Lishe watalipa, kwa nini mniamumunya, mbona liko wazi, andikeni pia tujue? Tukienda kuwaambia Watanzania hao mmeshajiharibia sana kwenye bajeti hii. (*Makofi*)

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul taarifa, Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Gekul kwamba, *identification ya informal sector* kote duniani, *best practice* kote, ni *process* ya kufanya kitu kinaitwa *incubation* kwenye *enterprise*. *Identification* ni suala la *incubation* kwenye mfumo wowote wa dunia wa kibiashara. *It has no relation with taxation, it has no relation na tax regimes.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosikitika tu, nina mwaka mmoja humu *I can see a lot of spinning and misleading zinaendelea ndani ya Bunge on both sides and this is wrong!*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimwambie *identificationya* Mama Lishe, *identificationya* Machinga kote, ukiangalia mfumo unaoitwa *black empowerment South Africa* wame-*identify* hadi *car wash*, wanaofanya *car wash* wako kwenye *proper database za Council*. Kwa hiyo, tusi-*mislead* vitu, kuna *issues* zipo mnajenga hoja za msingi, lakini siyo kila kitu tu-*mislead*. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.Mheshimiwa Pauline Gekul unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa imetumia dakika tatu, muda wangu uwe pale pale. Kwanza sina sababu ya kubishana naye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul leo una shida gani kwani, una shida gani? Wewe endelea kuchangia, Makatibu wapo hapa wanaangalia muda hajaongea kwa dakika tatu nami pia nilikuwa naangalia. Dakika tatu wewe saa yako inakimbia sana mbona. Naomba useme kama unapokea hiyo taarifa au hapana halafu uendelee na mchango wako.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa siipokei kwa sababu hata Waziri wakati ana-*wind up* alisema lengo la kuwatambua ni nini, kwamba baadaye wakawe walipa kodi, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge hakuwepo *Hansard* ipo itatafutwa, kama hakuwepo wakati ana-*wind up* tutatafuta *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kuwatambua mkawatambue, mkijua mmeshindwa kukusanya kodi kwenye makampuni ya madini, mnataka mkawalipishe hawa wanaotembeza mboga mboga, *it is ok* tutawaambia tu, tutakutana huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja nyingine ya ushuru wa hoteli. Mkanganyiko mwingine ni huu kwamba miaka sita niliyokuwa kwenye Bunge hili kulikuwa na mkanganyiko wa ushuru wa huduma kwa makampuni ya simu, mkasema mtakwenda kuyarekebisha, mtaangalia hilo mkashindwa, lakini hata huu ushuru wa hoteli, kulikuwa na mkanganyiko wa hoteli za *five stars* na hoteli zingine. Miaka mingi Halmashauri zikawa hazikusanyi, *this time* mmeleta tena mkanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tu Mheshimiwa Waziri aangalie na mwongozo utoke mapema ushuru huu wa hoteli unakusanywa kwa kiasi gani na Halmashauri zikusanye, kwa sababu mlivyoandika maana yake hata ukusanyaji wake ni mkanganyiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Halmashauri zetu mmeondoa vyanzo vingi, hata hivi vingine vinavyobaki muwe mnaondoa mkanganyiko, haisaidii, mnasema

isikusanywe, huku ikusanywe, sijui hoteli gani hampeleki mwongozo! Pelekeni mwongozo hili likae sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ushuru wa mazao, hili la ushuru wa mazao Mheshimiwa Waziri amesema kwamba tani moja imesamehewa mazao ya chakula, pia mmeshusha kwa asilimia mbili kutoka asilimia tano sasa ni asilimia tatu. Kimsingi Halmashauri zote zilikuwa zinakusanya asilimia tatu walikuwa hawajafika hata asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, toeni vitambulisho, kwa mfano Babati Mjini, wakulima wengi wanalima Babati Vijiji Galapo, lakini huu usumbufu siyo kwamba iwe ni tani moja, kama nimelima tani kumi ni mazao ya chakula yapitishwe kwa Halmashauri zote mbili, kukaa chini na kuwapa kitambulisho wakulima wanaotoka Halmashauri nyingine wanao-cross border. Hili la kusema iwe chini ya tani kumi haitosaidia wakulima wetu, kwa sababu pia kule wanakokodi mashamba wanakuwa wameshalipa fedha na wamechangia hiyo Halmashauri. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba wapatiwe vitambulisho sivyo ambavyo imekaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la kodi ya majengo, kuna watu wanasema kwamba Halmashauri za Wilaya ziko *excluded*, siyo kweli. Mmesema Miji Midogo, Miji Midogo iko kwenye Halmashauri za Wilaya! Mimi sijui uelewa wa watu ukoje? Hata huko wanasema nyumba ikiwa ya tofali na ya bati mtachaji. Kwa hiyo, Halmashauri za Wilaya zipo na huu mkanganyiko ulikuwepo hata juzi wakati mnahitimisha. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana muda wako umekwisha. Mheshimiwa Riziki Lulida tutamalizia na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, nimshukuru

pia Mwenyezi Mungu mwingej wa rehema kwa kunijalia nami kupata nafasi ya kuchangia katika hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya kwanza itaanzia katika uwindaji kutoa VATkwenye leseni za uwindaji. Nataka ku-*declare interest* ni Mwenyekiti wa kupambana na ujangili ndani ya Bunge, lakini kuondoa tozo ya leseni ya uwindaji kwangu mimi inanikwaza vibaya sana. Tunaangalia mbuga ya *Selous* sasa hivi hamna wanyama; wale *big five* tembo, simba, nyati, faru, chui wote wametoweke kwa asilimia zaidi ya 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri hawa wawindaji wanaokuja wengi ni *Professional Hunters* ambaao ni matajiri wakubwa sana, maana yake ni kuwa mnachangia wanyamapori kumalizika na kukandamiza uchumi wa utalii ambaao unachangia asilimia 17.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa sababu za msingi kwa nini nasema hii tozo irudishwe watozwe kama watu wengine. *TANAPA* wanatoa tozo kwa Serikali billioni 33, lakini hawa wawindaji wanatolewa tozo, *TANAPA* akijenga barabara analipa kodi, akipeleka maji katika maeneo mbalimbali mbugani analipa kodi. Leo tunashangaa hawa wawindaji ambaao wanamaliza wanyama, uchumi wa nchi utatoweke, wanaambiwa wasitoe tozo ya leseni ya uwindaji. Kwa kweli hatujawa *serious* kama kweli nchi hii tunataka kuingiza uchumi bora katika suala la sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia suala la mjisui muda mrefu lakini naona kama Serikali haiko *serious*, tunakimbizana na Mama Lishe, Ujerumanii peke yake inapata Euro milioni 600 kwa mwaka, lakini hata mrabaha wa kupeleka pale anapotoka mjisui Tendeguru hatupati, bado tunaona pana *silence*, mnakimbizana na wanaouza mboga za majani, na nini, vitu ambayo unaona kabisa haviko *sensible* kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia katika suala la uwekezaji, wawekezaji wa ndani tunasema tunataka

tuwahamashe, mimi pia ni Mwenyekiti wa kupambana na Malaria Tanzania, Tanzania *without malaria is possible*, lakini nishukuru *Patron* na Mwenyekiti wa Malaria ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Wao walipigania kuhakikisha panawekwa viwanda vyatengeneza vyandarua ambavyo vina-*quality* ambavyo vitawasaidia Watanzania kuweza kupambana na malaria, jambo la kushangaza tumejaribu kupigania humu ndani hakuna uwezekano.

Mheshimiwa Naibu Spika, A-Z ni Shirika ambalo linafadhiliwa na *Global Fund* pamoja na *USAID* walituita kwa ajili ya mkutano na humu ndani wemefanya semina, wanatoa *tax* ya bilioni 17.7, lakini utashangaa wanaleta vyandarua feki kutoka nje ya nchi, hasa kutoka China, vyandarua vile havina viwango, havina ubora, je, huyu atafanyaje kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *purchasing principals* ziko nne, *you have to buy the right quantity, with the right quality, with the right price, with the right time*. Leo unapoleta vyandarua vibovu kutoka nje mnafanya nini, je, mko tayari katika uwekezaji au mnataka kutubabaisha? Naomba majibu ya haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hawa wanaleta ajira wanaajiri Watanzania wananchi hasa akinamama 8,000, leo wanafunga kiwanda kile, nani atapata ajira pale Arusha? Hii ni hatari kwa Watanzania, uchumi wa nchi utaangamia kwa ajili ya kuangalia *viji-ten percent*, siwezi nikasema kama ni hivyo, lakini kwa nini Waziri anababaika kuzuia tozo kwa hawa wa nje wawe *zero* wa ndani wanalipa kodi hii haiingii akilini kabisa. Tufike mahali tujitambue, hawa washauri wanaoishauri Wizara wanafanya kazi gani kitaaluma kusaidia vitu kama hivyo ambavyo vinaleta kigugumizi katika uchumi wa nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie masuala ya uwekezaji hasa viwanda vyatengeneza maji, *juice*, tunaingiza maji kutoka nje kwa asilimia 61, hawa ndani tozo yake ni shilingi 58, jiulize asilimia tatu hii ni kiwango kidogo, je watakuwa tayari *ku-compete* na wale wa nje?

Hawa wa ndani wanafanyakazi, wana ajira, wamewekeza, mnaruhusu maji na sasa hivi tunaona tuna bidhaa feki hata maji, vyakula kutoka nje, michele, mafuta ya kula, lakini bado tunapiga kigugumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii iko katika *dilemma*, tunauza ufuta, nje tunapeleka ufuta nje, tunapeleka mbegu za pamba nje, tunapeleka mbegu za karanga nje, mbegu za alizeti nje, tunaletewa mafuta mabovu, nani wa kulaumiwa ni Watendaji. Inafika mahali unajuliza mafuta yanatoka nje tayari yameshaganda ni mafuta ya nini, ina maana ni mchanganyiko wa vitu vichafu wametuletea Tanzania, lakini wanasema tunaingiza mafuta, hivi ina maana kila kitu lazima uingize. Kuna vitu vingine havihitaji kuletwa Tanzania, tuna viwanda vimefungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi kuna kiwanda cha llulu kilikuwa kinatengeneza mafuta ya ufuta na karanga mmefunga. Kulikuwa na viwanda vyta pamba mmefunga, matokeo yake mnaagiza mafuta kutoka nje, kwa afya ya Mtanzania au mnataka katuongeza magonjwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, ningombaa hili eneo mfute kabisa kuleta mafuta kutoka nje ni hatari kwa maisha ya Watanzania inatuangamiza, kuleta maji kutoka nje vilevile inatuangamiza. Kama wao wanataka kuja Tanzania watumie *product* za Tanzania ambazo zimekaguliwa ziko katika viwango, kutuletea vitu vichafu kwetu ni hasara na inatumiza na ndiyo maana sasa hivi *cancerziko* juu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la maendeleo, miradi ya maendeleo Mkoa wa Lindi na Mtwara tuko nyuma. Miradi ya barabara Lindi na Mtwara ambapo korosho imeingizia pato la Taifa kwa asilimia kubwa sana ambayo haijapatikana katika mazao mengine yoyote, hakuna barabara ya kwenda Liwale, hakuna barabara ya kwenda Nachingwea, hakuna barabara ya kwenda Milola.

Je, tutafikaje katika uchumi bora ikiwa sisi kila siku tunapeleka uchumi bora wa mazao lakini tumewekwa nyuma Mkoa wa Lindi na Mtwara tuko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nisikatae bajeti hii kuwa haiwatendei haki watu wa Kusini, hivyo silazimiki na wala siwajibiki kusema ndiyo wakati naona kabisa kuwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kusema ndiyo kwa wachache ambaeo watanufaika, lakini kwa mimi nasema hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda niungane na wenzangu kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Miswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka 2017. Kwa kweli sikuhitajika nisimame nichangie kwa sababu Wizara ya Fedha imechukua karibu zaidi ya asilimia 80 mapendekezo ya Wabunge na ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa nimesimama kuweka sawa baadhi ya mambo ambayo yanaonekana yanapotoshwa kwa makusudi kwa misingi ya kujitafutia umaarufu wa kisiasa wa kiraishi rahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo nataka nilisemee ni kuhusu kupata Miswada miwili. Wakati nawasilisha hotuba yangu nilisema kwamba Miswada hii huu wa pili ni matokeo ya mchakato mzima wa majadiliano yaliyoanza kwenye Kamati za Kisikta, Kamati ya Bajeti na kupitia katika Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zilizoongezwa kwanza ni Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki. Sheria hii imependekezwa kupitia katika Kamati yangu, tukiomba suala la uuzaaji wa *share lisiishie* kwa Watanzania

peke yake, liende mpaka kwa watu wengine ili kuhakikisha kwamba tunavuta mitaji lakini tunachangamsha soko letu la mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili wakati tunatoa hayo mapendekezo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alikuwepo na yeye ni miongoni mwa waliochangia, sasa sjui kwamba wakati tulivyokuwa tunaiomba Serikali tulitaka watuambie kwamba walichukue mpaka mwakani? Nilitegemea kwamba tupongeze kwa Serikali kuchukua yale ambayo tumeyapendekeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, tumependekeza ndani ya Bunge. Sheria ya Usalama Kazini tumelalamika kwamba kumekuwa na suala la ukaguzi wa mara kwa mara ni kero, ni usumbufu. Kama Waziri amekuja na Muswada ambao vitu hivyo havimo, Wabunge tumeomba, Serikali imekubali, imeongeza hizo sheria, badala ya kushukuru Serikali tunasema tumeshtukizwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia...

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia kuna taarifa, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

## T A A R I F A

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nitoe taarifa kwamba kuwepo kwenye Kamati hakuzuii kutoa mawazo mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu wakati tunajadili haya mambo mpaka tunaafikiana alikuwa ni mtoro, akiingia, anatoka. Kwa hiyo, hawezи akajua tulifikiaje katika marekebisho hayo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba haya yaliyoletwa na Serikali kama ziada ni mapendekezo ya Kamati, ni mapendekezo ya Wajumbe, nami naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa kupokea mapendekezo ya Kamati na kuyafanya kazi na kuandika upya Muswada wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa wale wenzetu walipenda, kwamba yale tuliyomshauri Waziri wa Fedha asiyakubali illi waje walalamike kwamba Waziri huyu siyo msikivu. Sasa anakuwa msikivu wanalamika, sijui tuwekwe wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda nilichangie, sikuwa na sababu ya kuchangia kwa sababu bajeti ni nzuri. Suala la kusema kwamba tumeanza sera za ubaguzi ndani ya Bunge hili. Hakuna ubaguzi, tulichokiuiza na ambacho tunasimamia ni suala la kukaa zaidi ya miezi mitatu hapa tunajadili bajeti, tunatoa mapendekezo, Serikali inayachukua, halafu mtu anakuja anasema siungi mkono, au anasema hapana.

**MBUNGE FULANI:** Ni lazima?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na njia tatu, ulikuwa na uwezo wa kusema hapana, ulikuwa na uwezo wa kusema ndiyo na ulikuwa na kusema sina maamuzi. Huna maamuzi kwa sababu yapo uliyoyakubali na yapo ambayo hujayakubali. Hakuna aliyesema kwamba hana maamuzi, badala yake wamesema wanakataa, sasa kama bajeti umeikataa...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Naomba mtulie kama sindano imeingia si mtulie.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia kuna taarifa. Mheshimiwa Mussa.

## T A A R I F A

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka Msemaji anayesema aone hayo ni mambo ya kawaida kwenye siasa. Kwa sababu hata hao wanaosema ndiyo wanapongeza na kuunga mkono halafu mwisho mtu anasema shule yangu haina madawati, hospitali sina, barabara hakuna, kama ni kupongeza halafu wasilalamike waendelee kupongeza hata kama mtu ana matatizo aendelee kupongeza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa taarifa yangu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu napongeza pale napopongeza, nisipokubaliana na hilo ninatoa ushauri jinsi gani Serikali yangu ifanye na pale Serikali yangu inavyochukua ule ushauri wangu nilioutoa ndipo ninapokuja nasema naunga mkono Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wazima hivi au ile maana ya *abstain* watu hawakujua maana yake ndiyo maana hakuna hata mtu mmoja aliyesema *abstain*. Waswahili wanasema ukiligoroga lazima ulinywe, mmeikataa bajeti kwa hiyo madhara ya kukataa bajeti lazima yawafikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naona sindano zangu zimeingia vizuri sana na ndiyo maana watu wote sasa wanashindwa, wanagugumia kama ambavyo watoto wakichomwa sindano wanalia. Poleni sana mwakani mjifunze jinsi ya kuunga mkono bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi cha kwanza, tutaendelea jioni. Niyasome majina ya Wabunge wachache tutakaoanza nao mchana halafu nitatoa maelezo ya jambo moja liliojitekeza hapa.

Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Paschal Haonga, Mheshimiwa Raphael Michael na Mheshimiwa Abdallah Mtalea. Hao ndiyo tutakaoanza nao lakini majina yako hapa zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe ufanuzi wa jambo moja, maana naona linajitekeza mara kadhaa kuhusu maelezo ya ubaguzi. Jambo hili lilitokea juzi, jana limerudiwa tena, humu ndani na leo naona likirudiwa tena.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu ziko wazi namna ya uendeshaji wa Bunge humu ndani, ikiwa Kiti kimefanya maamuzi au kimefanya jambo ambalo huridhiki nalo Kanuni ya Tano (5) inakupa wewe utaratibu wa kufanya. Siyo jambo zuri kabisa, mtu aliyekuwa amekaa kwenye Kiti,

unatoa maelezo kuhusu mtu huyo akiwa si ye ye aliye kaa kwene ye Kiti na wakati Kanuni zina elekeza nini wewe cha kufanya.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tumezoea kufanya hivi na wengine pengine ni wavumilivu kidogo, wengine siyo wavumilivu, tunaona ni jambo la kawaida. Siyo utaratibu mzuri mtu anapokuwa amesimama hapa, ama amekalia Kiti, ye ye ndiye ana mamlaka kama hukukubaliana na alivyotumia mamlaka Kanuni ya tano (5) inakupa utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, tusitumie fursa ya kutaka kuonesha namna ambavyo mtu fulani akikaa, mtu mwingine akikaa, basi unataka kuleta hoja ambazo haziko sawa sawa. Kwa hiyo, hoja ya kuhusu ubaguzi, kama mtu anayo hoja hiyo, achukue Kanuni ya tano (5) alfanyie kazi, afuate utaratibu. Hatuwezi kuwa tunaendelea kuijadili hiyo hoja humu ndani kana kwamba haikuamuliwa wala haikuisha siku hiyo. Kwa hiyo, tusiilete kwa namna ambayo kila wakati tutakuwa tukirudi nyuma kwenda mbele. Kanuni ya tano (5) inaeleza utaratibu na naomba tufuate utaratibu huo tusianze kuijadili hiyo hoja hapa kwa namna ambavyo kila mtu anaona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, nitatoa mifano miwili maana mwingine anaweza akaona natoa maelezo gani. Ni hivi, pande zote mbili, hiyo siku ya juzi watu walismama zaidi ya mmoja, wakirudia jambo hilo moja. Kwa hiyo, siyo suala la kulaumu upande mmoja na mimi uzuri nilikuwepo kwa hivyo majina ninayo ya akina nani walizungumza. Mbunge mmoja tu na huyo nitamtaja jina kwa sababu ye ye alifanya jambo jema Mheshimiwa Aida Khenani ndiye pekee aliyesema jambo langu limeshazungumzwa, kwa hiyo sina haja ya kuzungumza. Wengine wote walirudia jambo hilo hilo pande zote mbili.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya kulisema kana kwamba upande mmoja labda ulikuwa unafanya vile, upande mwingine haufanyi. Siyo sawasawa, Kanuni zetu namba tano

(5) tuitumie, tusirudie jambo hili kulizungumza kana kwamba halikufanyiwa maamuzi. Naamini hapo tutakuwa tumeelewana tutaendelea na uchangiaji jioni, tuaanza na majina ambayo nimekwishayataja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa Kumi Jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wetu uwiano tuliokuwa nao kuanzia asubuhi tuna saa moja ya uchangiaji. Kwa hivyo tutapata Wabunge wawili kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Wabunge wanne kutoka Chama cha Mapinduzi, kwa upande wa Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa sababu alishachangia Mbunge mmoja na muda wetu uliobaki ni saa moja, muda wao utakuwa umemalizika.

Tuaanza na Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Pascal Haonga ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake nzima kwa bajeti nzuri pia kwa Sheria hii ya *Finance Bill* ambayo imekaa vizuri sana, tunawapongeza. Kwa niaba ya wakulima wote wa nchi hii, lakini pia kwa niaba ya huduma zingine zote za jamii, tunawapongeza. Najua hatukupata yote na huwezi kupata yote siku zote. Tunaomba mwendelee na moyo huo na naamini kwamba huko tunakotarajia tutafika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa ushauri. Kuna maeneo ambapo tungependa Wizara iendelee kuangalia. Pamoja na kuwa wametoa msamaha mwingu

sana kwenye sekta hii ya mbegu kwa Wizara mbalimbali ambapo haipo Wizara ya Fedha. Kwa mfano (*skills development levy*) kwenye sekta ya kilimo, masuala ya *OSHA*, masuala ya *fire, weights and measurements* na ushuru wa mazao. Ingawa sheria kuititia kilimo inasema ushuru wa mazao hautatozwa kwenye mbegu bado unaendelea kutozwa. Kwa hiyo ni mambo ya kiutawala. Naomba muiweke sawa ili watu wasiendelee kusumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulileta mabadiliko ya sheria kwenye *Gaming Act* ambapo tulipendekeza na tunaendelea kuomba kwamba badala ya *six percent* iwe *12 percent* na zile *three percent* kuwa *six percent* na ile *18 percent* kwenda *21 percent*. Zile fedha za nyongeza zote tulikuwa tunaomba ziende kwenye Mfuko wa Mazingira ambao hauna chanzo chochote cha mapato. Itaweza kusaidia Mfuko wa Mazingira kufanya kazi yake vizuri na mazingira ndiyo afya ya nchi yetu kwa sababu hali iliyoko huko ni mbaya na hii ni moja katika vyanzo ambavyo vingeweza kusaidia mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa *motor vehicle licence* kulipa kila mwaka, badala yake tutalipa mara moja wakati tunasajili, naona watu wengi bado tunaendelea kujichanganya. Hii ni Sheria ya *Traffics, Traffic Act – motor vehicle licence*. Tunachanganya Sheria ya *excise duty* ambapo ni sh. 40/= imeongezwa kwenye mafuta yoyote siyo kwa kufidia hii Sheria ya *Motor Vehicle Act*, hii ya leseni. Ile sh.40/= inaenda kwenye Mfuko wa Barabara, hao ambao tunawatetea kwamba mafuta ya taa yakipanda maisha yao yatakuwa magumu hivi hamhitaji wapate barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hiyo pesa ije Babati Vijijini na maeneo yote ya vijijini tunaomba hiyo pesa ije barabara zipone. Tungeomba Wakala wa Barabara Vijijini ingeanzishwa haraka ili iwe kama *TANROADS* sasa iwe ya vijijini ili suala hilo lifanyiwe kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kushukuru

kwamba kwenye suala la nyumba *property tax* imekaa vizuri kabisa. Pia tuendelee kukumbusha kwamba suala la wazee mlishaliondoa kuanzia mwaka jana, naona watu wengi wanachangia, suala la wazee wenye umri wa miaka zaidi ya 60 kama ilivyokuwa kwenye afya na maeneo mengine wameshasamehewa. Kwa hiyo, mzee kama ana nyumba tatu au nne, achague moja asamehewe zile zingine za biashara aendelee kulipa. Kila Mtanzania aliye kodi kwa kiwango chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu tunaomba Wizara iangalie kwamba mtu asije akaonewa, yule mdogo ukamtoza kubwa zaidi na yule mkubwa ukamsamehe. Tunachotaka ni pawe na uwiano wa kodi, kila Mtanzania mwenye uwezo aliye kodi, kidogo kidogo na njia hiyo ni kuondoka kwenye ile sekta isiyokuwa rasmi tuje kwenye sekta ambayo ni rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iendelee kufanya kazi namna ya kurasimisha sekta isiyo rasmi, kwa sababu vivutio vya kuondoka kwenye sekta isiyokuwa rasmi kuwa kwenye rasmi bado havijawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko tunakoelekea kwenye uchumi wa viwanda, naendelea kuomba kwamba Serikali iangalie, ije na mfumo wa kodi ambaa unaweza kukaa miaka mitano bila kugusa, ili watu wote ambaa wanataka kuwekeza wawe na uhakika kwamba siyo kila mwaka patakuwa na mabadiliko, kama mabadiliko basi yawe ni kupunguza siyo ya kuongeza. Kila Mtanzania akilipa kodi naamini mengi zaidi yanaweza kufanyika kutokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naendelea kuomba kwamba kwenye mfumo wetu Wizara iangalie, Serikali kwa ujumla iangalie pamoja na Bunge. Leo hii tunaanza kukimbizana kipindi hiki cha dakika ya mwisho, naomba bajeti hii ikishapita, tukishaanza Julai Mosi, basi ndiyo iwe mwanzo wa bajeti ijayo. Tuanze kukutana mapema, mipango yote, yale ambayo tunatarajia yapande, yashuke,

tuwe tumeponga kabla ya Oktoba ili Halmashauri zote, Serikali, na Idara zote wakati wanaenda kupanga bajeti zao tujue kabisa hii haitaruhusiwa kupangwa kwenye bajeti yao kwamba ni chanzo cha mapato na yale ambayo tumesema yaongezwe, wajue kabisa huku ndiyo watapata nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwapongeza *TRA* kwa kukusanya mapato yote. Naomba hata yale mengine ambayo bado hayako kwenye orodha ongezeni, mapato yote yawe *centralized*. Muhimu tujue, mimi kwenye Halmashauri yangu kama nilikuwa nimeweka wakala wa kukusanya mabango labda ilikuwa ya kwangu ndiyo maana nanung'unika, lakini kama hayo mabango utanirudishia hiyo pesa, nanung'unika nini? Kwa sababu *TRA* itakusanya badala ya huyo wakala ambaye ni *private* na hiyo pesa itakuwa inaratibiwa vizuri. Pesa zote hata hiyo ya *property tax*, mabango, kila Halmashauri ipeleke *bill* yake vizuri na nina uhakika Serikali italeta hizo pesa, muhimu ni kuangalia pesa zitumike vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa hilo na nina uhakika hizi pesa zitakuwa na matumizi mazuri. Wengi wamelalamika kwamba kwenye bajeti hii inaumiza wadogo, hakuna kuumiza mdogo. Hii bajeti itasaidia uchumi wa nchi hii na patakuwa na maendeleo, nina uhakika miradi ya maji, miradi ya umeme yote itafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi tunakushukuru kwamba kulikuwa na wengine wanassema suala la kuondoa pasiwe na tani moja, mtu ambae analima chakula apeleke kiasi chochote kutoka Wilaya moja kwenda nyingine. Naomba sisi kama viongozi ndiyo tuwe wa kwanza kulipa kodi, kwa sababu kama ni gunia kumi, hakuna familia inayokula zaidi ya gunia kumi kwa mwaka, hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Waziri na Mheshimiwa Rais kwa agizo hilo, nina uhakika, hiyo inatosha. Kwenye hayo mazao mengine, kila mmoja aliye kodi kwa sababu, kama unafanya kazi kwenye Wilaya ya mtu

mwingine hiyo Wilaya pia inataka i-survive, wewe kwako unapoona kwamba huhitaji, ile Wilaya nyingine inahitaji kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru lakini naendelea kuomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Haonga na Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017 ambao kimsingi ni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambazo zitawezesha sasa Bajeti Kuu ambayo tumeipitisha iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza kwa dhati Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti nzuri ambayo imepita kwa kishindo, kwa vyovyote vile haya marekebisho ambayo sasa yatasababisha bajeti hiyo itekelezeke, tutayapitisha kwa kishindo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukubaliana na mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ambayo sasa yanakwenda kupunguza ushuru wa mazao. Wabunge ambao Majimbo yetu eneo kubwa ni vijiji hii maana yake tunaifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Bukene asilimia 99 ni vijiji na shughuli kuu ya watu wangu ni kilimo, ili wawewe kunufaika na kilimo, sehemu ya mazao haya ni lazima wayauze. Kwa hiyo, ilikuwa ni kero kubwa wakulima wangu wanapokuwa wana gunia saba, nane au tisa wanapotaka kuzihamisha kutoka kwenye eneo la uzalishaji kupeleka kwenye eneo la soko walikuwa wakisumbuliwa na kero ya vizuizi nya ushuru huu. Sasa mapendekezo ya sheria hii yanakwenda kuondoa ushuru huu kwa mazao yote ambayo yatakuwa ni chini ya tani moja. Hili ni jambo ambalo nalikubali na litaondoa kero kwa wananchi wangu wengi wa Jimbo la Bukene amba ni wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii pia inapunguza ushuru wa mazao kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano mpaka asilimia tatu kwa mazao ya biashara na asilimia mbili kwa mazao ya chakula. Hapa ningeshauri tu tafsiri nzuri ipatikane kwa sababu kuna mazao mengine, kwa mfano, zao kama tumbaku au ambalo moja kwa moja linajulikana ni zao la biashara kwa sababu pamba huwezi kuila, lakini kuna mazao kwetu tunalima kule kama mpunga au mahindi ambayo ni mazao ya chakula lakini pia ni mazao ya biashara. Kwa hiyo sasa inapotokea kwa mfano mpunga ama mchele amba kwetu ni zao la biashara lakini mpunga/mchele huo ni zao la chakula. Kwa hiyo, tunataka tafsiri sahihi kwamba utatozwa asilimia ngapi kwa sababu uko kote, ni zao la biashara vilevile ni zao la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine ambayo nayaunga mkono ni hii sheria ambayo inakwenda kurekebisha Sheria ya Kodi ya Majengo. Hii inakwenda kuwa mkombozi hasa kwa wamiliki wa nyumba wote amba wana umri kuanzia miaka 60 na kuendelea. Tunajua miaka 60 watu wamestaafu hata kama siyo mfanyakazi kama ni mkulima nguvu zimekwisha, hana kipato, kwa hiyo kuna *logic* ya kumwondolea kodi ya majengo. Hivyo, suala hili la kuwaondolea, kuwasamehe kodi ya majengo wazee wote kuanzia miaka 60 naliunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu linakwenda kuwapa nafuu kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono pia sheria hii inakwenda kutoa tafsiri sahihi ya nyumba zipi zitozwe kodi ya majengo. Nimeona kwamba kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango ameainisha kwamba nyumba zote zilizojenga kwa miti, kwa tope zilizoezekwa kwa nyasi zote hizi zitaondolewa, hazitahusika na kulipa kodi ya majengo. Kwa hiyo, hii inadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujali watu ambao wana hali za maisha ya chini. Kwa hiyo, hili nalipongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kupata tafsiri kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, yale maeneo ambayo yanastahili kutozwa kodi ya majengo, yametajwa kwamba ni Majiji, Manispaa, Miji na Miji Midogo. Kuna Halmashauri, kwa mfano pale Wilaya ya Nzega tuna Halmashauri mbili. Kuna Halmashauri ya Mji wa Nzega ambayo inajumuisha pale Nzega Mjini, lakini kuna Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ambayo asilimia mia moja ni vijiji tupu hakuna Mji wala hakuna hata mamlaka ya Mji Mdogo. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ni vijiji tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tafsiri sahihi kwamba Halmashauri kama hii ya kwetu ya Nzega Vijijini ambayo asilimia moja ni vijiji tupu, je na yenewe inakuwemo katika kuondolewa kabisa kulipa kodi ya majengo kwa sababu haina hata kamji kamoja kalikofikia hadhi ya kuitwa Mamlaka ya Mji Mdogo, ni vijiji tupu, kwa hiyo tupate tafsiri kwa sababu *as we speak now* Halmashauri hii ya Nzega Vijijini watu wanatozwa, wanalipa kodi ya majengo wakati ni vijiji tupu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri tupate *clearance* nzuri ili tuweze kuwa na uelewa wa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine ambayo nayaunga mkono ni hii asilimia moja kwenye madini kama *clearance fee* ambako Serikali itaanzisha utaratibu wa kuweka maeneo maalum kwenye migodi, kwenye viwanja vya ndege ili madini yanayopatikana yaweze kuhakikiwa. Kwa hiyo wafanyabiashara ambao wana malengo ya kuyauza iwe ndani ya nchi au nje ya nchi, waweze kulipa asilimia moja ya thamani ya hayo madini. Hili litatuongezea

mapato ya kutosha ambayo kwa sasa hivi tulikuwa hatuyapati. Kwa hiyo naunga mkono hili kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naliunga mkono ni kuondoa ada ya kibali cha kufungua maduka ya madawa. Hapa naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa jitihada kubwa za kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua madawa. Hii ni dhamira tosha ya Serikali ya Awamu ya Tano kwamba inajali afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunafahamu kwamba juhudzi za Serikali lazima ziungwe mkono na sekta binafsi, hivyo pale ambapo watu wanajitokeza ili kuanzisha maduka ya madawa, ni mantiki na ni hoja sahihi kwamba waondolewe hii ada ya vibali iwarahisishie kufungua maduka ya madawa ili upatikanaji wa madawa kwa wananchi wetu uweze kuongezeka. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo naliunga mkono kwa sababu lengo lake ni kuimarisha afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naliunga mkono ni uamuzi wa kufanya marekebisho ya sheria ili kuondoa VAT kwenye magari ya wagonjwa. Hili ni jambo jema kwa sababu tunajua huko tuliko kwenye Majimbo vituo vya afya, hospitali za Wilaya, magari ya wagonjwa hayatoshi na tunahitaji tupate mengi zaidi lakini VAT ilikuwa moja ya kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu uamuzi wa kuondoa kodi hii ya VAT kwenye magari ya wagonjwa nauunga mkono kwa sababu ni uamuzi ambao unakwenda kuimarisha afya za Watanzania na kimsingi unakwenda kuokoa maisha ya Watanzania ambao wangeshindwa kuwashishwa kwenye huduma za afya, lakini sasa upatikanaji wa haya magari ya wagonjwa utawafanya waweze kufikishwa kwenye vituo vya afya ili waweze kupata huduma muhimu ambazo wanazihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema

kwamba, kimsingi marekebisho ya sheria hizi ambazo yatafanya sasa utekelezaji wa bajeti tulioipitisha uweze kufanyika, nayaunga mkono kwa asilimia mia moja, kwa sababu yamekaa vizuri, nina uhakika sasa tunakwenda kuwa na bajeti ambayo itatekelezeka na ambayo kwa kweli inakwenda kujibu kero za wananchi wetu ambazo tumekuwa tukizisemea ziku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimpongeze Waziri wa Fedha kwa safari hii kuleta bajeti ambayo ni sikivu, bajeti ambayo imezingatia maoni na ushauri kwa kiwango kikubwa sana ya Waheshimiwa Wabunge ambaao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiyatoa. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael, tutakaporudi upande wa CCM tuaanza na Mheshimiwa Josephat Kandege ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niweze kuchangia Muswada huu. Awali ya yote naomba niseme kwamba kumetokea sintofahamu tangu siku ya kuitisha bajeti hadi leo, jana nimesikia baadhi ya Manaibu Waziri wakiwa wanajibu maswali ya Wabunge wanasema kwamba "wewe unauliza swali na wewe, au unahitaji mradi fulani kwako? Kwa sababu ulikataa kuitisha bajeti hatutakuletea." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lile onyo ambalo ulilitoa nadhani unavyoahirisha Bunge mchana nadhani pia ungewapelekea baadhi ya Manaibu Waziri pia maana inawahuusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupeleka maendeleo kwenye Jimbo fulani hivi sio hisani. Kupeleka maendeleo

kwenye Jimbo ni lazima, kodi zinalipwa wananchi wa Majimbo husika wanalipa kodi lazima wapelekewe huduma. Mwananchi anapokuwa ananunua sabuni, anapokuwa ananunua nguo, anapokuwa ananua bidhaa mbalimbali analipa kodi. Anapolipa kodi anategemea kodi hiyo iweze kurudi kutengeneza barabara, kodi hiyo iweze kuleta dawa hospitali, kodi hiyo iweze kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ili mambo haya yaweze kwenda vizuri ili siku nyingine basi hizi kura tatu hii kura ya ndiyo, hapana na *abstain* ondoeni zote basi ibaki ya ndiyo ili muweze kwenda vizuri kama mnadhani kwamba itasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upotoshaji huu tukiuruhusu ukaendelea, naamini kwamba kama alivyoongea Mheshimiwa Silinde tutakuwa tunaligawa Taifa, hatuwezi kufika popote pale tutaligawa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya kuzungumza hayo wako baadhi ya Mawaziri au Manaibu Waziri kwa mfano, yuko ndugu yangu hapa Naibu Waziri kutoka kule Katavi, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji unapotoka hapa unaenda Katavi lazima upitie kwangu pale Mlowo, kama utapitia Mlowo pale kwangu maana yake mkisema kama hayo yanayozungumzwa kwamba hayatafanywa kwenye Majimbo yetu, maana yake na wewe Naibu Waziri tukuzuie usipite pale kwa sababu hiyo barabara hawatumii wa Mbozi tu, wanatumia hata ninyi Mawaziri mnapopita maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee marekebisho katika...

## **TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kuna taarifa. Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ni kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliongoza nchi hii kwa kura nydingi kutokana na kura ambazo zimetoka katika Jimbo langu na sasa hii sera ya kusema tu tumesema waliosema hapana wasipewe maendeleo, basi mniamuumiza Mheshimiwa Magufuli ambaye alichaguliwa na kura nydingi na watu wa CCM kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kabla sijakuuliza kama unaipokea hiyo taarifa ama huipokei, nadhani umeanza vema kwa kusema kwamba nilishatoa maelezo kabla hatujasitisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tufuate huo utaratibu. Kama kuna jambo liliifanyika humu ndani kuna Mbunge hakubaliani nalo afuate Kanuni zetu zinavyosema ili tusijikute kwamba tunajadili jambo lilishafungwa humu ndani twende kwenye hatua nydingine.

Mheshimiwa Haonga unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Bungara?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya ndugu yangu hapa naipokea kwa mikono yote kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sidhani kama amewatuma hao watu kuzungumza hayo maneno kwamba hawatapeleka bajeti huko, kwa sababu alichaguliwa na wananchi wa maeneo mbalimbali, hata kama kuna maeneo mengine kura hazikutosha, lakini walimchagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba niende sasa katika maeneo mengine kuhusu marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa mabango na

kodi ya majengo kuchukuliwa na Serikali Kuu huku ni kwenda kuziua Halmashauri zetu. Tunaenda leo kukusanya ushuru wa majengo, tunaenda kukusanya ushuru wa mabango, leo Halmashauri zetu zitakufa kwa sababu hivi ndivyo vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri zetu hapa nchini. Sasa kama leo tunakusanya ushuru huu Serikali Kuu inaenda kuhodhi, Halmashauri zetu kwa kweli zitakuwa katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakapokuwa anahitimisha Waziri wa Fedha naomba haya mambo ujaribu kuyaangalia, leo tupo hapa ndani wako wachache amba wao wenyewe jambo likizungumzwa hata kama ni baya kwa wananchi wanapiga makofi, kesho litakapokuwa limeharibika hao hao wanakuruka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tafadhali akili za kuambiwa changanya na za kwako, kama ni wataalam wako walikupotosha tafadhali katika hili jaribu kurekebisha, kwa sababu leo huwezi ukaenda kupora vile vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri zetu, kwa sababu ndivyo tunavyovitegemea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba pia nizungumzie suala la kuwatambua wafanyabiashara wadogo, kuna jambo moja mmelizungumza hapa na kuna mtu mmoja hapa alikuwa anasema hapana, eti Machinga hawatalipa kodi, mnapotosha. Naomba hii hotuba ya Waziri msome ukurasa ule wa 47 inawezekana kuna wengine hawasomi . Ukurasa ule wa 47 unasema naomba nisome kidogo kwamba:

*"Hatua za mapato na maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali, hatua za kisera na kiutawala."*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale kwenye hatua za kisera na kiutawala wameweka baadhi ya mambo pale kwa mfano jambo mojawapo ni kwamba kukusanya kodi kwa kutumia *machine* zetu (*electronic machine*) lakini ukisoma kipengele cha nne kinasema kwamba:

*"Kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi."*

Mfano, Mama Lishe, wauzaji mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mbogamboga, ndizi, matunda na na kadhalika, kwa kuwapatia vitambulisho maalum kwa kazi wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa tunazungumza haya mambo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha aweze kulitolea maelezo vizuri, huu ni uwongo mchana kweupe, mnataka hawa wafanyabiashara mkishawatambua ili muweze kuanza kuwatoza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mbunge mmoja wa Mwanza alikuwa analalamika, anasema kwamba Machinga wanafukuzwa na Rais akaagiza kwamba Machinga wasionewe popote pale wala wasifukuzwe, leo mnasema Machinga wasifukuzwe, mnataka muanze kuwatoza kodi. Hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu ambalo lina rasilimali za kila aina, Taifa ambalo lina madini, lina *Tanzanite*, lina dhahabu, lina gesi, lina kila kitu, kwenda kukimbizana na ushuru wa Mama Lishe.....

**MHE. SEIF KHAMIS S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kuna taarifa. Mheshimiwa Gulamali.

## **TAARIFA**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji kwamba, ili nchi iweze kuendeshwa ni lazima tutoe kodi. Hivyo basi, hata kama ni mfanyabiashara mdogo na alivyokuwa anazungumza mzungumzaji nakumbuka. Siku hiyo Mbunge wa Mwanza alisema tuwape vipaumbele hawa Machinga,

tuwape maeneo ili iwe rahisi kulipa ushuru wa Halmashauri ya Jiji. Hivyo, usipotoshe nchi inaongozwa kwa kodi, usieleze tofauti na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.(*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyu bwana nadhani inawezekana kabisa kwamba hayuko makini na taarifa yake naomba sasa rasmi niikate kwa sababu kuna vitu ambavyo nadhani havielewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokizungumza hapa ni kwamba, unapoenda kuwatoza wa machinga kodi, unapoenda kuwatoza mama lishe kodii, leo tuna madini; dhahabu, *Tanzanite* na juzi mmesema kuna triliioni 108, mnataka kudai hizo ndiyo sasa ziongezwe kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme badala ya kuwatoza hawa Mama Lishe, kuwatoza hawa wauza mboga mboga na matunda nendeni mkawatoze wale wanaochimba madini katika nchi yetu, wanaotorosha madini, nendeni mkawatoze wawekezaji wakubwa kwenye vitalu vya uwindaji, nendeni mkawatoze wale wakubwa ambaa wamewekeza kwenye miradi mikubwa mikubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kama Chama cha Mapinduzi kimechoka kutawala nchi hii na mnataka 2020 muambulie zero, nendeni kwenye hili ambalo mnataka kulianzisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuhakikishia kabisa Mheshimiwa Waziri kwa sababu najua na wewe pia inawezekana ni mgombea mwenzangu kwa sababu nimesikia juzi unawapongeza wananchi wa Jimbo la Buhigwe, unasema unawashukuru wananchi wa Buhigwe wakati wewe ulichaguliwa na Rais, wale wananchi unakutana nao maeneo gani mpaka unaenda kuwapongeza? Kwa hiyo, inawezekana ukawa ni mgombea

na wewe kama ulivyokuwa wagombea wengine, sikukatazi wewe nenda, lakini wale wananchi kule utakachokutana nacho utakutana na wamachinga hao hao ambao umewatoza kodi, utakutana na mama lishe, utakutana na wauza mboga mboga, ndiyo wapiga kura wetu kule.

Naomba kwenye hili kama Serikali haitachukua hatua Mheshimiwa Waziri imekula kwako, hii na nina amini kabisa usifanye mchezo Jimbo si mchezo, na nina amini lakini Obama yupo makini sidhani kama ataruhusu hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye jambo lingine, yuko Mbunge mwenzetu humu ndani amezungumza jambo, amesema mimi nilidhani kumbe hizi kodi zitakusanywa kwenye Majiji, sijui kwenye Miji, kwenye Halmashauri haihusiki, amedanganya na kama hajadanganya basi hakuelewa vizuri, kwa sababu..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga muda wako umekwisha, Waheshimiwa Wabunge sasa nafasi inaenda kwa Mheshimiwa Japhary Michael, tutakaporudi upande wa CCM wachangiaji watachangia kwa dakika tano tano, Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa muda huu wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nianze kwenye suala la vyanzo vyatia mapato ambavyo vimeondolewa katika Halmashauri zetu. Dhana ya *decentralization* ilikuwepo kwa sababu ya kutaka kuipunguzia Serikali majukumu. Bahati nzuri nchi yetu imepita katika hatua mbalimbali mpaka kufikia hatua za sasa ya ugatuaji wa madaraka kwa maana ya *decentralization by devolution (d by d)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua ni kitu gani kinaifanya Serikali Kuu ipate raha ya kukimbizana na mapato madogo ya kawaida ikiyaacha mapato makubwa ambayo hata Mheshimiwa Rais ameyaona yanayopotea, ambapo wangeweza wakapata fedha lakini wakimbizane na mapato madogo kama *property tax* na *bill boards* (mapato ya matangazo).

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa Serikali Kuu ya Awamu ya Tano utazidhoofisha mno Halmashauri hata kama tungejitetea kwa kiwango gani, kwa kiwango chochote tunachojitetea, utaratibu huu utazidhoofisha sana Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa sababu sasa tunajadili sheria; na kwa sababu tayari bajeti imeshapita, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa ukweli kabisa, kwamba ni kiasi gani atazirejeshea Halmashauri baada ya *TRA* kukusanya. Kiwango hicho kitamkwe kwenye sheria, kwamba ni kiwango gani kitarejeshwa Halmashauri baada ya fedha hizo kukusanya. Mwaka 2003 Mheshimiwa Mramba aliondoa kodi zilizokuwa zinaitwa kodi zenye matatizo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Lukuvi aache Mheshimiwa Waziri anisikilize, halafu watajadili mambo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary yupo Naibu Waziri anakusikiliza.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, nimekuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukzungumza hapa ni kwamba ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba lazima kwenye sheria itamke bayana ni kiwango gani kinachorejeshwa katika Halmashauri zetu baada ya kukusanya, ndiyo hoja yangu ya msingi. Kwa sababu mwaka 2003 Mheshimiwa Mramba alipokuwa Waziri wa

Fedha kuna vyanzo viliondolewa hapa na tukaambiwa tutarejesha katika Halmashauri lakini mpaka leo Halmashauri hasa za mijini hazipati hata shilingi moja...

## **TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nimpe taarifa Mheshimiwa Japhary na nimkumbushe kwamba huu ni mpango thabiti kabisa wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wa kuondoa *property tax* kwa sababu Majiji yote, Miji Midogo na Miji nchini imechukuliwa na Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, waliona kabisa kwamba tunaweza tukafanya maendeleo makubwa na CCM wamechukua zaidi vijijini, wameona afadhalii zile fedha kwa mtindo ullokuwa unafanyika huko nyuma wakati wanaongoza wao waziondoe wahakikishe kwamba zile fedha zinagawanywa.

Naomba sana uwakumbushe tu kwamba ziko kazi ambazo Halmashauri zinafanya, kazi ya kwanza ambayo inafanya Halmashauri ni pamoa na kuajiri wale wafanyakazi wachache ndani ya Halmashauri, lakini bado pia kuna asilimia 10, uikumbushe Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, nadhani atakuwa amekuelewa, lakini umesema Majiji yote yamechukuliwa na CHADEMA, sijui hiyo taarifa ataipokea vipi, Majiji yote yamechukuliwa na Chadema. Mheshimiwa Japhary unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake nimeipokea kwamba kwa mara ya kwanza Majiji yaliyo mengi yamechukuliwa na UKAWA. Inawezekana sitaki kuizungumzia Serikali kwamba ina hiyo ni *bad intention*, inawezekana kuna *intention* mbaya ya kudhoofisha Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijirejeshe kwenye hoja kwamba niamini Serikali ina nia njema, kama ina nia

njema niamini kwamba wanapaswa kutusikiliza tunachoshauri na ushauri wangu kwa Waziri ni kwamba inawezekana kwa mtazamo wa Serikali hii na mtazamo wa Waziri wanadhanu *TRA* ina uwezo wa kukusanya kuliko Halmashauri zilivyokuwa zinakusanya, jambo ambalo siyo kweli kwangu mimi ninavyoamini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni hivyo na kwa sababu tayari tumeshapitisha sheria, ninachoomba Mheshimiwa Waziri atuoneshe tu kwa kiwango gani *minimum* ambacho kitarejeshwa katika Halmashauri zetu baada ya kukusanya. Tuna kodi ya *retention* ya ardhi ya asilimia 30 mpaka leo ni ugomvi hairudi katika Halmashauri zetu. Nilikuwa nakusanya shilingi milioni 700 ya *property tax* katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, wamerudisha shilingi milioni 163 tangu wameanza kukusanya wao! Najiuliza shillingi milioni 500 niliyokuwa nakusanya kwenye *bill board* itarudishwa kwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana naomba Mheshimiwa Waziri kwenye mabadiliko ya sheria anasema, hiyo hela itaenda Hazina na atarejesha kwa kiwango kile kulingana na bajeti ya Halmashauri. Namshauri Waziri atamke kwamba ni kwa *percentage* gani *minimum* ambacho lazima Serikali ikirejeshe Halmashauri na kwa wakati, huo ni ushauri wangu wa kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, sifa moja kubwa ya kodi ni watu kuridhia kodi kulipa (*tax compliance*), sasa leo tunapokuja kwenye Bunge tukaambiwa kwamba kuna watu watakaolipa kodi lakini hawapaswi kupelekewa maendeleo tunahamasisha wananchi wasilipe kodi na lazima Serikali ikubali kwamba imeteleza. Haiwezekani watu walipe kodi halafu muwaambie hamuwaapelekei maendeleo kwa sababu ya mfumo wa kisiasa mliokubaliana nao Kikatiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imekubali mfumo wa Vyama vingi vya Siasa yenyewe tena katika Bunge la Chama kimoja cha siasa, mkajitengenezea Kanuni zenu

wenyewe kwamba tupige kura za ndiyo, hapana na *abstain*. Sasa leo watu wakifanya uamuzi huo wa kidemokrasia ndani ya Bunge mnawaadhibu vipi walipa kodi? Kama mnaamua kwamba hamuwezi kupelekeea wananchi maendeleo kuanzia leo, muwatangazie kwamba wale ambao hawapelekewi maendeleo wananchi milioni sita waliochagua *Opposition* wasilipe kodi! Nadhani ingekuwa imekaa vizuri, vinginevyo mnalipasua Taifa la Tanzania na hatuwezi kukubaliana na jambo kama hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sheria zinazohusiana na makosa yanayofanywa kulingana na Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa, mapendekezo ya Serikali ni kwamba adhabu ziongezwe kutoka 200,000 mpaka 1,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaofanya makosa ya kutema mate kule Manispaa ya Moshi ni wananchi maskini. Moshi mtu akitema mate chini anatozwa 50,000, leo kwa sheria hii tunayopitisha hapa atatozwa 200,000 mpaka 1,000,000. Sh.50,000/= walikuwa hawawezi kulipa, leo mnataka wakalipe sh.200,000/= mpaka Sh. 1,000,000/=, watatoa wapi hizo fedha? Kwa nini tunatunga sheria za kuwaumiza Watanzania wetu, hivi tungeongeza tu ikawa hata Sh.100,000/=, tungepata shida gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Waziri, hii sheria faini zibaki sh.100,000/= mpaka sh.200,000/= kulingana na aina ya makosa na kifungo kisizidi mwaka mmoja, lakini kusema mtu afungwe miaka miwili au kwa pamoja vyote aliipe na faini ya sh.200,000/= mpaka sh.1,000,000/= ni kwenda kuwaletaa matatizo wananchi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kwamba kodi ya majengo ioneshwe wazi katika sheria kwamba pamoja na kusamehe nyumba za tope, nyumba za tembe na nyumba zingine za majani, pia wajane na yatima watakaokuwa wameachiwa nyumba wapate msamaha kuititia kwenye sheria. Kuititia kwenye sheria yenye we itamke kabisa kwamba wajane na yatima watasamehewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wa zaidi ya miaka 60 tayari sheria ya mwanzo ilikuwa inawatamka siyo jambo jipya kwa Serikali hii, isije ikaonekana kwamba Serikali hii imeanzisha jambo jipya, tangu sheria ya mwanzo ya *Urban Authorities Rating Act, No. 289* ilikuwa inatambua kwamba Wazee wote wanaoishi katika nyumba zao, wenyе zaidi ya miaka 60 walikuwa hawapaswi kulipa kodi ya *property tax*. Sasa hivi tuongeze Wajane na Yatima na Watu wenye Ulemavu. Sizungumzii wagane kwa sababu wagane najua wengine wana uwezo hata wakipata hiyo shida. Nazungumzia wajane, yatima na Watu wenye Ulemavu. Naomba sana hoja hiyo iingizwe kwenye marekebisho ya Sheria ya Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona muda wangu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia na naunga mkono mawazo yote ya Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Kandege dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo dakika tano, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata nafasi jioni ya leo ili niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi leo dakika tano ni nyingi, kwa sababu karibu yote ambayo tulichangia kama Kamati ya Bajeti Serikali imezingatia naipongeza sana. Ni

vizuri tukakumbushana kwa sababu inawezekana wengine ni wapya kidogo, pia ni vizuri hata ukarejea msingi mpaka tunafika hapa hali ilikuwaje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika vyanzo vya mapato kwa maana ya vile vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi, vyanzo visivyo vya kodi vimekuwa vikikusanya kwa kiasi kidogo sana na Wabunge tumekuwa tukilalamika kwamba chanzo hiki hakifanyi vizuri, ndiyo maana tutakubaliana kwamba namna nzuri ni kuhakikisha kwamba *TRA* inaenda kukusanya pamoja na hiyo *property tax* ili tuje tuwapime katika *performance*. Kwa hiyo, nia ni njema naomba wenzetu siyo vizuri kupotosha katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niboreshe baadhi ya maeneo machache sana, ukianzia na nia njema ambayo unaiona Serikalini kwamba inavutia uwekezaji wa ndani ni jambo jema, lakini naomba niboreshe kuhusiana na suala zima la mazao ambayo yanazalishwa nchini na yakatumika nchini ili kuongeza thamani kuwe na tofauti katika ushuru ambao unatozwa ukilinganisha na mazao ambayo yanatoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivyo nalenga bia ambayo inazalishwa kwa kutumia *barley* ambayo inalimwa Tanzania, kimea kikatengenezwa Tanzania, kuwe na tofauti na ile *barley* ambayo inazalishwa kutoka nchi za nje ikaleta Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? ukiongea na *TBL* wana nia njema kabisa ya kuhakikisha kwamba wanafanya *expansion* katika uzalishaji na wana nia ya kuanzisha kiwanda kipyaa pale Iringa na tayari wameshafanya utafiti kwa kuwahusisha wananchi wa Njombe, Mbeya pamoja na Iringa na wameshafanya *test* kuonesha jinsi ambavyo udongo ule unaweza ukalima *barley* tukaacha kuagiza kutoka nje, tukazalisha hapa nchini, tukaongeza ajira kwa watu wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachoomba siyo kikubwa wanasema tunataka kuwe na tofauti ili tuvutiwe kuzalisha ndani, tukaongeza ajira kuwe na tofauti na kile ambacho kinaagizwa kutoka nje. Ukituwa katika hotuba pamoja na Muswada ambao Mheshimiwa Waziri ameleta hii hali njema tunaiona jinsi ambavyo zabibu ambayo itatumika kusindika mvinyo ambao unazalishwa Dodoma, *treatment* yake na ule mvinyo ambao unazalishwa kwa kuagizwa kutoka nje kuna tofauti. Kwa hiyo, Serikali wakalitazame waone namna ambavyo tutaweza kuwasaidia wananchi wetu wakazalisha *barleywakaongeza* ajira na kuongeza kipato kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuboresha kidogo ni kuhusiana na uwekezaji jinsi ambavyo tunavutia, ni jambo jema. Viwanda vinajengwa vingi, lakini hebu tuulizane, viwanda vingi vinajengwa wapi na kwa nini vinajengwa maeneo fulani? Itakuwa vizuri Mheshimiwa Waziri wakati anafikiria katika siku za usoni, kuwe na kivutio maalum ili Mwekezaji ambaye alitaka ajenge kiwanda Dar es Salaam aseme badala ya kujenga Dar es Salaam naenda kujenga Kigoma kwa sababu kuna kivutio A, B, C, D. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo itasaidia badala ya viwanda kurundikana maeneo fulani, ni vizuri tukawa na maendeleo kwa Mikoa yote, ili vijana wetu wasije wakalazimika kukimbilia baadhi tu ya maeneo kwa sababu wawekezaji *wana-concentrate* eneo ambalo tayari miundombinu ipo. Kwa hiyo, namna pekee ya kuweza kuvutia ni kuhakikisha kwamba maeneo ambayo hayajaendelea na hayana vivutio vingine, basi vivutio vyatia kodi ndivyo ambavyo vinaweza vikawasukuma hawa Wawekezaji wakaenda kufungua viwanda katka maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na asilimia 15 ya *industrial sugar* na hasa ambayo mara nydingi inatumika katika kuzalisha vinywaji baridi. Nia ya Serikali ni njema ya kuhakikisha kwamba hakuna *abuse*, kwamba sukari

ambayo nia yake ni kutumika kwa ajili ya kuzalisha vinywaji baridi isije ikaingia mitaani ikauzwa kama sukari ya kawaida... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Richard Mbogo dakika tano, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza naomba nimpongeze Waziri na timu yake kwa namna ambavyo wameweza kuleta mabadiliko ya sheria mbalimbali kutokana na maoni ya wadau pamoja na Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kulisema ni kuhusu hizi tozo zilivyoshushwa na baadhi ya vyanzo vyatoto mapato kutoka kwenye Halmashauri ambayo yatakusanya na *TRA*. Naomba niwakumbushe Wabunge wenzangu kinachofanywa na Serikali siyo kwamba ni kwa nia mbaya, siyo kwamba ni kwa nia ya kisiasa. Halmashauri haziendeshwi kwa asilimia mia moja na mapato ya ndani. Kuna fedha zinazotoka za Mfuko wa *Local Government Capital Development Grants*, hizi mbona mnapokea halafu hamzilalamikii? Kwa hiyo, naomba mlizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ni kwamba, namwomba Mheshimiwa Waziri utoke tu waraka ambao utamwelekeza Katibu Tawala wa Mkoa kuhusiana na halmashauri zilete maombi na jinsi gani zilivyoathirika kutokana na haya mabadiliko.

Mheshimiwa Nabu Spika, mfano mzuri kwenye Halmashauri ya Nsimbo kutokana na mabadiliko ya hii sheria, tozo kutoka asilimia tano kwenda tatu upande wa tumbaku

kwenye bajeti hii tulikuwa na milioni 440 kwa kupunguza hii itapungua kwa milioni 176. Wakati huo hiyo milioni 440 tulishaipangia kuongeza zahanati moja, kituo cha afya kimoja, kujenga sekondari na kuboresha miundombinu ya maji, kwa hiyo tunaenda kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Fedha nafikiri wa-revise tupandishiwe zile *Capital Development Grants*ili tuweze kutimiza yale ambayo tulikuwa tumejiwekea kwenye bajeti, nitashukuru sana. Pia mazingira yanatofautiana kuhusu hii tani moja, tutaomba baada ya mwaka mmoja tukupe mrejesho kwamba kutohana na tani moja kushuka chini hakuna tozo, mazingira yanatofautina. Sisi tuna wale *petty trader's* ambaao mtu anabebea kwenye baiskeli, kwenye punda, kwa hiyo ndiyo wengi ambaao walikuwa wanatupa vipato. Kwa hiyo, tutampa mrejesho Mheshimiwa Waziri baada ya mwaka mmoja tumeathirika kiasi gani, halafu wataangalia namna gani ya ku-revise. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwenye upande wa mbegu zinazozalishwa ndani, tunaomba tena waziangalie kwenye mabadiliko ya tozo na sheria mbalimbali za kodi ili na wao waweze kunyanyuka na wananchi ambaao ni wakulima wengi waweze kupata mbegu kwa bei ambazo ni nafuu, kama sekta ya elimu ambavyo wameiona kwenye *SDL, OSHA* na mambo ya *fire* basi na uzalishaji wa mbegu nao waweze kuwaangalia. Pia kwenye mifugo na kwenye waweze kuangalia mambo ya chanjo na vifaa na dawa waweze kupunguziwa upande wa kodi na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu machinga, rafiki yangu Mheshimiwa Haonga, nimemshangaa kuona anasema kwamba machinga wasilipe kodi. Nimpe tu taarifa akienda Kariakoo sasa hivi watu wa maduka pale ndani hawauzi, wanaouza pale nje ni Machinga ambaao wamezagaa. Sasa tunasema na kila mtu anayepata kipato inatakiwa ali pe kodi. Ndiyo maana Serikali imesema wanarasimisha watapewa na vitambulisho. Kwa mfano, ye ye anakatwa *pay as you earn*

lakini mkulima hana hiyo *pay as you earn* kwa hiyo atalipa kodi ya aina nyingine, hii yote ni katika kuchangia Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Machinga ningombwa Waziri kama itakufaa aangalie ile *penalty* kwa mtu ambaye atakuwa amekiuka ya Sh. 200,000/= mpaka Sh. 1,000,000/= au kifungo cha mwaka na kisizidi miaka miwili. Naomba tuiweke kulingana na mtaji mtu alionao, kuna Machinga wengine wana mtaji wa Sh.200,000/=, wengine mtaji wa Sh.100,000/=. Kwa hiyo, nafikiri hizi *penalty* tungeziweka kutokana na *category* ya mtaji ili isiumumize. Utaenda kumchaji mtu *penalty* ya Sh.1,000,000/= wakati mtaji wake ni Sh.200,000/=, matokeo yake ataenda tu gerezani, hivyo, tutaongeza gharama ya wafungwa huko kwenye magereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni *declaration*, mtu anavyofanya *wrong declaration* kwenye *ku-forge* hizi *invoice* hasa kwenye *importation*, tozo imepandishwa toka dola 10,000 mpaka 20,000. Inawezekana mtu akawa na mzigo mkubwa. Kwa hiyo, ningombwa iwe *minimum* dola 10, 000 na nyingine iwe kwa *percentage*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami kwa dakika tano nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mpango, Naibu wake na Watendaji kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Hawa Ghasia nilipata nafasi kushiriki katika Kamati, kwa hiyo, nita-*summarize* tu. Nampongeza Waziri kwamba mambo mengi ambayo tulikuwa tunazungumza ameshayafanya *amendment*, tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali ya Awamu ya Tano hii ni bajeti yao ya pili na unaona kwamba tunafanya maendeleo *progressively*. Mimi yangu sasa ni *recommendations* ambazo Mheshimiwa Waziri nimempa kwa kirefu, mambo mengine kimaandishi, lakini haya tu naya-*highlight*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ili kusudi tuwe na uchumi wa viwanda ni lazima tuwe na *stable tax regime*, yaani hali ya kodi iwe imetulia. Kwa hiyo, naomba kabisa kadri tunavyoendelea tusiwe tunabadilisha sheria mara kwa mara ile misingi yake. Tubadilishe viwango lakini siyo misingi ya sheria kwa sababu Mwekezaji akija ataangalia kama sheria iko *stable* au kama inayumba. Hilo ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili naomba nitoe ufanuzi, wachangiaji wengi hapa wamezungumzia habari ya mafuta, napongeza Waziri na Serikali kwamba wamependekeza kama ilivyopendekezwa na imekaa vizuri. Huwezi kuwa na tofauti kubwa kati ya mafuta na *diesel*. Watu wa pembezoni Mkoa wa Kagera, Kigoma na Kadhalika tulikuwa tunapata tabu sana, watu walikuwa wanachakachua mafuta, vituo vya *petrol* vile vimeyeyuka vimekwenda wapi? Kazi yao ilikuwa ni kuchakachua, walikuwa wanaharibu magari, wanaharibu vifaa na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa dakika tano.....

**MHE.PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga taarifa kwa kifupi muda wetu umekwenda.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba hata wananchi wake wa kule Jimboni kwake hawana uwezo wa kununua mafuta ya taa kwa bei hiyo mpya ambayo itakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba bei itakuwa kubwa sana haitakuwa nzuri sana, kwa hiyo kauli yake kidogo airekebishe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka unaikubali taarifa hiyo?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Taarifa nimeikataa kwa sababu kule kwangu shida yetu ni magari yasiharibike, *engine* zisiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie, ninaowazungumzia mimi ndiyo Mwakilishi wao, hata viwanda kama Kagera *Sugar* karibu isimame kwa sababu *diesel* ilikuwa inachakachuliwa. Kwa hiyo, uchakachuaaji ni mkubwa, jambo hili ni zuri msileté siasa ambazo hazitufikishi mahali popote. Kwa hiyo, mafuta ya *petrol*/*ilivyokaa* kwenye bajeti imekaa poa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *withholding tax*. Mheshimiwa Waziri naomba ufanuzi bila shaka utatolewa kama Mheshimiwa alivyosema kwenye Kamati ilivyokaa hapa kwenye sheria, tuweze kujua walipaji wa *withholding tax* itakwendaje iko *clause* ya 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu samaki, mimi nawakilisha wavuvi hapa, hili nimeambiwa na nimeahidiwa kwamba sasa ile *regulation* ya samaki itabadilika iwe kwa shilingi siyo kwa dola tena. Kwa hiyo, wapiga kura wa Muleba na wavuvi wengine kwa ujumla Tanzania waliokuwa wanalipishwa kwa dola sasa hili sasa linaondoka na tunashukuru sana kwamba Waziri ameshatangaza hili. Kwa

hiyo, Waziri wa Uvuvi basi asichelewe kubadilisha suala hili kwa sababu linatesa sana wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwango vya kodi. Sisi hapa ni waajiriwa tunalipa asilimia 30 ya kodi katika mapato yetu. Rais wetu sasa hivi anapambana na hawa watu waliokuwa wanachukua madini yetu kwa bei poa. Napendekeza na pendeleko hili nimempa Mheshimiwa Waziri huko tunakokwenda *going forward, progressive tax system* iingie hapo, watu wanaovuna madini, sisi tupate asilimia 51 ya *corporate tax* wanayopata. Viwango visilingane, hiyo inaitwa *progressive taxation*, kwa sababu sasa mfanyakazi asilimia 30, mtu wa mgodi asilimia 30, watu wa mafuta asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi nyingine halko hivyo na Mheshimiwa Waziri anajua ninaloliongelea, naomba lifanyiwe kazi. Tuwe na *progressive taxation* wale wanaovuna madini yetu tuweze kupata faida kubwa, sasa hivi wakati Rais anapambana na sisi tumuunge mkono katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo naweza kusema ni suala la kuwapa haki wafanyabiashara. Kama nimezungumza *tax regime* katika ile *tax appeals process*, kama *TRA* wakibishana na Mlipa Kodi ni muhimu sana ionekane kwamba anaweza akapata haki huko anakokwenda. Kwa hiyo, unapokuwa na mgogoro lazima unakuwa na *status quo* inakuwa *maintained*. Kwa hiyo, kuna vipengele vingine vinaweza kuleta ukakasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo maelezo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa George Masaju Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mpango.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wangu kwa kazi kubwa anayoendelea nayo Mkoani Pwani. Tumeona kwenye vyombo vy ya habari akifungua viwanda kama sera yetu ya Chama cha Mapinduzi inavyosema. Tunamshukuru Mungu kwa sababu tumeanza kutekeleza ndani ya miaka miwili angalau kuna watu walisema viwanda hivyo vitabaki kuwa historia havitajengwa lakini tumeona Rais akifungua vile viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Waziri wa Fedha na Serikali nzima kwa bajeti yao itakayobaki kuwa ya Kihistoria kwa sababu imechukua maoni mengi ya Wabunge. Vilevile, bajeti hii imekwenda kugusa kabisa matatizo ya Watanzania, naipongeza sana Serikali yangu kwa kuonesha dhamira ya waziwazi ya kuwa na nchi ya Tanzania ya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia kwenye kitabu cha sheria *Part Four* inasema *Amendment of Excise Management and Tariff Act, Cap. 147* ikiongelea tozo ya shilingi 40. Niiambie Serikali kwamba tumekubaliana kabisa na tozo ya sh.40/= na tunawapongeza sana Serikali kwa kutuleta tozo hiyo. Naomba Serikali yangu, kwa sababu tumekubali kutozwa sh.40/= na kwa sababu wanawake tuna shida ya maji na Watanzania kwa ujumla. Kwa sababu tuliahidi kumtua mwanamke ndoo ya maji, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hii sh.40/= asilimia kubwa ya pesa hii iende kwenye maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hii bajeti ya 2017/2018, hatuwezi kumaliza matatizo yote ya nchi hii ya maji, lakini tuoneshe *concern* yetu kwamba kweli tumedhamiria kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani. Kwa hiyo, niombi Serikali ipeleke asilimia kubwa ya pesa hizo katika maji vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wenzetu hawa wanasema hii tozo ya sh. 40/= tumewaonea watu wa vijijini

ambao wanatumia mafuta ya taa. Mimi bado napingana nao kabisa na naiomba Serikali iwapuuze wala isiwasilizile, kwa sababu miaka yote Tanzania kodi inayokusanya, kodi ikikusanya kwenye maliasili na utalii Arusha inatumika nchi nzima, ikikusanya kwenye madini Geita *GGM* inatumika nchi nzima, ukikusanya kwa wafanyabiashara wa Dar es Salaam inatumika nchi nzima, kila mnachokifanya tunakitungia Watanzania wote bila kujali maskini, tajiri, sijui kabilia gani, kabilia gani, hilo suala hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wenzetu hawa wamedhamiria. Tuliwaambia siku ya bajeti kwamba mbona tunalipa tozo ya *Railway Development Levy* watu wangapi wanapanda treni? Hii reli inatumiwa na watu wachache, lakini Mtanzania yejote atakayenunua mafuta analipa kodi hii. Tunalipia *REA* vijijini siyo wote wa mijini wanataka huo umeme wa vijijini, lakini kwa sababu ni jambo letu sote tunakuwa tunalifanya sote, lakini wenzetu hawa hawakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza Waziri Kivuli wa Fedha wa Upinzani amekuja hapa amekataa kila kitu, hakuunga mkono hata kitu kimoja kizuri kwenye bajeti hii, ndipo utakapojuwa hawa watu wana matatizo yao mengine tofauti. Wameikataa bajeti hii wamesema bajeti yote ni mbaya na bajeti hii itaingia kwenye historia ya bajeti mbaya kuliko zote nchini. Ndipo unapoweza kuwaona hawa watu ni watu wa aina gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hawa watu tumewazoea.....

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. MONDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumewazoea sana hawa watu kwa sababu kupinga kwao ni kawaida ila hatuna habari nao tunaendelea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde kuna taarifa. Mheshimiwa Silinde taarifa kwa kifupi.

## T A R I F A

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe Taarifa mzungumzaji, ni vizuri akasoma hotuba yetu, unajua kusoma ni jambo la msingi sana, tumekosoa na tumejhauri. Kazi ya Upinzani ni kukosoa na kushauri kutaka kuboresha mambo mengi ambayo Serikali inataka kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, aangalie kila eneo ambalo tulikuwa tunaainisha kwa nini hatuungi mkono na tumeweka vilevile *way forward* ya namna ya kutekeleza. Kwa hiyo, asiwe anaropoka tu kama kufurahisha labda kuna mtu anamsikiliza kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Ushauri wa...

**NAIBU SPIKA:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Munde, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza yeye ndio anaropoka, yeye na Kambi yake ndio wanaropoka si mimi, hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili wamekosoa na wameshauri, hawakuunga mkono hata kitu kimoja kwenye bajeti na ndilo nililolisema, kwa hiyo yeye ndio ameropoka. Hata Bajeti Kuu hawajawahi kuunga mkono hata neno moja wakasema hili kwa leo mmesema zuri. Angalau Wajumbe wao wa Kamati Kuu ya CHADEMA walimuunga mkono Rais kwenye makinikia, lakini wao wamekataa kila kitu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu ni watu wa ajabu sana, mimi nasema aliyewaroga labda amekufa, kila kitu wanakataa. Leo hii wanathubutu kuongea, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya nini, hakuna chochote kilichofanywa na Serikali hii; wakisahau kwamba sasa hivi tunajenga reli ya *standard gauge* ambayo tulikuwa tunatoka Dar-es-Salaam mpaka Mwanza kwa siku tatu lakini leo hii

tutatoka kwa saa saba kutoka Dar-es-Salaam mpaka Mwanza, hawaoni yote hayo. Hawaoni kila tulichokifanya hawakioni! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hawa watu tuwahurumie wana laana ya kumkataa Dkt. Slaa. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia. Pia nikupongeze kwa jinsi ambavyo umeendelea kuliongoza Bunge hili kwa ufanisi ipasavyo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia na nawashukuru sana watumishi wote na Wanasheria wa Serikali wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jinsi ambavyo wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ipasavyo kwa maslahi ya Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri sana ambayo naiunga mkono. Niipongeze Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa waliyoifanya kui-*engage* Serikali ambayo ilisababisha Serikali ikaja na mapandekezo haya ambayo sasa inayajadili na Wabunge wanaunga mkono kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanua mambo machache kwa sababu ya muda mfupi nilionao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kwa ufupi na kwa harakaharaka sana, baadhi ya Wabunge wamechangia juu ya kuleta mabadiliko kwenye ile *Urban Authorities Rating Act*, kwamba wale wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea wasitozwe kodi ya majengo. Uamuzi huu tayari

ulishafanyika kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016. Ukitisoma Kifungu cha 69 kimeeleza na pale tumeweka vizuri, pale wazee miaka 60 na kwenda mbele, lakini na watu watu wengine wote wenye ulemavu ambao hawana namna ya mapato, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo naomba kuliweka wazi ni hili; kumekuwa na michango hapa kwamba msamaha wa tozo ya usajili wa magari kwamba, ni kiini macho kwa sababu hatukuleta Mabadiliko hapa ya Sheria ya *Traffic (Road Traffic Act)*. Ukweli ni kwamba hizi kodi ziko kwenye Kanuni, kwa hiyo, hatuhitaji kuleta hapa Muswada. Someni hizi Kanuni, *Government Notes Number 177* ya Mwaka 2001 ambayo ilirekebishwa tena na Kanuni Namba 235 ya Mwaka 2013, kwa hiyo hatuhitaji kuleta Muswada hapa, kila kitu kiko sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo naomba kushauri ni hili la uhalali wa Muswada huu. Kwa ufupi naomba kusema hivi; Muswada huu haukuvunja Kanuni yoyote zinazo-*cover*utungaji wa sheria, sehemu ya nane yote imezingatiwa. Waheshimiwa Wabunge wameshirikishwa ipasavyo kupitia kwenye Kamati, hawa wadau wameshirikishwa na wadau wale pamoja na Wabunge ndio tukaborresa ule Muswada kwa yale waliyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa awali ulikuwa na sheria tisa, kwa waliyopendekeza tumeongeza sehemu ya sheria sita. Sasa Kanuni zetu zinazotuongoza kwenye Bunge linapokaa, linaturuhusu kufanya mabadiliko kuboresha kwenye vifungu vya Sheria zilizoko kwenye Muswada, haikuwepo! Kwa hiyo, hekima ikasema tuuchapishe huu Muswada upya, na kuuchapisha Muswada upya imeruhusiwa kwenye Kanuni zetu, someni Kanuni ya 86(10), Muswada ulichapishwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo kwa sababu ni ya msingi sana, naomba muishukuru Serikali kwa kuyakubali haya na naishukuru sana Kamati ya Bunge na Wabunge wote ambao wameunga mkono suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kuendelea kuwaunga mkono ndugu zangu Waislamu ambao wanashiriki toba hii, Mungu aendelee kuwabariki. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuendesha vizuri majadiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017/2018. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia kwa umahiri wake wakati wa uendeshaji wa Vikao vya Kamati ya Bajeti wakati ikiwa inajadili Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa maoni na ushauri wao waliooutoa wakati wa majadiliano ya Muswada, ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa sana kuboresha Muswada huu uliowasilishwa mbele ya Bunge zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutambua michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi. Naahidi kwamba Serikali itafanya kazi ushauri na mawazo mazuri ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja zimetolewa na Kamati ya Bajeti, kuna hoja za Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambazo ningependa nizitolee ufanuzi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba adhabu za makosa ya barabarani zimekuwa kama ni chanzo cha mapato. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba si kweli kuwa fedha ambazo zinakusanywa na Jeshi

la Polisi ni chanzo cha mapato. Adhabu inayotolewa kwa madereva ni kuhakikisha kwamba madereva wanafuata na kutekeleza bila shuruti Sheria za Usalama wa Barabaran kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo si kweli hata kidogo kwamba, hiki kimehesabika ni chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba Serikali kuhamishia fedha za taasisi na mashirika ya umma Benki Kuu inakiuka sheria. Serikali kabisa kabisa haijakiuka na hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu, Kifungu cha 32(1) ambacho kinataka Taasisi na Mashirika ya Umma kuhifadhi fedha zao Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba kupandisha ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zinazotengenezwa kwa kutumia malighafi za hapa nchini pengine hatuwezeshi zaidi *competitiveness* ya bidhaa zetu za ndani. *Excise Duty* tulizoleta mbele ya Bunge lako Tukufu tulirekebisha ushuru wa bidhaa kulingana na mfumuko wa bei na hali ya uchumi. Hatuwezi kurekebisha tu bila kuwa na misingi. Kwa hiyo, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge kuzingatia hili, hatuwezi tu kwenda *arbitrarily*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo pia hoja kwamba, ukiongeza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa tunawaonea wananchi maskini waishio vilijini. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao katika michango yao wamelifafanua hili; nami tu niongeze kwamba kwa kweli hatua ya kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa ililenga kuwalinda Watanzania wote dhidi ya madhara ya uchakachuaji wa mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama zile sh.40/= kwa lita tungefanya kwenye dizeli na petroli peke yake tukaacha mafuta ya taa, huu uchakachuaji wa mafuta ambao tuna uzoefu nao kama Taifa (*fuel adulteration*), basi ingekuwa ni shida kubwa kwa maana ya vifaa hivi vya moto ambavyo watu wote hata maskini nao wanatumia, ambayo ina madhara makubwa sana kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha ambazo zitapatikana kutohana na chanzo hiki, sehemu ya mapato yanaenda kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo maji, afya na elimu ambayo inakwenda kumgusa mwananchi wa kawaida kabisa, hawa wanaoitwa maskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba, Serikali ina poka vyanzo vyahalmashauri na hivyo kuua dhana nzima ya *Decentralisation by Devolution*. Hili si kweli hata kidogo. Serikali imeamua kuboresha ukusanyaji wa majengo na tozo za mabango kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania. Serikali itaendelea kusimamia na kuzipatia ruzuku halmashauri zake, ili tuhakikishe kwamba, zinaendelea kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, lengo letu si kudhoofisha halmashauri hata kidogo na ndiyo maana tunasema tukishakusanya zile fedha sisi tunaamini kwamba ufanisi utakuwa mkubwa, tutapata fedha nyngi zaidi na ndio maana tutazirejesha kwa kuzingatia Bajeti za Halmashauri lakini vilevile ni lazima tujiridhishe kwamba, matumizi hao yako sawasawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo pia hoja kuhusu kuwatambua na kukusanya kodi kwa wafanyakiashara wasio rasmi. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu, kwanza ni lazima kama Taifa tujenge utaratibu wa kila mtu kulipa kodi, ni lazima na lazima tupate mahali pa kuanzia. Tusidanganyane, kama tunatafuta fedha ya maji, tunatafuta fedha ya dawa hospitali, tunatafuta fedha za kujenga barabara, nimesema na narudia tena, nimeshachoka kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanao uwezo wa kuchangia maendeleo kulingana na kipato chao. Hata hivyo, kwa mwaka huu tunachofanya kwanza ni kuwatambua na nilisema wakati wa Hotuba ya Bajeti Kuu; tunawatambua ili tuweze kuwapatia sehemu muafaka za kufanya biashara zao, hilo ndilo jambo la msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kurekebisha Sheria ya *EPOCA* kwa kuondoa *Local Share Holder* na kuweka *Public* ili kuondoa dhana nzima ya kuwawezesha Watanzania kumiliki kampuni za simu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba, Marekebisho ya Sheria ambayo yametajwa kwenye hoja hayaondoi dhana na madhumuni ya awali ya Sheria ya *EPOCA*. Ifahamike kwamba, Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana ina wajibu kisheria wa kusimamia Sheria, Kanuni na Kudhibiti mwenendo wa biashara katika Masoko ya Mitaji nchini na jukumu hili ni pamoja na kuhakikisha ulinzi wa maslahi ya wawekezaji wa Kitanzania katika Masoko ya Mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mauzo ya hisa katika soko la awali yatafanyika kwa umma nchini Tanzania na baada ya mauzo ya hisa kufanyika mgawanyo wa hisa (*Allotment*) kwa wawekezaji walioomba kununua hisa utatoa kipaumbele kwa wawekezaji wa umma wa Watanzania kwanza kabla ya uwekezaji wa nje kupata mgawo wa hisa zilizouzwa na kampuni husika kwa mujibu wa Sera ya Mgawanyo wa Hisa (*Allotment Policy*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na *CMSA* imekuwa ikitekeleza sera hiyo hata kwenye mauzo ya awali (*IPO*) ya hisa yaliyofanyika hapo nyuma. Kwa hiyo basi, marekebisho ya Sheria yaliyotajwa kwenye hoja hayaondoi dhana na madhumuni ya awali ya Sheria ya *EPOCA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali ilete Muswada Kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Madini ili kuongeza mapato kutoka sekta ya madini kwani *clearing fee* ile ya asilimia moja si suluhisho. *Clearing fee* inayopendekezwa ni kwa ajili ya kutambua madini yote yanayochimbwa na kuuzwa hapa nchini na yale yanayosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, muda ni mfupi, tutawasilisha maelezo kwa maandishi kwa hoja ambazo tumezipokea. Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 ni sehemu ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa Fedha nilioiwasilisha mbele ya Bunge tarehe 8 Juni, 2017. Muswada huu ndio unaowezesha utekelezaji wa Kisheria wa Bajeti ambayo ilipitishwa na Bunge tarehe 20 Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Serikali iweze kutekeleza ahadi zake kwa wananchi, ikiwemo kutatua matatizo na kero zinazowakabili wananchi ikiwemo huduma za maji, afya, elimu, barabara na kadhalika, ni vyema Bunge lipitishe Muswada huu na Muswada huu ndio unaidhinisha Kisheria hizi kodi na tozo na hatua mbalimbali za kiutawala za kukusanya mapato ya shilingi trilioni 31.7 na uamuzi wa kujenga Tanzania ya Viwanda chini ya uongozi wa Rais wetu unahitaji hatua za kijasiri katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na Muswada huu umetafsiri hatua hizo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, nawaomba Waheshimiwa Wabunge mridhie Muswada huu, ili upite na kuiwezesha Serikali iingie kazini kukusanya mapato kwa ajili ya ku wahudumia Watanzania na kutekeleza bajeti hii ya kihistoria katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo, tutaendelea na utaratibu wetu.

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. PHILIP I. MPANGO, THE MINISTER FOR  
FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF  
A BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2017"**

*(Made under S.O 86(10)(b))*

A Bill entitled "The Finance Act, 2017" is amended as follows:

- A:** In Clause 7 by-

  - (a) deleting the words "in section 26" appearing at the end of the opening phrase;
  - (b) deleting the phrase "in the case of network facilities or network service licensee" appearing in the proposed paragraph (a) and substituting for it the phrase "in the case of a holder of network facilities or network services licence,";
  - (c) deleting the word "deleing" appearing in the proposed paragraph (b) and substituting for it the word "deleting"; and
  - (d) deleting the words "fails to obtain the" appearing in the proposed subsection (6)(d) and substituting for them the words "does not attain the prescribed threshold of";

- B:** In Clause 27(a)(i) by-

  - (a) deleting the words "thirty five" appearing in the proposed subsection (2)(a) and substituting for them the word "thirty"; and
  - (b) deleting the words "of the United Republic of Tanzania" appearing in the proposed subsection (2)(b);

- C:** In Clause 30(c) by deleting the words "local authorities" appearing in the proposed subsection (6)(a) and substituting for them the words "local government authorities";
- D:** In Clause 32(a) by deleting "2%" appearing in the First and Second Column of paragraph (b) and substituting for it "3%";
- E:** In Clause 37 of the proposed section 90A by-

  - (a) deleting the word "inspection" appearing in subsection (2) and substituting for it the word "clearance";
  - (b) deleting the words " an inspection" appearing in subsection (3) and substituting for them the word "clearance";
  - (c) deleting the words "amount of inspection" appearing in subsection (4) and substituting for them the word "clearance"; and
  - (d) inserting the words "mineral or" between the words "value of" and "minerals" appearing in the proposed subsection (5);

- F:** In Clause 38 by deleting the words "inspection and" appearing in the proposed paragraph (i);
- G:** In Clause 40(a) by deleting the word "owned" appearing in the proposed subsection (4);

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- H:** By deleting Clause 42 and substituting for it the following:  
"Amendment 42. The principal Act is amended in section 67 by adding  
of section 67 immediately after subsection (2) the following:  
" (3) The Tanzania Revenue Authority shall collect  
wharfage revenue and deposit the same in a bank account  
opened at the Bank of Tanzania, and the revenue shall be  
disbursed to the Authority by the Paymaster General.";

**I:** In Clause 44 by-  
(a) deleting the words "in section 6" in the introductory Clause; and  
(b) deleting the word "under" appearing between the words "prescribed" and  
"regulations" in the proposed subsection (2) and substituting for it the words "in the";

**J:** By adding immediately after Clause 46 the following:  
"Amendment 46A. The principal Act is amended in Part B of the First Schedule  
of First Schedule by adding item 50 as follows:  
" 50. The Ports Act, Cap.166.";

**K:** By deleting Clause 49 and substituting for it the following:  
"Addition of 49. The principal Act is amended by adding immediately after  
section 22A section 22 the following:  
Registration 22A.-(1) The Commissioner General shall  
of small recognise and register small vendors and service  
vendors providers conducting business in an informal  
and service sector.  
providers  
(2) A person registered under subsection  
(1), shall be issued with an identification card by  
the Commissioner General.  
(3) For purposes of this section, "small  
vendors and service providers" include hawkers  
(*machinga*), caterers, event managers, masters  
of ceremony and such other small vendors and  
service providers as the Minister may prescribe.";

**L:** By deleting Clause 52;

**M:** In Clause 64 by deleting the words 'the like" appearing in the interpretation of the term  
"rateable property" and substituting for them the words 'such other similar houses";

**N:** By deleting Clause 66 and substituting for it the following:  
Amendment 66. The principal Act is amended in section 16 by-  
of section 16  
(a) inserting immediately after subsection (1) the following  
subsections:  
 (1A) Notwithstanding subsection (1), a building  
 which is not valued in accordance with this Act, shall be  
 charged property rate at the rate of-  
 (a) ten thousand shillings for ordinary building; and

(a) fifty thousand shillings for each storey in a storey building;

Provided that a fraction of a building belonging to one or several co-owners in accordance with the Unit Titles Act shall be Cap.416 treated as a separate building."

(b) deleting the proposed subsection (2) and substituting for it the following subsections:

"(2) The property rate collected under this section shall be deposited in the Consolidated Fund.

(2A) The apportionment and disbursement of the proceeds collected under this section shall be made to a local government authority based on its budget."

(c) inserting in the proposed subsection (9) the following definition in its alphabetical order-

"ordinary building" excludes mud huts, thatched houses, mud houses and such other similar houses ordinarily used for residential purposes."

O: By renumbering Clauses 53, 54, 55, 56, ... 74 as Clauses 54, 56, 57... 73 respectively;

P: By inserting immediately after Clause 73 as renumbered the following new Part:

**"PART XVII**  
**AMENDMENT OF THE RAILWAYS ACT,**  
**(CAP.170)**

Construction Cap. 170      **74.** This Part shall be read as one with the Railways Act, herein referred to as the "principal Act".

Amendment of section 20      **75.** The principal Act is amended in section 20A by deleting the "full stop" appearing at the end of subsection (3) and substituting for it the following:

"and Kerosene type Jet Fuel (Jet A1) classified under HS Code 2710.19.21."".

Dodoma,

....., 2017

**PIM**  
MoFP

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae, kuna tangazo moja la wageni. Kuna wageni ambao walitangazwa asubuhi, lakini hawakuwa wamefanikiwa kuingia humu ndani; kundi moja ni la qanafunzi 86 na Walimu sita wa *Black School of Linguistics and Literature* kutoka Mkoani Dodoma, hawa wamekuja kujifunza shughuli za Bunge. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia asubuhi nilitangaza wageni wa Mheshimiwa Jafari Michael kutoka *FPCT*. Saa hizi nimeletewa tena tangazo nikiambiwa ni wageni wa Mheshimiwa; sijui kama ni wageni tofauti ama ni kundi hilo hilo wameletwa na Wabunge wote wawili, lakini natangaza kwamba, kuna wageni 40 wa Mheshimiwa Joshua Nassari amba ni Vijana wa Kanisa la *Free Pentecostal Church of Tanzania* Jimbo la Arusha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Hayo ndio matangazo tuliyonayo; kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada ya Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017**  
*(The Finance Bill, 2017)*

Ibara ya 1  
Ibara ya 2  
Ibara ya 3  
Ibara ya 4  
Ibara ya 5  
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilliptishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 20 Waheshimiwa kina marekebisho ya Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka marekebisho kwenye Muswada wa kwanza ambapo sasa ina-appearkwenye Ibara ya 30 na 31 na si tena ya 20 kwa mujibu wa nani ya kwanza. Nimekuletea taarifa hapo mbele.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye ibara 20 na ibara 21, hivyo hivyo itaenda 30 na 31 kwa marekebisho ya Muswada sijui wa pili au wa nyongeza.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwa ridhaa yako na ya Serikali kwamba kifungu hicho kitaje kiasi ambacho kitarejeshea halmashauri baada ya kukusanya kodi ya mabango na nilishauri angalau

kiwango cha chini *at least* kiwe ni asilimia 50 (*fifty percent*) ya kiasi ambacho kimekusanya na *TRA* ili kuzihakikishia halmashauri uhakika wa kutekeleza bajeti zake. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye hotuba yake; kwamba lengo kubwa la kuchukua kodi hii ni kuleta ufanisi katika kukusanya. Pia Mheshimiwa Waziri akaendelea kueleza kwamba zitakapokusanya zitarejeshwa kwa halmashauri kulingana bajeti zao. Kwa hiyo hilo ndiyo la muhimu kabisa kwa sababu imekuwa ni kawaida kwa Waheshimiwa Wabunge kila mmoja anasema hajapelekewa maji, barabara pamoja na wale ambaao walikuwa wakikusanya mapato ya kutosha katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lengo la Serikali ni jema kabisa la kuhakikisha mapato haya yanakusanya yanawekwa pamoja na hakuna halmashauri hata moja itakayokosa pesa kulingana na bajeti yake kama ilivyowekwa. Kwa hiyo, niombe tu Mheshimiwa Japhary akubaliane na hii *clause* iliyoletwa na Serikali. Lengo ni jema na lengo ni kuhakikisha maendeleo yanafika maeneo yote ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapingana na Serikali kwamba hawana mchango wao wanaopelea katika halmashauri kwa sababu mapato yanayozientesha Halmashauri ni pamoja na mapato yanayotoka Serikali Kuu. Hoja yangu ni kwamba, halmashauri hizi zilikuwa na fedha zinazokusanya kwenye bajeti zao na fedha hizi zimechukuliwa na Serikali Kuu. Sasa unaposema zitarudishwa kwa mujibu wa bajeti za halmashauri inafanana

na mapato mengine tu na haya ni mapato ambayo yamenyang'anywa halmashauri yakapelekwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichokuwa nakihitaji ni *commitment* ya Serikali kwamba ni kwa kiwango gani watahakikisha kwamba fedha hizi ambazo zilikuwa zinakusanya kwenye halmashauri zinarudi kama zilivyo. Na mimi nikashauri kwamba, kwa sababu ya gharama za ukusanyaji angalau isipungue asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii ichangiwe na Wabunge ili tuone kwamba ni namna gani tunaweza tukaishauri vizuri Serikali kwa pamoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Mwigulu Nchomba.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu tunauona pale. Akishaitwa wa CHADEMA mmoja maana yake CUF hawesi kuwepo, wakiitwa wao wawili *then* ninyi ni mmoja. Kwa hiyo mkitaja *ratio* ndiyo maana yake hiyo. Sasa mkitaja *ratio* maana yake huku saba waongee ninyi mzungumze watatu. Wakati wa Kamati hatutumii *ration* hiyo ndiyo maana tunajaribu kutumia hekima kidogo.

Sasa ukitaja *ratio* maana yake huku nitaje saba ndiyo ufuate wewe. Kitu ambacho kitakuwa kigumu katika uendeshaji wa Bunge, ndiyo maana tunajaribu kuweka hivyo kama watu wakizunguza wawili, basi wamepewa nafasi hao. Kwa hiyo twende vizuri.

Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Mwigulu Nchomba.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ningependa kabisa na niliombe Bunge tukubaliane na hoja ya marekebisho ya Mheshimiwa Japhary. Tukumbuke kwamba hizi fedha zilikuwa ni *own source* na tayari tulikuwa tumeshaziwekea bajeti kwenye halmashauri zetu. Hata hivyo, Serikali inaendelea kudhoofisha halmashauri zetu kwa kuendelea kuchukua mapato na kupeleka Serikali Kuu. Mheshimiwa Japhary kaiweka vizuri kwamba angalau asilimia 50; na *in fact* mimi ningekuwa nimeleta hiyo *amendment* ningesema kabisa zirudishwe zote asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ile sheria wameweka masharti kwamba kama halmashauri inabidi iandike barua ijieleze inaomba hizo fedha kwa ajili ya nini *and then* mtapitia msiporidhika na kile ambacho halmashauri imeandika, hamleti hizo fedha. Huku ni kuua halmashauri; na wakati huo huo Serikali inasema halmashauri ambazo hazitafikisha asilimia 80 mnaenda kuzifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Mheshimiwa Japhary na Waheshimiwa Wabunge kama kweli tunahitaji halmashauri zetu zijiendeshe, basi tumuunge mkono ili Serikali iweze kuondoa gharama tu za ukusanyaji, fedha zingine zote zirudi tena bila masharti kwamba halmashauri ijieleze inakuja kufanya kazi gani. Nashukuru. (*Makofii*)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwenzangu ambaye alitoa hiyo hoja akubaliane na hoja ya Serikali. Kuanzia mwanzo tunesema mapato yote yakikusanywa na *TRA* sisi kwenye bajeti zetu pamoja na Halmashauri za Wilaya Babati, kile kiasi ambacho tulikuwa tunakusanya (*property tax*) au kodi yoyote ya majengo au nyingine yoyote tutarudishiwa kutokana na bajeti tulivyopanga na itaendelea kuwepo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato mengi yote hayo tuna uhakika tutafanya vizuri. Sehemu kubwa ya hizi kodi tunazonung'unikia kwa mfano kwenye wilaya yangu hiyo ilikuwa inakusanywa na wakala; wakala sasa atakuwa *TRA*

badala ya huyo mtu binafsi. Kwa hiyo, naomba tuiunge mkono hoja ya Serikali na mapato yetu yote yakusanywe kwenye *central*, turudishiwe ili kazi iende vizuri. Ahsante na naunga mkono.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni niunge mkono hoja ya Serikali na huu ni uamuzi wa Serikali ambao umezingatia mambo mengi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, utekelezaji wa maendeleo ni bajeti, hapa sisi Waheshimiwa Wabunge jambo ambalo tunatakiwa tusizitize ni suala la makusanyo na makusanyo kwenda kwenye bajeti zilizotengwa kwenye kila halmashauri. Hilo ndilo jambo la msingi ambalo tunalionelea hapa. (*Makof*)

Mhesimiwa Mwenyekiti, tukianza kuongelea kuhusu makusanya *in piecemeal* kutoka kwenye halmashauri na kwenye sekta zingine, tukumbuke kwamba tuna sekta nyingi sana zinazokusanya na kama kila sekta itataka ipate angalau asilimia 50, maana yake hatutakuwa na *logic* ya kuwa na bajeti kubwa ya Serikali. La msingi hapa ambalo na ndio uamuzi wa Serikali ambacho kimefanyika ni kuboresha ukusanyaji na tukishaboresha ukusanyaji, tunapeleka kwenye mahitaji ya bajeti yaliyopitishwa kutoka kila halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunatambua kwamba halmashauri hizi zinatofautiana. Ili kujenga usawa huu utaratibu ulioletwa na Serikali ndio utatambua halmashauri maskini na utaweza kusaidia zile halmashauri zilizo maskini na *at the same time* kuweza kusaidia halmashauri kubwa ambazo mara nyingi ndizo zinakuwa na miradi mikubwa ambayo inahitaji fedha nyingi za Serikali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aridhie utaratibu ulioletwa na Serikali; na ndilo jambo ambalo linaonekana lina tija kuliko utaratibu mwingine ambao tulishaujaribisha na haukuleta matunda mema.

**MHE. MUSSA A.ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtoa hoja Mheshimiwa Japhary akubaliane na wazo la Serikali. Sisi kwenye Kamati ya Bajeti tulilipitia sana hili na Serikali ukitazama imefanya marekebisho mazuri tu, kwa sababu sasa kwenye *amendment* ya Serikali wanasesma:

*“...disbursement of the proceeds collected under this section shall be made to a Local Government Authority based on its budget.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye Sheria ya kabla ya *amendment* hii ilikuwa inasema *budget needs*, lakini sasa Serikali ita-*disburse* hizi pesa kuzirudishia halmashauri, *tuli-negotiate*; na ukiangalia halmashauri yangu mimi ya llala ambayo bajeti yetu ya kodi ya majengo ni shilingi bilioni 18. Sasa mpaka sisi tumeridhika kwenye Kamati ya Bajeti, tunaamini Serikali ina nia njema na hizi pesa zitarudi. (*Makof*)

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaweka fedha nyingi kuboresha Serikali za Mitaa, kwa maana ya dhana ya ugatuaji wa madaraka mojawapo ya dhamira ilikuwa ni kuhakikisha halmashauri zinajitegemea kwa zaidi ya asilimia 35 na mapato yalikuwa yanategemewa lazima yatoke kwenye mabango, kwenye *property tax* na kodi zingine kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Serikali kwamba lazima hizi kodi zigawanywe sawa kuna halmashauri zinazokusanya kodi za mazao, mbona hazijahamishwa kwenye maeneo mengine? Miji inakusanya kodi za mabango, *property tax mnazinyang’anya*. Sasa ninachoshauri Serikali ni *commitment* tu kwamba kiasi kilichokuwa kinakusanywa huko nyuma kwenye halmashauri, kwa sababu wamesema kuna *efficiency*, basi kirudishwe kwenye halmashauri. Kama tunakubaliana kwamba *TRA* ni kama wakala, basi wakala huyo arudishe 50 percent ndicho ninachokiomba. Naomba Serikali ilitekeleza hili vinginevyo naomba suala liamuliwe kwa kura. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa hapa tulipofikia inabidi tuamue kwa kura kama Mheshimiwa mwenye hoja yake alivyosema.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 31 kina marekebiso ya Mheshimiwa Japhary Michael. Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba marekebiso kwenye kifungu hicho kwa sababu kifungu hicho kinahusiana na marekebiso ya kiwango cha faini kwa makosa ya watakaokiuka masharti ya sheria za fedha katika Serikali za mitaa; kutoka kiasi kilichokuwa kinatozwa cha Sh.50,000/= mpaka Sh.200,000/= hadi Sh.1,000,000/= au kifungo cha mwaka mmoja au miwili au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu, hizo faini ni kubwa sana ukilinganisha na uwezo wa watu wetu. Najua kwamba faini ni sababu mojawapo ya kurekebisha tabia za watu, lakini pia kuweka faini kubwa sana siyo kigezo kimojawapo cha kurekebisha tabia za watu. Huko nyuma Sh.50,000/= watu walikuwa hawawezi kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitolea mfano Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ambapo hata kutema mate ni makosa yaliyokuwa yanatolewa Sh.50,000/=, maana yake kwa Sheria hii Manispaa ya Moshi sasa hivi mtu akifanya kosa, atatakiwa atozwe kati ya Sh.200,000/= mpaka Sh.1,000,000=.. Hivyo, watu wengi wataumia, watafungwa, watateswa sana. Kwa hiyo, nashauri kwa Serikali wakubaliane na wazo langu la kuvirudisha viwango kuwa Sh.100,000/= hadi Sh.200,000/= na kifungo cha miezi sita mpaka mwaka mmoja,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika hili namwomba tu mtoa hoja aweze kuacha kama ambavyo imewekwa Serikali kwa sababu moja. Mpaka mtu anafika kulipishwa faini ziko *procedures* mbalimbali ambazo zitakuwa zimefuatwa mpaka kufika hapo pa kulipwa faini au kufungwa. Kwa hiyo, naomba nikumbushe tu kwamba amesema vizuri Mheshimiwa Mwigulu wakati anachangia hoja hii kwamba hakuna maendeleo bila kulipa kodi na wote tunaongelea maendeleo ya Taifa letu lazima kodi hizi zilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msemo unaosema kwamba *Taxes are collected and not paid* kwa hili lazima tuweke hii faini kubwa ili watu waone uzito wa kulipa kodi, na kodi hii wanalipa kwa ajili ya maendeleo yao na wala si kwa ajili ya maendeleo ya mtu yejote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Japhary Michael aweze kukubaliana na mapendekezo ya Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya mijibu hoja kwa niaba ya Serikali. Kwa sababu anataka kuniridhisha au kunithibitishia kwamba chanzo cha mapato cha Serikali ni faini, ambapo mimi siamini. Kwa hiyo, kama tunaweka faini na vifungo kama vyanzo vya mapato ya Serikali basi Serikali itakuwa imekwisha, hiyo Serikali itakuwa haipo. Ninachoamini lengo la faini na vifungo na adhabu ni kurekebisha tabia za watu, ndiyo imani yangu. Mimi siamini kwamba tutawarekebisha kwa kuwatoza viwango vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachoshauri na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ni Mbunge wa Jimbo,

anafahamu uwezo wa watu wake, angekuwa amejibu Waziri wake ningejua angalau lakini yeye ni Mbunge wa Jimbo, wale watu hawawezl kulipa hiyo fedha. Kwa hiyo, ndicho ninachokizungumza hicho, siwatofautishi kwa thamani yao, lakini najua Mbunge wa Jimbo anajua jinsi ambavyo ataanza kupata tabu ya kutakiwa awalipie watu shilingi laki mbili mpaka milioni moja. Kwa hiyo, naomba Serikali na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walione hili katika sura hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili nalo lijadiliwe na Wabunge ili lipate uamuzi sahihi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Niungane na mtoa hoja, na kwa kweli kwa heshima kubwa na kwa unyenyekevu kabisa, naiomba Serikali itusikilize kwa makini kwenye jambo hili; kwa sababu hili jambo linahusu kule katika Serikali zetu za Mitaa na Halmashauri zetu. Wanaoenda kuhukumiwa ni wananchi wetu wa kawaida katika makosa ambayo yalikuwa hayana sheria; yawezekana yakawepo makubwa lakini sana tuyategemee na madogo madogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapotoza faini ya laki mbili mpaka milioni moja na kumfunga mtu mwaka mmoja mpaka miaka miwili, tutajaza magereza. Chukulia hawa tunaowakusudia ni wafanyabiashara wadogo wadogo, ukimfunga hata miezi mitatu mfanyabishara ni adhabu kubwa sana; miezi mitatu mpaka miezi sita inatosha. Ukimwambia faini kati ya shilingi elfu hamsini mpaka laki tano inatosha, hii milioni moja jamani haitekelezeki. Nawaombeni sana kwa heshima kubwa na unyenyekevu mlitazame katika sura hiyo. (*Makofi*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa mara ya kwanza na mimi

naomba niungane na Mheshimiwa Japhary. Ni kweli kabisa kwamba kuna wakati mwingine mtu anaweza akawa hana hata uwezo wa kulipa hii; inawezekana kabisa mtu mwingine hali ya kiuchumi ikayumba akashindwa kulipa. Ikafika sehemu *fine* ingeanzia basi hata laki moja, inaanzia laki mbili kwenda milioni. Kwa hili, naomba upande wa Serikali iliangalie walipunguze na miaka miwili ya kifungo ni miaka mingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tukumbuke *fine* ikiwa kubwa sana inaweza ikachochea rushwa. Ni bora nitoe, kama naona *fine* inaweza ikawa ni milioni moja, tunachocochea mtu kutoa hata laki tano ili asichajiwe shilingi milioni moja. Kwa hili, naomba upande wa Serikali waliangalie lirekebishwe. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge awa Jimbo lakini nashangaa sana yanayotokea hapa katika hoja hii. Yaani mnachomaanisha ni kwamba watu lazima wafanye makosa na kwa maana hiyo tuweke adhabu ndogo, *that's the meaning*, mimi nashangaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi Namtumbo nitahamasisha wananchi wangu wa-*comply* na sheria, wasifanye makosa na baada ya hapo nitawaambia mkifanya makosa hii ndio adhabu yake. Ndivyo ilivyo kwa wenzetu ambaao kuna *high level of compliance*, adhabu zake ni kubwa, hii ndogo sana hata hii laki mbili haitoshi. Ili tuongeze *compliance* lazima adhabu iwe kubwa zaidi, hata hii aliyoiweka ni ndogo sana. (*Makofii/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amenisikitisha sana. Kwanza yeye najua kabisa kwamba anaongoza watu ambaao labda nikiwalinganisha na wa Moshi kuna tofauti kubwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa najaribu kukieleza hapa ndio ukweli uliopo mtaani, ndio ukweli wa watu wetu na najua kabisa kwamba, shida ni kwamba bahati nzuri au mbaya Waheshimiwa Wabunge wengi hatujui utendaji wa watendaji wetu wa Halmashauri hasa wana mgambo. Watu wetu watateseka sana na watafungwa kila siku na matokeo yake mnaiongezea Serikali hasara hata ya kulisha hao wafungwa magerezani kwa sababu ya kutafuta laki mbili ama milioni moja, wakosaji lazima wawepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema bado naendelea kusititiza hoja yangu kwamba hii faini ni kubwa kwa Watanzania, si *relevant* na maisha ya Watanzania. Kwa hiyo ni vyema Bunge hili lifanye uamuhi huu ili iwe *registered* kwamba walio wengi waliamua kwa wingi wao. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tutapiga kura kuhusu hoja hiyo. Mheshimiwa Haonga sijui kwa nini umehamia mbele hapo naona una lako jambo. Nitawahoji, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Japhary Michael ya marekebisho katika kifungu cha 31.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja illamuliwa na Kukataliwa*)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhesabu kura kwa mujibu wa kanuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul unataka kusema wewe umezisikia kelele za ndio nyingi kutoka upande huu?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Si kweli, lakini kwa sababu kanuni zinaruhusu tutazihesabu hizo kura halafu uonekane namna

ambavyo masikio yako hayataki kusikia. Tutazihesabu hizo kura. Hoja yake haijaungwa mkono, nakumbushwa hapa. (*Makofii*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 33

Ibara ya 34

Ibara ya 35

Ibara ya 36

*(Ibara zilitzotajwa hapo juu zilliptishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya sheria ibara ya 37 ilikuwa inaelekeza kwamba kutakuwa na asilimia moja ya *inspection fee* kwenye upande wa madini. Rai yangu kwa Serikali ilikuwa ni kwamba, kwa sababu ya sekta yenye ya madini na kwa sababu ya thamani ya madini na kwa sababu ya umuhimu wake katika nchi yetu, kwa maana ya mapato na kwa sababu tunahitaji mapato ya kutosha asilimia moja ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nafikiri kwamba Serikali ingefanya angalau hata asilimia tano ya *inspection* ya madini ili kuihakikisha nchi kupata mapato ya kutosha kuziba pengo la kibajeti ambalo linaweza likatokea na ambalo *certainly* lina nafasi kubwa ya kutokea ili tusiendelee kila siku kuwa na *budget deficit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Serikali nani anazungumza kwenye hili?  
Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui tafsiri ameichukuliaje lakini *inspection fee* inayozungumzwa hapa ni kwa madini ambayo yako tayari kwa ajili ya kusafiri. Sasa kodi nydingi zinakuwa zimekwishalipwa na hatua hiyo inakuwa ni ya mwisho sana. Kwa hiyo, ni *fee* inayopaswa kuwa ndogo kwa sababu ya ile *inspection* kwa maana ya kitu ambacho kipo tayari *for export or something* kwenye ile *transaction*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Japhary hakuilewa vizuri akadhani ni kama kodi inayojitegemea hivi, lakini kunakuwa kuna kodi nydingi zimekwishakulipwa na ile hatua ni kwa ajili ya kazi hiyo tu. Kwa hiyo, Serikali ikaona wanapofungasha na kusafirisha madini haiwezekani tu wakaondoka bila kulipa hako ka-*fee* kwa ajili ya *inspection*. Kwa hiyo, tafsiri yake ni hiyo, si kwa maana ya kwamba hakujafanywa malipo yoyote yale au *tax* zingine zote pale, hapana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni ya 28(5) naongeza nusu saa ili Bunge liweze kumaliza kazi zake.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais yamefanana na ile mitazamo kwamba upande huu hatuko sawasawa sana; kwamba mimi nilikuwa sielewi ninachozungumza. Mimi nilikuwa naelewa ninachozungumza, yaani si mjinga kiasi hicho kwamba madini hayalipiwi kodi nydingine ni kodi ya *inspection* wala sio kwamba sijui maana ya *inspection*. Kwa hiyo, nadhani ni kadharau fulani hivi, lakini kwa sababu niko huku nimezoea dharau sina tatizo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba nilikuwa najaribu kuiongoza Serikali namna ya kupata mapato katika maeneo sahihi kuliko kufikiri vyanzo

vya faini na vyanzo vingine ambavyo sio vya uhakika. Madini ni kitu cha thamani ambacho tunacho, sioni ubaya wa kuwatoza watu asilimia tano, sioni ubaya wowote ule. Kwa hiyo, ina maana kwamba mimi niliona iongezewe asilimia tano katika kodi zote; bahati mbaya huo sijui mnaita mrahaba sijui mrabaha ni asilimia tatu. Kwa hiyo, ina maana kwamba tungepata pesa hapo, ndio maana yangu ya kuisaidia Serikali kwamba ni vizuri itoze asilimia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Wabunge watatamani kuchangia naomba pia hoja hii waichangie kama wana hoja za ziada ili waweze kusaidia katika hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Mwassa, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Nailbu Waziri wa Elimu. Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kabisa niungane na Mheshimiwa Japhary na leo nawashangaa sana wenzetu nyie wa upande mwagine huko, watawala kwa sababu juzi hapa mlituambia kabisa kwamba mnamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kuangalia sekta ya madini. Leo tena sisi tunashauri kwamba iongezewe hiyo asilimia moja iende asilimia tano, mimi nilifikiri mngesema wote sasa hivi ndio kwa maana ya ile ndio mliyoisema juzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashindwa kuelewa sasa inakuwaje tunakuwa vigeugeu, leo wa kijani, kesho wa njano na keshokutwa mtakuwa hata bluu kwa sababu nashindwa kuwaelewa kabisa. Naomba kabisa kwa umuhimu uliopo kwenye madini tuongeze hiyo asilimia tano. Kama tunaweza kumkaba Machinga, mnamtambua ili aweze kulipa kodi bila ya kumtengea eneo, inakuwaje mnawasamehe hawa walipe asilimia moja? Kwa hiyo, naomba tu waongezewe. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kimsingi hata ndugu yangu Mheshimiwa Mwassa alichomalizia ndicho ambacho Serikali inasema. Kwa sababu *figure* tuliyonayo kama *loyalty* ni four percent, na unapotoza one percent; ukijumlisha one percent na four percent unapata five percent ambayo ndijo ameisema. Kama ingekuwa *figure* hii unaikokotoa sio kwenye gross ingeonekana ni ndogo lakini kwa gross ni *figure* kubwa. Naomba tukubaliane na mapendekezo ya Serikali kwa sababu si kwamba ni namba imeshuka, tunatafuta na best practice wenzetu wanafanyaje. Kwa hiyo, naungana mkono na hoja ya Serikali kwamba one percent inatosha. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya.*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napingana na hoja ya Mheshimiwa Japhary, naunga mkono hoja za mwanzo alizozungumza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na mchango wa Mheshimiwa Kandege. Suala ninalotaka kuzungumza ni kwamba sisi Wabunge inapokuja kwenye mambo mazito yanayohusu tarakimu na mambo maalum ni vema yawe yamefanyiwa kazi ya kutosha, unaposema iwe hivi na si vile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema kwamba unataka asilimia tano, umekokotoa wapi na sisi tuna *evidence* gani ya kufanya maamuzi sasa hivi hapa? Kwa hiyo, nadhani kama kuna umuhimu wa kufanya jambo lolote basi zitakapokuwa zinaletwa sheria nydingine na kuangalia kwa undani suala hilo, ndipo tufikie maamuzi, lakini sio hapa tu mtu anaamka anasema tano, mwingine atasema kumi, hiyo sio sahihi hata kidogo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani wakati kuna jambo ambalo lina maslahi ya taifa na Waheshimiwa Wabunge wakakataa kuliona katika sura yale, lakini wakati huo huo Waheshimiwa Wabunge hao hao

wanaosema ni watu wanaohitaji sana tarakimu miaka 18 wameibiwa mpaka wanaambiwa leo na Rais Magufuli wakati walikuwa hapa Bungeni, wala huwezi kuelewa hicho kinachozungumzwa; ni jambo la kushangaza. Ndiyo maana nasema ni vizuri mkaelewa tunachokizungumza kwa sababu kwa nia njema ya kusaidia Taifa. Hizi tarakimu ndiyo maana Mheshimiwa Magufuli amezikataa ameamua ya kwake anayojua yeje kichwani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri suala hili pia liamuliwe kwa kura.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji kuhusiana na hoja hii ya marekebisho ya Mheshimiwa Japhary Michael kwenye kifungu cha 37.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

Ibara Mpya ya 46A

Ibara ya 47

Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 50

Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Hapa iliyokuwa Ibara ya 52 ya Muswada imefutwa.  
Hivyo, ibara zilizofuata zimekuwa renumbered)*

Ibara ya 52  
Ibara ya 53  
Ibara ya 54  
Ibara ya 55  
Ibara ya 56  
Ibara ya 57  
Ibara ya 58  
Ibara ya 59  
Ibara ya 60  
Ibara ya 61  
Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 63

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 64

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 65

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel; Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU (K.n.y. MHE. RUTH H. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Ruth Mollel, pamoja na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, napenda kupata ufanuzi zaidi juu ya jambo ambalo alilizungumza kwenye hotuba yake kwamba zile nyumba ambazo wazee wenye miaka zaidi ya 60 wanaishi hazitatozwa kodi, lakini kwenye hii sheria sioni mahali popote. Kwa hiyo tunapendekeza kiongezwe kifungu kidogo cha 1(c) kuweza kufanya wasitozwe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kinachopendekewa kiko *covered* kwenye sheria na imeandikwa kama ifuatavyo, naomba kusoma:-

*"one residential/ratable properties which is owned and resided by a person of above 60 years or a person living with disabilities who has no source of income."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii iko *covered* kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka wa jana.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na majibu ya Serikali. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiki kifungu namba 66, nilichokuwa nataka kuomba Serikali ikifanye, imejaribu kuongea kwenye mazungumzo ya kawaida kuhusu suala la watu *disabled* kwa maana ya watu wenye ulemavu, wajane na wale watu ambao wana hali duni sana kwamba wanakuwa-*treated* vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lengo langu lilikuwa kuishauri Serikali kwamba tuongeze hiki kifungu *number 1(c)* katika hiyo sheria ili kiwatamke kabisa, isiwe kwamba ni kwa utashi wa mtu bali itamkwe wazi kwamba watu wenye ulemavu, wajane, yatima na watu ambao wana hali duni kabisa, kwa sababu katika jamii yetu kuna watu ambao wana nyumba, walikuwa na vipato huko nyuma lakini bahati mbaya wakawa hawana tena uwezo, hawa watu watamkwe na sheria kwamba wanasamehewa *Property Tax*. Kwa hiyo naomba nipate maelezo kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *disabilities* nimetoka kulijibu muda si mrefu, kwa hiyo hili liko *covered*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tukija katika hii sehemu sasa ya *widow* anayopendekeza hapa ambaao ni wajane. Sijui tunakuwa tunafungua mlango wa aina gani. Wapo wajane wenye uwezo, kwa hiyo tukisema tu kila mjane asemehewe kulipa kodi inakuwa ni ngumu kidogo. Naomba tuiache kama iilivyo Mheshimiwa Japhary Michael, wapo wajane wenye uwezo kuliko hata watu ambaao wana waume au wake, sasa tuliangalie na tukubaliane na mapendekezo ya Serikali. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiangalia hapa ni *proportion*. Hata *disabled* wapo wenye uwezo, kwa hiyo tusingewatambua kama tungekuwa hatuangalii *proportion*, lakini *proportion wise disabled* wengi hawana uwezo. Tuchukue mzigo wa wanawake wajane wanapofiya na waume zao, nimesema tuache wagane kwa sababu wanaume wengi wanakuwa na uwezo, lakini wanawake wanapokuwa wamefiwa na waume zao, matatizo wanayobaki nayo, wananyang'anywa mali, wanafanya nini, wanabaki na familia, tungewa-*consider* katika kipengele hiki kama watu wa kuwa *exempted*; mimi ndio nilikuwa natafsiri hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sababu mnajiangalia kama Wabunge ambaao mko hapa kwamba ndio mna uwezo, ibaki hivyo, lakini kwa maana halisi ya wanawake wa Tanzania, wanaobaki kuwa wajane wenye shida ni wengi na watashindwa kulipa hii kodi na mtawachukulia nyumba zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeishi katika mazingira ya halmashauri, nafahamu hayo mateso. Nimekuwa Meya nikiwa nafanya *exemptions* za hizi *Property Taxes*, kwa hiyo nafahamu mateso ya wajane ndio maana nimesema

kwamba ni vizuri mkai-*consider* katika uzito wake. Hata hivyo, nimezungumzia hali ya watu wenye maisha duni sana lakini walikuwa wamejenga nyumba, mnawa-*consider* vipi? Nataka majibu ya Serikali pia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wawze kujadili hili pia ili tuweze kupata muafaka wa pamoja. Natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Japhary kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu pia hata kuna wazee wa miaka 60 wenye uwezo. Kama umri wameweza ku-*determine*, ni kwa nini kwa hili la wajane hawataki ku-*determine*? Mheshimiwa Japhary anachoonesha ni kwamba pawepo na nafasi ya kuwatambua hawa watu wakati wa utekelezaji na sheria iseme kwamba na hawa wajane wako *included*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui kwa nini na Mheshimiwa Naibu Waziri kama mwanamke mwenzetu hilo halioni wakati wanawake wengi, anafahamu, hata wanao-*own property* ni wachache, hata wanao-*own land* ni wachache na mara nyingi wakifiwa na waume zao wanaachiwa majukumu ya kulea watoto; na mara nyingi akinamama hawatoki nje wakafanya biashara, anafahamu, hata wa jimboni kwake anafahamu wengi hawajishughulishi na hizo biashara, wanaume wanafanya hizo kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunasema wakubaliane na hoja ya Mheshimiwa Japhary ili hili waliangalie kama walivyoangalia la hawa watu ambao wana ulemavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wenzetu wakubaliane na maoni ya Serikali. Linapozungumzwa suala la wajane tusifikirie wajane wanawake tu, wapo wajane hata wanaume ambao wameachiwa mali na wake zao. Kwa hiyo mimi sioni kama kuna tatizo kwa mwanamke mjane ambaye ana uwezo wa fedha kutolipa... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha iliyotumika inaudhi, wanaume si wajane.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** ...haya basi, wagane.

**MBUNGE FULANI:** Wanaume ni wagane.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, uwe unasubiri ukipewa nafasi ndiyo uzungumze. Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Basi ndugu yangu, wagane, naelewa hicho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba ni vizuri tu hivi ilivyokaa, walivyoleta Serikali iko sahihi kabisa. Nafikiria hivyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nafikiria tunachanganya mambo, kwa sababu ujane ni hadhi ya ndoa (*marital status*) si *income status*. Kwa sababu tukiendelea

kusema hivyo maana yake hata wanawake au wanaume ambao hawajaoa nao vilevile wangeweza kuwa na hoja ya kusema kwamba wawe *exempted*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, tunapofikiria kuhusu walemavu au watu wenye *disability* au wazee, wale tunaangalia kwamba wana vikwazo vyta kupata *income* kwa sababu hizo na ndiyo maana hatuvezi kuwafananisha. Kwa hiyo, nafikiri tuendelee kama ilivyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na *position* ya Serikali na sababu yangu kubwa ni moja; unajua kutunga sheria ni taaluma, sheria haitungwi tu. Moja kati ya misingi ya utungaji wa sheria ni kwamba *the law has to be general in nature*, lazima iwe na *generality*. Yaani sheria huitungi ikawa ama *discriminatory* au ikawa inabagua au inatenga baadhi ya watu, *so it has to be general in nature*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni nyingine ya pili ni kwamba *there is no law without exception*, yaani utatunga sheria ukatengeneza kanuni, kila kanuni ina *exception* yake. Kwa hiyo, unapoona jambo lina mgongano mkubwa kama hili lilivyo, kwamba kinachotafsiriwa hapa ni kipato cha huyu mhusika anayezungumzwa, lazima uiache sheria ibakie vile halafu hizi *exceptions* nyingine zitakuwa zimezingatiwa kwa kadri ya mazingira yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukisema leo hii wajane, Mheshimiwa Jenista Mhagama hapa ni mjane lakini hawesi akapata msamaha. Kwa hiyo, nataka nishawishi na nimshawishi rafiki yangu Mheshimiwa Japhary kwamba akubaliane kwa sababu sheria hii inayotungwa ikianza kuweka vipengele vyta ubaguzi hakuna mstari utakaokamilika hapa, maelezo yatakuwa marefu na hakuna sheria ya namna hiyo duniani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naongoza halmashauri nilikuwa na *power* ya kutoa *exemption* kwa wazee kuititia Kamati ya Fedha. Nakumbuka Mtanzania mmoja bilionea lakini kwa sababu amejenga pale Moshi, kwa sababu ya umri wake wa uzee alikuwa anapaswa kuwa *exempted* bila kujali kipato chake. Sasa hoja yangu hapa ni kwamba, sheria iwatamke na wanawake wajane kwamba wanapaswa kusamehewa, labda iongezwe kwamba kama wana kipato, lakini kutowatambua wanawake wajane na matatizo walionayo si sahihi, ndiyo hoja yangu, sheria iwatamke kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na watu wenye uwezo duni kabisa wanapaswa kusamehewa, itamkwe na sheria hapa ione kane hivyo. Ilikaa hivyo, nitawaelewa, lakini mkijaribu kuwa-*generalize* wanawake wajane wakati wengi wa kule vijiji wanapata matatizo sitawaelewa kwa sababu tumekuja kuwawakilisha wananchi hapa, wala huwezi kumchukua Mheshimiwa Waziri ukamlinganisha na hawa wajane ninaowazungumza. Kwa hiyo, bado nasimama kwamba hoja hii iamuliwe na kura na Wabunge. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaungwa mkono.

**MWENYEKITI:** Hakuna Wabunge waliosimama, sawa, kwa hiyo hoja yake haijaungwa mkono. (*Makofii*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Japhary imeshajadiliwa, kilichokuwa

kimebakia ni kupiga kura, hatujapiga kura ikaungwa mkono au ikakataliwa. Ahsante.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. *Time* ya kufuturu imesogeasogea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy, naomba ukae tafadhalii.

Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 65 nimeshahoji Bunge na Bunge limeridhia kifungu hiki, kwa hiyo hatuwezi kurudi nyuma tena, kwa hiyo tunaendelea.

Ibara ya 66  
Ibara ya 67  
Ibara ya 68  
Ibara ya 69  
Ibara ya 70  
Ibara ya 71  
Ibara ya 72  
Ibara ya 73  
Ibara Mpya ya 74  
Ibara Mpya ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

## T A R I F A

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepititia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Act, 2017*), kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka, Kutoza, Kubadili baadhi ya Kodi, Tozo, Ada na Ushuru na kufanya Mabadiliko ya Sheria mbalimbali zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma (*A Bill for an Act to Impose and Alter certain Taxes, Duties, Levies and Fees and to Amend certain Written Laws relating to Collection and Management of Public Revenues*).

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017*  
(*The Finance Bill, 2017*) *Ulipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 imepitishwa Rasmi na Bunge leo.

Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge kwa kazi kubwa sana mliyoifanya kuanzia kipindi cha Bajeti ilipoanza mpaka leo ilipokamilihwa na hii sheria ambayo sasa inaisaidia Serikali kwenda kutekeleza kile ambacho tarehe 20 Juni, kilipitishwa. Kwa hiyo niwashukuru kwa kazi nzuri mliyofanya.

Kwa upande wa Serikali pia niwatake sasa kwamba hii sheria tunaamini kwamba baada ya kutiwa saini kama ulivyo utaratibu, mtaendelea na utekelezaji kwa kadri mlivyowaahidi Waheshimiwa Wabunge amba ni wawakilishi wa wananchi na namna bajeti mlivyoliomba Bunge hili ambalo limeidhinisha kiasi kile ambacho mlikuwa mmekionba. Niwatakie heri katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, Ijumaa, tarehe 23 Juni, 2017, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.20 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 23 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*